**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Ishirini na Mbili - Tarehe 15 Juni, 2015**

*Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 30**

**Kutolewa kwa Kibali cha Uchimbaji Kwa Watu Maalum**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) -** Aliuliza:-

Idara ya Mazingira baada ya kufanya uchunguzi kuhusiana na masuala ya mazingira, katika kuvuna rasilimali zisizohamishika kama vile mawe, kifusi na mchanga, hutoa kibali cha uchimbaji wa rasilimali hizo katika eneo husika. Kwa kuwa hivi karibuni wametoa kibali cha uchimbaji wa mchanga katika eneo liliopo baina ya shule ya Sekondari ya Fidel Castro na Pemba *Airport* na wameruhusu watu watatu tu kuchimba mchanga katika eneo hilo.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea Idara ya Mazingira Pemba kufanya ubaguzi wa kutoa ruhusa kwa watu watatu tu kuchimba mchanga katika eneo hilo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwakilishi napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Serikali kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka ambayo haswa ndiyo taasisi yenye dhamana ya kutoa vibali vya maliasili zisizorejesheka, huwa inautaratibu wakutoa vibali vya maombi ya uchimbaji mchanga au udongo kwa baadhi ya maeneo kwa miradi maalum ya maendeleo. Maeneo hayo hutolewa baada ya kufuata taratibu zote ziliopo ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi shirikishi wa wadau na kwa kuzingatia mahitaji maalum ya aina ya mchanga unaohitajika kwa ajili ya shughuli za mradi huo husika.

Aidha, uchunguzi wa kimaabara wa kuangalia aina ya mchanga au udongo hufanywa ili kubaini eneo linalofaa kuchimbwa. Kwa ujumla maeneo haya maalum hutolewa mbali na maeneo ya jumla ya uchukuaji wa mchanga au udongo

na wanaohusika kuchukua mchanga au udongo kwenye maeneo haya ni wale tu wanaohusika na shughuli za mradi unaohusika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 30 kama ifuatavyo:

Serikali kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka haijawahi wala haina sababu ya kufanya ubaguzi wa kutoa ruhusa kwa mtu yeyote kuchimba mchanga katika maeneo mbali mbali ya Visiwa vya Unguja na Pemba. Eneo linalohusika limefunguliwa kwa kazi maalum ya ujenzi wa nyumba za Jeshi la Wananchi Tanzania Zanzibar ambazo zinajengwa katika eneo la Ngerengere kwenye Kambi ya Jeshi ya Wawi.

Mkandarasi wa ujenzi wa nyumba hizo alihitaji kupata mchanga maalum ili kufikia masharti ya ujenzi wa nyumba hizo. Kutokana na hali hiyo na baada ya kufanya uchunguzi wa kimaabara wa mchanga katika maeneo mbali mbali, ndio mchanga wa eneo hilo ukaonekana kuwa unafaa kwa mahitaji ya ujenzi wa nyumba hizo za Jeshi la Wananchi wa Tanzania hapa Zanzibar. Baada ya uchunguzi huo kuthibitisha hali hiyo ndipo taratibu zote za maombi zikafuatwa na baada ya taratibu hizo kukamilika ndipo Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka ikatoa kibali kwa ajili ya uchimbaji huo.

Kimsingi mchanga unaopatikana katika eneo hilo ni wa aina ya "*fuwe*" ambao upo kama kichuguu kidogo katika eneo la Changaweni. Mkandarasi wa ujenzi wa nyumba hizo hutumia mchanga huo kwa kuuchanganya na mchanga wa kawaida kutokana na maeneo ya jumla yaliyoruhusiwa kuchukua mchanga wa Ging'ingi, Kishindeni, kwa ajili ya kupiga matofali ya kujengea nyumba hizo.

Mhe. Spika, kufunguliwa mashimo ya mchanga au udongo kwa kazi maalum sio jambo geni, kwani kuna makampuni mbali mbali ya ujenzi baada ya kufanyiwa vipimo vya kimaabara vya udongo au mchanga hupewa ruhusa kama hiyo ya kuchukua tofauti na maeneo ya jumla yaliyofunguliwa kwa watu wote. Mfano Mkandarasi wa Ujenzi ya Hosplitali ya Mkoani amepewa sehemu maalum ya eneo la Ging'ingi, mkandarasi wa maji ya Kampuni ya Serengeti amepewa eneo maalum la uchimbaji la Kiongoni na aina ya mfano huo.

Hivyo, eneo liliopo baina ya Skuli ya Fidel Castro na Pemba *Airport* limetolewa kwa kazi maalum kwa kampuni husika na mkandarasi anatumia watu watatu walioelezwa na Mhe. Mwakilishi kwa ajili ya kuuchukua mchanga wa eneo hilo kwa kazi iliyokusudiwa.

Aidha, uchukuaji wa mchanga katika eneo hilo utafungwa mara tu baada ya Mkandarasi kukamilisha mahitaji yake ya mchanga huo wa "*fuwe*". Mkandarasi huyo amepewa masharti ya kulitengeneza au kurejesha eneo hilo mara tu atakapomaliza shughuli za uchukuwaji mchanga katika kichukuguu hicho.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, hasa kuhusu kule Ging'ingi, naomba nimuulize maswali madogo sana ya nyongeza.

1) Mkandarasi sio tatizo ya kulitumia eneo hilo, tatizo lilokuwepo kwa Mkandarasi kwamba hana magari ya kutosha ya kukodi. La kusikitisha Idara yako sijui kama wizara yako kuna gari ina zuia, gari zinazokwenda kuchukua kule ni za familia moja au za rafiki, na Kampuni inaitwa Bin Aboud ndiyo inayochukua mchanga ule. Wananchi walipa kodi wa eneo lile wamekuwa wakikosa kazi, gari tatu tu au nne zinazokwenda mle.

    a) Je, unatoa kauli gani, yule Mkandarasi pale gari zake hazitoshi huchukua gari za nje kutaka kuchukua mchanga ule lakini haziruhusiwi.

    b) Mzee mwenye eneo lile maarufu au mwenye shamba lile anaitwa Abdalla Said Muhammed (Makongwe) alifungua kesi. Nataka kujua kesi ile imekwisha Mahakamani na aliahidiwa kuwa atalipwa fidia ya mchanga unaotumiwa katika shamba lake. Nataka kujua kesi ile imekwisha au inaendelea Mahakamani na mchanga unaendelea kuchukuliwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Spika, nafikiri kadhia hii nimeieleza kwa undani kabisa kitu gani kilichofanyika. Mhe. Spika, nafikiri Mkandarasi anayo haki ya kutafuta usafiri anaotaka pale anapotaka kwenda kupokea au kuchukua mchanga katika eneo ambalo ameruhusiwa kutokana pengine na bei ambayo wale ambao wanaokwenda kumchulia wamempa. Hilo nafikiri liko hivyo.

Kama nilivyosema swali hili zaidi ni la Wizara ya Misitu na Maliasili. Mimi naingia pale kama sehemu ya mdau katika kupasisha tu lile eneo wakati wa uchimbaji. Hiyo ni fikra ambayo mimi nnayo. Lakini zaidi swali hili labda alipeleke kwenye Wizara husika juu ya usahihi huo wa kutumia gari za wale waliokuwepo pale au gari ambayo mkandarasi mwenyewe amechagua kuitumia.

Hili la pili la Bwana Abdalla Said Muhammed, ambalo nalo pia amesema limefunguliwa kesi Mahakamani. Kwa kweli sina uelewa nalo, nalisikia sasa hivi.

Kama linahusika na Wizara ya Misitu na Maliasili ni bora basi likaelekezwa huko kama suala mama ili liweze kujibiwa. Mimi kwa upande wangu kama halitohusika huko naweza kulifanyia utafiti wa kuweza kulijibu swali hili kwa maandishi lakini sio sasa hivi.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa uchunguzi unafanyika wa aina tofauti za mchanga kama Mhe. Waziri, ulivyotueleza katika majibu yako. Je, uchunguzi unafanyika katika kujua kina cha uchimbaji huo wa mchanga au tuendelee kuchimba tu mpaka tukutane na maji ya bahari.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Spika, uchunguzi unaofanyika wa kucheki mchanga ni ile tunayoiita kwa lugha ya kigeni "*soil test"* pale ambapo Mkandarasi anaona udongo au mchanga uliopo hawezi akautumia pekeyake katika majenzi. Pale tunafanya uchunguzi wa kujua aina ya udongo. Lakini hili ambalo amelielezea ni kwamba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira ina miongozo na imeweka kima ambacho wanaochukua mchanga hawawezi kwenda zaidi ya hicho, kama sikosei ni kama mita tano, si zaidi ya hapo. Tunao muongozo na wanaochimba mchanga wanaotakiwa kufuata muongozo huo pamoja na kulirejesha eneo katika hali yake ya uasilia.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa sababu nchi yetu ni visiwa na kutokana na umasikini kila mahala panachimbwa sio mchanga tu lakini pia mawe, kifusi, watu wanakata tofali na mote mnafanywa mashimo na kwa sheria ni lazima kuzibwe. Kurejesha maana yake ni kushukua sehemu nyengine kutoka Visiwa hivi na kujaza kwenye hayo mashimo. Na ukiondoa hiyo sehemu nyengine maana yake ndiyo kuwa unaifanya iwe kamwe kwa sababu mbolea iko *top soil.*

Mheshimiwa, haoni kuwa iko haja ya kutafuta utaalamu mwengine zaidi kuliko huu unaofanywa, kwa sababu *at the end of the day* nchi hii itakuwa jangwa kutokana na kuichukua ile ardhi ya *top soil* na kuijaza katika mashimo ambayo yanachimbwa kwa shughuli za kibinaadamu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba kwa sababu ya maendeleo ya nchi, lakini pia kwa shughuli zetu za kibinaadamu za majengi na nyengine tunahitaji kuchukua vifusi, mchanga na mawe katika maeneo mbali mbali. Tunasema kwamba katika muongozo wetu ni lazima maeneo haya na sasa hivi kwa kweli imo ndani ya Sheria ya Mazingira

mpya ambayo tumeipitisha hapa. Mchukuaji wa kifusi au udongo anatakiwa kulirejesha eneo lile katika uhalisia wake.

Mhe. Spika, ni kiri kwamba sio rahisi kulirejesha eneo katika hali yake ya uwasilia likawa *flat* kama lilivyokuwa mwanzo. Mfano mzuri katika eneo la Uwandani kikawaida wale wanaochimba mchanga huwa wanatowa ile *top soil* ya juu kwanza huwa wanaiweka pembeni halafu ndio wanachimba au wanaochimba matofali. Sasa kinachofanyika katika maeneo kama hayo sio kwenda kuchukua udongo katika maeneo mengine.

Unachukua ile *top soil* ambayo ilitolewa ukairejeshea pale katika eneo na baadae ukapandisha miti. Wataalamu wanatwambia unapopanda mimea katika maeneo haya basi uoto wa asili ule unasababisha pia eneo kujirudi katika hali yake. Linaweza kuthibitika katika maeneo ambayo tayari yamefanyiwa kajaribio kama katika eneo hili la Uwandani. Lakini sio rahisi kwamba tukachukue eneo jengine tuje kujaza pale, huwa haifanyiki hivyo.

**Nam. 53**

**Kupoteza Kiwango kwa Nyasi Bandia za Uwanja wa Gombani.**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) -** Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla kuuliza swali hili kwanza nitoe pongezi za dhati kwa ndugu zetu, rafiki wa kweli watu wa Jamhuri ya China kwa jitihada walizochukua kuhusu uwanja wa Mau hivi sasa na jitihada hizo tunaziona. Tunashukuru kwa hilo na tunaishukuru serikali vile vile kwa jitihada hizo.

Uwanja wa Mpira wa Gombani ni mmoja kati ya Viwanja viwili vya michezo vyenye hadhi ya kitaifa na Kimataifa hapa nchini. Kwa kuwa uwanja huo tayari umeshawekwa nyasi bandia ambazo ni ghali sana na kuna taarifa kwamba nyasi hizo hupoteza kiwango pamoja na kuchakaa kama zikikosa kuchezewa angalau mechi mbili kwa siku, jambo ambalo kwa uwanja wa mpira wa Gombani limekosekana kabisa.

a) Je, taarifa hizo ni za kweli.

b) Kama ni za kweli, kuendelea kuunyima mechi uwanja huo si kuzifanya nyasi hizo zichakae, ziharibike pamoja na kushindwa kabisa kuhimili mikiki ya mchezo huo.

**Mhe. Naibu Waziri Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Umaduni, Utalii na Michezo, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 53 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli Uwanja wa Gombani ni moja kati ya viwanja viwili vya michezo vyenye hadhi ya kitaifa na Kimataifa na tayari kumeshawekwa nyasi bandia. Baada ya kueleza hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ufuatavyo:

a) Mhe. Spika, sio kweli kwamba nyasi bandia hupoteza kiwango na kuchakaa kama zitakosa kuchezewa angalau mechi mbili kwa siku.

b) Mhe. Spika, tafauti iliyopo kati ya uwanja wenye nyasi bandia na wenye majani ya kawaida ni kwamba wenye nyasi bandia unahimili kuchezewa mechi nyingi na kila unapochezewa vipira vinavyotiwa kwenye uwanja huo ndivyo vinavyozidi kushindilika na kuimarisha uwanja huo.

   Kutokana na jibu langu napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi, kwamba kusita kuchezewa uwanja huo hivi sasa hakutozifanya nyasi zilizowekwa katika uwanja huo kuchakaa na kushindwa kuhimili mikiki ya michezo hiyo.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri yenye ukweli ndani yake.

Mhe. Spika, mbali ya uwanja wa Gombani Pemba kuwekwa nyasi bandia na kuwa katika hali ya uzuri. Lakini kuna ujenzi ambao umeanza katika uwanja ya Mao Tse-Tung. Nichukue fursa hii pia kuipongeza Serikali katika ujenzi wa uwanja huo. Swali langu ni kwamba:

a) Je, ujenzi wa ule uwanja wa Mao Tse-Tung utawekwa nyasi bandia ambazo zinauwezo wa kuhimili kuchezwa mechi nyingi zaidi au utawekwa nyasi za majani ya kawaida.

b) Ujenzi huo uliokwisha kuanza kujengwa utategemea kumalizika mwaka gani.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, nakushukuru na naomba kujibu Maswali mawili ya Mhe. Nassor (Jazira) Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Rahaleo maswali yake kama ifuatavyo:

Katika ujenzi ambao umeanza katika uwanja wa Mao Tse-Tung kitu ambacho kinaendelea hivi sasa ni matayarisho ya ujenzi na yatakapomalizika kutakuwa na viwanja viwili vya mpira wa miguu ambavyo vyote vina majani bandia. Kwa hivyo, asiwe na wasiwasi hakutakuwa na majani haya ya kawaida kutakuwa na majani bandia kama ambavyo yako katika Uwanja wa Amani na kama yale ambayo yapo katika Uwanja wa Gombani. Ujenzi tukijaaliwa unategemewa rasmi kuanza kwa kasi kubwa kuanzia mwezi wa Februari, tukijaaliwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 na kama tunavyowajua wenzetu wa China wakianza kazi huwa wanaanza kwa kasi kubwa na ari kubwa na nguvu kubwa, kwa hivyo, tunategemea baada ya muda wa miezi 6 hivi watakuwa wametukabidhi kiwanja chetu kuanzia hapo.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kabla sijauliza swali Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Je, Mhe. Naibu Waziri, huoni kuchelewa kwa kumaliza njia ya kukimbilia Uwanja wa Gombani inadhoofika michezo yetu Kisiwa cha Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi wa Viti Maalum ninajua kwamba ni mwanamichezo ukiwa uko Kisiwa cha Pemba, lakini kuhusu Uwanja wa Gombani kuchelewa kuweza kumaliza njia ya kukimbilia kama mnavyojua karibuni tu tulikuwa na mvua za masika lakini sasa hivi mafundi wapo na wanaendelea na kazi na tunategemea miezi ijayo 2016 takriban tutamaliza uwanja ule.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, swali la msingi limehusu Uwanja wa Gombani, kwa vile wananchi wa Pemba wanapenda sana mpira wa miguu kiasi ambacho kimetoa wachezaji wazuri sana wa kimataifa akiwemo Thomas Thomson Tohoye akichezea Miembeni huyo, Nassor Said Cholo yuko Simba hivi sasa, Khamis Gopi mlinda mlango wa Taifa ya Zanzibar, Khamis Mafua yuko Arabuni anacheza mpira wa kulipwa, Willium John Mngazija alikuweko timu ya Taifa. Je, swali liko hapa, kuendelea kuuacha uwanja ule haioni Serikali kuwa inapoteza vipaji vya wachezaji na kuacha kuwa hautumiki kwa mechi za kimataifa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Serikali kwa sababu hata Rais wa Zanzibar na yeye alikuwa ni mwana michezo. Sasa nataka nikuhakikishie Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inawajali

sana wale wote waliokuwa ni waasisi na wanamichezo wa zamani. Mheshimiwa, nataka nikuhakikishie karibuni tu tulikuwa nao wanamichezo na kwa kweli Wizara tukazungumza nao na wakaweza kuipa maelekezo wizara jinsi gani ya kuweza kukaa na wanamichezo wakongwe ili kuendeleza michezo kwa vijana wetu na kuwapa maelekezo zaidi ili kushinda kwenye mechi zetu ambazo vijana wetu wanacheza nchi mbali mbali.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2015/2016 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea tunao wachangiaji watatu kabla ya kumwita Mhe. Waziri. Nao ni Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma pamoja na Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Tuanze kumsikiliza Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, afate baadae Waziri Haroun.

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kwa asubuhi hii ya leo kuweza kuchangia mawili matatu katika wizara yetu hii muhimu na nyeti. Mhe. Spika, sina budi vile vile kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuweza kukutana hapa pamoja na kuendelea na shughuli zetu kama ambavyo ilikuwa tumejipangia.

Mhe. Spika, mimi sina mengi sana ya kuzungumza katika Wizara hii hususan ilivyokuwa ni wizara moja kati ya wizara mbili ambazo tunazisimamia na kwenda nao katika utekelezaji wetu wakila siku. Lakini nilikuwa na maongezo tu kati ya yale ambayo tulikisha kuyaelezea katika ripoti yetu pamoja na msisitizo wa baadhi ya mambo.

Mhe. Spika,vile vile, ninamshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kushirikiana pamoja ndani ya kipindi cha miaka miwili na nusu na hatimae sasa hivi tunafikia tamati ya kamati hii kuendelea na kazi tukiwa tayari kama kamati tumekwisha kutengeneza msingi mzuri, msingi imara ili kwa wale ambao watakuja kuendeleza kamati hii waweze kushika na kuendelea vizuri na utaratibu wa kusaidiana katika wizara hii na kundosha baadhi ya changamoto ambazo zimebakia katika wizara hii.

Mhe. Spika, wizara hii ni wizara kubwa, ni wizara ambayo inagusa wanajamii kwa ujumla wao. Pamoja na mambo mengi ambayo tayari tumekwisha kufanikiwa kuyaweka katika *position* nzuri, lakini pia kwa vile tunakabiliwa na mwezi mtukufu wa Ramadhan, Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza

kuwatakia kheri ya Ramadhani njema waislamu wote ambao watakwenda kufunga mwezi wa Ramadhani nikiwemo na mimi ili Mwenyezi Mungu atupe wepesi katika kufunga mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Lakini pamoja na yote hayo bado kuna baadhi ya maeneo Mhe. Spika, yana tatizo la maji ndani ya maeneo yetu. Ningewaomba, pamoja na mipango mizuri na mikakati ambayo inaendelea katika wizara hii kwa kuwa na uhakika nayo ningeliwaomba katika kipindi hiki cha Ramadhani yale maeneo ambayo yana matatizo ya maji wajipange kuhakikisha kwamba wananchi wanapelekewa maji katika utaratibu wetu ule ule tuliouzoea ili wasiweze kupata usumbufu katika suala zima la kupata huduma hii muhimu ya maji.

Lakini nikiondoka hapo Mhe. Spika, naomba vile vile Mhe. Waziri. atakapokuja hapa anisaidie, pamoja na maeneo mengi ambayo yanapata maji ndani ya Zanzibar yetu na ndani ya maeneo yetu ambayo tunakaa siku hadi siku na pamoja na changamoto tuliokuwa tunakabiliana nazo, ningeliomba basi kufahamu katika *block No.* 10 Michenzani kuna tatizo gani linalosababisha hata ikabidi ngazi ya kwanza na ya pili watu wanapata maji, lakini hii ngazi ya mwisho huku ambayo iko karibu na Madema ngazi ile ina matatizo ya maji. Ningeliomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie ni sababu gani ya msingi inayosababisha eneo lile kila siku inayokwenda kwa Mungu na kipindi chote hiki bado tatizo la maji halitatuki katika eneo lile na maeneo mengine kwa ujumla wake.

Mhe. Spika, lakini nikiondoka hapo vile vile kumuomba na kusisitiza kwa mara nyengine Mhe. Waziri, lile eneo la ile nyumba ambayo iko pale Forodhani palipokuwa na *custom* ya zamani, nyumba ile kila kukicha hali yake inaashiria kuwa ni mbaya zaidi, naomba juhudi za dharura zichukuliwe ili athari isije ikatokea katika eneo lile.
Nikiondoka hapo Mhe. Spika, ninakuja sasa katika eneo la Dimani. Mhe. Spika, ningelimuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie wale wananchi wa Fumba ambao wameomba kuongezewa eneo ili waweze kutawanyika zaidi kuweza kuishi kwa nafasi zaidi na maombi yao wameyaleta katika wizara yako sasa hivi zaidi ya mwaka wa tatu, lakini hawajajibiwa naomba nifahamu, je tatizo ni nini na kitu gani kimekwamisha na kama hakuna jambo lolote ambalo limekwamishwa, kwa nini mpaka leo wananchi wale wanakwenda wakirudi bila ya kupewa mustakbali wa kuweza kuongezewa eneo ambalo wanataka kufanya makaazi ya kukaa wananchi wenyewe wanyonge ili kuendesha maisha yao.

Jengine Mhe. Spika, ilikuwa vile vile namuomba Mhe. Waziri, bado tungali tuna matatizo ya mafuta katika maeneo yetu ya miji ya Zanzibar na zikiwemo taarifa ambazo ziliwahi kuja kusomwa hapa katika Baraza inaonekana bado pamoja na tatizo la meli linaloleta mafuta yale, lakini pia tuna matatizo ya huduma ya

uhifadhi wa mafuta yale bado ni tatizo katika nchi yetu. Ningeliomba sana na pamoja kwamba tumeelezea katika ripoti yetu tuweze kuangalia uwezekano wa kuweza kuangalia watu au *investors* ambao wanaweza kutusaidia eneo hili la kufanya *storage* ya mafuta tukawa na mafuta ya uhakika zaidi katika visiwa vyetu vya Zanzibar, ningeliomba basi kama wenzangu ambao walikwisha kuchangia kuna wawekezaji wa nje ambao tunawakaribisha, lakini na wawekezaji wa ndani vile vile kama ambavyo ripoti yetu ilikuwa inazungumza tungeliomba wapewe kipaumbele.

Mhe. Spika, kuna muekezaji ambaye ni mzalendo amekwisha kupata eneo katika maeneo ya Bumbwini kule au Pwani Mchangani amekwisha kujitolea kuboresha eneo lile hadi amefikia kutumia pesa zisizopungua shilingi bilioni moja takriban kwa ajili ya matayarisho, kwa ajili ya eneo hili ambalo litaweza kutumika kwa muekezaji yeyote ambaye ataweza kuja hapa na kufanya utaratibu huu wa kuwekeza katika kuweka *storage* ya mafuta, basi muekezaji huyu naomba aangaliwe ikiwezekana apewe kipa umbele ili katika maeneo ambayo yatakuwa yanaangaliwa kupewa kipa umbele katika suala zima la kuwezesha kuweka *storage facilities* katika nchi yetu ya Zanzibar ili tuondokane na tatizo hili la mafuta ya mara kwa mara ambayo yanatokezea ningeomba muekezaji huyu aangaliwe na hili eneo liende likaangaliwe na hatimaye ikiwezekana eneo lile liweze kupewa kipa umbele ili muekezaji yule kwa wawekezaji ambao watakuja hapa,waweze kutumia eneo lile na eneo lile liweze kuwasaidia Wazanzibari kwa mustakbali wa kuhakikisha kwamba suala hili la mafuta linapatiwa ufumbuzi na kuadimika adimika kwa mafuta kila mara katika visiwa vyetu linakwisha.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, atakapokuja hapa ninaomba kwa vile unayo taarifa ya muekezaji huyu utusaidie taarifa, ni sababu gani inayosababisha mpaka dakika hii kuna baadhi ya mambo yanakwama kwama na muekezaji huyu hajapewa ruhusa ya kuweza kuendelea kufanya shughuli zake.

Jengine Mhe. Spika, ningelimuomba Mhe. Waziri pamoja na mipango makini ambayo ipo tayari na tunakuja nayo na kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba Zanzibar, lakini ningeliomba kujua Serikali ina mkakati gani kwa nyumba ambazo tayari tunazo katika maeneo yetu hizi nyumba za maendeleo zote ambazo zimejengwa na muasisi wetu Mzee Abeid Amani Karume ili tuone ni namna gani nyumba hizi kwa sasa zinafanyiwa ukarabati au zinavunjwa na kujengwa upya ili wananchi wetu waendelee kutumia matunda ya nchi yetu ya Zanzibar.

Baada ya Maelekezo hayo Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo mengi nilikwishakuyasema katika ripoti na mengi na tumekwisha kuelekezana katika wizara mimi niwatakie kila la kheri kama kuna tatizo lolote ambalo wizara ilikwaruzana na kamati yetu tunaomba radhi na tunawaomba kwamba sote ni

binaadamu, binaadamu yeyote ana mapungufu, kwa hivyo, tunaomba tuwe pamoja na tushirikiane kwa pamoja na yale ambayo kamati iliyaasisi waendelee nayo ambayo yana faida na nchi yetu pamoja na wizara yao na yale ambayo yana matatizo tunaomba watuachie wenyewe.

Baada ya Maelekezo hayo Mhe. Spika, kwa niaba yangu, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Mhe. Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango mdogo kwa Wizara hii muhimu sana. Lakini kwanza niitaje *title* yangu hasa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, uwezeshaji uko kwa Mhe. Bi. Zainab, maana yake uliponitaja Waziri wa Uwezeshaji ananitizama, lakini niliwahi kuifanyia kazi wizara hii.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, ninamshukuru sana mawaziri kumpongeza yeye pamoja na timu yake yote ya wizara hii muhimu sana kwa nchi yetu, lakini nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutengeneza timu nzuri ya wizara hii inayoongozwa na Mhe. Waziri Ramadhan Abdalla Shaaban. Kwa kweli nilichofanya nisimame hapa Mhe. Spika, dunia isingenifahamu na wizara hii isingenifahamu lakini hata na wananchi wa Jimbo la Makunduchi wasingenifahamu. Kwa hivyo, nitangulize kwa furaha yangu kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi tunaunga mkono hoja hii asilimia 100.

Mhe. Spika, Makunduchi tulikuwa tuna matatizo makubwa sana ya maji na baadhi wakaitumia *platform* ile ya tatizo la maji miongoni mwetu wakajenga hoja mbali mbali *is if* kwamba Serikali imeshindwa. Lakini Mhe. Rais alipofanya ziara kule katika Jimbo la Makunduchi, akapita katika maeneo mbali mbali na akaahidi kabisa kwamba tatizo la maji jimbo hili litakuwa ni historia. Mhe. Spika, muungwana ni vitendo, Rais wetu anapoahidi anatekeleza na Mhe. Waziri, alifanya ziara maalum kule jimboni na wananchi wakamuuliza hebu tueleze habari ya maji katika jimbo letu, akaeleza tangi hili limeagizishiwa Uingereza na ninakuahidini kwamba mtaletewa tangi jipya litakuja kufungwa. Mhe. Spika, hivi ninavyozungumza sasa hivi faraja ile sasa imeleta zahma kubwa kwa sababu tangi limeshafungwa maji yanatoka kwa nguvu sana mabomba yanapasuka.

Sasa Mhe. Waziri, umenitatulia tatizo katika jimbo letu na hata wale waliokuwa na maneno mengi sasa hivi *Alhamdulillahi* wamenyamaza kimya, wale wakorofi korofi wa kule Makunduchi, *Alhamdulillahi* walikuwa wanasema tangi hili litatoka Sweden, sijui litatoka wapi, sasa hivi maneno yote yamekwisha Mheshimiwa

tunatumia maji yetu *Alhamdulillahi* yameenea kila mahali mpaka vijijini. Kila siku ninapokea simu ninaambiwa kwamba mpaka sasa kuna tatizo la mabomba kupasuka.

Hii ina maana kwamba sasa hivi kwamba maji yetu yanafika sehemu mbali. Isipokuwa Mheshimiwa, nina ombi moja kwa niaba ya wananchi hawa wa Jimbo la Makunduchi. Maji haya mazuri na tumeshaunganisha kisima kimoja tu mpaka sasa hivi kuna visima vitatu pale. Kuna kisima kile kilichochimbwa na *Ras al Khaimah* ambacho nadhani bado hakijaunganishwa na tangi lile ili kuongeza nguvu, kuna na kisima ambacho tunatarajia sio kisima lile pango la Mywambiji litakuja kuunganishwa hivi karibuni, kwa sababu vijana wangu wanafanya kazi sana pale wanachimba mtaro katika mazingira magumu kidogo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ninakuomba sana tuunganishe nguvu zetu sote ili kuhakikisha kwamba kisima kile cha *Ras al Khaimar* nacho tunakiingiza kwenye utaratibu wa kuunganisha maji yale yaingie kwenye tangi kubwa.

Mhe. Spika, lakini pia ninamuomba Mhe. Waziri, kwamba ile kazi ambayo inafanywa na vijana ambao *Alhamdulillahi* wana furaha kubwa isipokuwa wanaomba tu Mhe. Waziri, mwezi wa Ramadhani unaanza basi jicho la rehma liwaone *Inshaallah* vijana wale wanaofanya kazi ya kuchimba mitaro ile.

Mhe. Waziri,  nina ombi jengine vile vile katika wizara hii, maji yetu zamani yalikuwa yanafika mpaka kule pwani, na pwani sasa hivi kule sio pwani baharini pwani ya kule Kigaeni kumejengwa nyumba nyingi sana sasa hivi watu wengi wamechimba chimba visima, lakini kwa sababu tuko karibu na bahari tunaomba sana Mheshimiwa maji haya yawezeshwe, mabomba yalikuwepo, lakini bahati mbaya sasa hivi hatuyaoni yalipokwenda hatuyajui. Lakini ingefaa kama Wizara ya Maji kupitia kwa Mkurugenzi wake na timu yake ambao ni watu wazuri sana. Mimi nasema Mhe. Waziri, umebahatika unawatendaji wazuri sana, sitaki kumtaja mmoja mmoja lakini nianze kwa Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote *you have a very good team*, mimi nina hakika kwamba wakilisimamia jambo hili basi tutafanikiwa vizuri.

Mhe. Spika, lakini pia niombe kwa Mhe. Waziri, baada ya juhudi hizo ambazo zitafanyika za kusaidia kupatikana maji maeneo ya pwani ambapo nyumba zetu ziko kule nyingi na wananchi wengi wamejenga kule kama ni mji mpya, kuna jambo tumelifanya kule tunaomba *ZAWA* tushirikiane. Tumewahi kushirikiana hapo mwanzo visima ambavyo tulichimba wakati ule wa matatizo ya maji, wakatusaidia utaalamu isipokuwa ni vichache vilifanyiwa utafiti huo, kwa hiyo, na maji yale yana ubora wa kiasi gani. Mhe. Spika, ombi la wananchi wa Jimbo la Makunduchi tunaomba visima vile vyote tulivyochimba sisi wenyewe basi wataalamu wako waje wavitizame na watizame maji yale kama ni salama kwa

matumizi ya binadamu, na kama kuna matatizo watwambie mapema kabla haijaleta athari kubwa.

Mhe. Spika, nashukuru sana na nitashukuru sana kama hili la kuangalia maji haya kama tutalifanyia haraka kidogo, kwa sababu wananchi ndio wanaendelea kutumia maji yale yasije yakaleta athari nyengine.

Mhe. Spika, jengine ambalo naomba nitoe pongezi ni suala zima la umeme, *Alhamdulillah* Makunduchi sasa hivi karibu maeneo yote yanapata umeme. Kwa hivyo, huwezi kusema sasa tuko kijijini au tuko mjini, ni sawa sawa na Mjini mahali popote kwa sababu kila kipembe umeme unapatikana. Naomba tu Mheshimiwa, ule utaratibu wa kuwakopesha wafanyakazi umeme wananchi wetu basi naomba utaratibu ule uendelee, kwa sababu umewasaidia wananchi katika suala zima la kupata huduma hii muhimu ya umeme.

Mhe. Spika, lakini pia naomba kidogo Mheshimiwa, tusaidie nina ombi maalum, mimi leo nakuja na maombi na pongezi tu. Tumepata habari kwamba kuna nyongeza ya visima 50 vya *Ras al Khaimah*, sina hakika lakini wewe mwenyewe waziri utanithibitishia hayo. Na tuna mpango wa kujenga tangi moja jipya la maji kule Mtende, na *Alhamdulillah* nakuthibitishia kwamba kazi hiyo inaendelea vizuri.

Sasa nina ombi kwa wananchi wa Makunduchi hasa Kijiji cha Kajengwa wana kisima chao cha siku nyingi kule Mheshimiwa. Mimi naomba Mheshimiwa, tufanye juhudi maalum katika awamu hii ya pili ya visima 50 basi na wananchi wa Kajengwa na wao tuwapatie tangi kama lile la Mtende wala hawana makubwa wakataka kama lile ambalo liko pale Uwandani. Tujitahidi wananchi hawa wa Kajengwa na wao wameshakaa na kisima kile muda mrefu sana, wanakushukuru Mheshimiwa na wanakupongeza sana kwa kazi nzuri ambazo unazifanya na wanakutakia kila la kheri na kutaka mfungo wa kheri wa Ramadhani *Inshaallah* wewe pamoja na Naibu wake na timu yako.

Mhe. Spika, mimi sina zaidi ila ni kupongeza na kutakia kheri waziri, kiukweli muadilifu amefanya kazi nzuri. Nimpongeze sana Mhe. Rais kwa ahadi yake ya kutuletea maji kule Makunduchi sasa hivi wananchi wanafurahia maji hayo na mwezi mtukufu wa Ramadhani *Inshaallah* hawatokuwa na shida yoyote. Baada ya hayo nitamuomba Mhe. Waziri, tuje tuzindue rasmi maji yale tufanye sherehe kubwa kwa sababu suala la maji ndio uhai, kwa hiyo, tuje tufanye sherehe Mhe. Waziri, ili tusherehekee na wananchi wa Jimbo la Makunduchi. Baada ya hayo naunga tena mkono hoja hii Mheshimiwa, Mungu awabariki na *Inshaallah* naomba Waheshimiwa wenzangu wote tuunge mkono hoja hii ili ipite bila ya matatizo. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Tunataka kuanza majumuisho mara baada ya majumuisho tupitishe mafungu ya wizara hii, kwa hiyo, wale wote Waheshimiwa Wajumbe waliko nje basi waje waingie ndani tumalize shughuli hii. Naomba sana watendaji basi wawatafute Waheshimiwa Wajumbe, warudi ndani ili tumalize kazi hii. Watendaji fanyeni hiyo kazi kuwaita Waheshimiwa Wajumbe walioko nje.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, ahsante kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutuwezesha kutukanisha hapa asubuhi hii tukiwa wazima wa afya na salama. Lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mchango mdogo sana, kwa sababu sitopenda nichangie sana ili nipate nimpe nafasi Mhe. Waziri, ili aweze kupambanua yale yote ambayo tumeyakusanya.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze tu katika mchango wangu kwa hoja ambayo imeletwa na Mhe. Kazija Khamis Kona, kuhusu suala la hoteli ya kuziba maji yasiende kwa wananchi ndani ya maeneo ya Kijiji cha Matemwe Kigomani.

Mhe. Spika, naomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi wa Viti Maalum kwamba suala hili tumelipata kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji baada ya kulipata suala hili tumelifuatilia pamoja na mimi mwenyewe. Na vile vile tukapata ripoti zaidi kupitia kwake yeye Mhe. Mwakilishi wa Viti Maalum pamoja na Mhe. Abdi Mossi Kombo na baada ya kuipata taarifa hiyo, tukafanya ziara ya pamoja mimi Naibu Waziri pamoja na Mhe. Abdi, pamoja na Mhe. Kazija tukafatilia katika maeneo hayo na katika kufatilia huko tukashirikiana pamoja na wananchi ili kuweza kujua ukweli wa tatizo hilo.

Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi mwenyewe nimekaa na watu wangu wa Mamlaka ya Maji na tukalifuatilia tatizo hilo na baada ya kulifatilia hatukugundua kama kweli wawekezaji wameyaziba maji hayo, isipokuwa tu tulichokiona katika maeneo hayo ni kwamba kulikuwa na tatizo la uzibaji wa mabomba yetu ambayo ilikuwa inaelekeza maji katika maeneo ya Kigomani. Lakini pia kwa kazi nzuri ambayo wameifanya Mamlaka ya Maji, basi tumefanikiwa kulindoa tatizo hilo na wananchi hao kwa muda mdogo wamefanikiwa kupata mahitaji hayo ya maji na katika kumbukumbu zangu ilikuwa ni kipindi ambacho kilikuwa kinakaribia kabisa na mwezi huu mtukufu wa Ramadhani wa mwaka uliopita.

Lakini tumefanikiwa wananchi hao kuwasaidia katika kulitatua tatizo hilo na pia nimuombe sana Mhe. Kazija pamoja na Mhe. Abdi Mossi ambao ni wawakilishi wanaohusiana na maeneo hayo, basi yanapotokezea matatizo kama hayo washirikiane na Mamlaka ya Maji. Aidha, na wizara yangu kupitia Naibu Waziri au Waziri kwa sababu tuko hapa kwa ajili ya kuyashughulikia matatizo ya

wananchi. Lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wote wa Zanzibar wanapata huduma hii ya maji safi na salama. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa hawa wawe karibu nasi na washirikiane nasi kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika, vile vile, kuna suala la Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Mtambwe nae pia kazungumzia kuhusiana na suala zima la matatizo ya maji katika maeneo ya Mtambwe Kusini kulikuwa na kisima ambacho kilikuwa kinatumia *pump* lakini *pump* hiyo imefunguliwa na ikawekwa *pump* nyengine ndogo. Namuomba Mhe. Mwakilishi, aelewe kwamba ni kweli katika kisima hicho ilikuwepo *pump* ambapo *pump* hiyo ni kweli ilikuwa ina matatizo na Mamlaka ya Maji kupitia tawi letu la Pemba baada ya kupata ripoti hiyo wamefatilia na wakenda katika kisima hicho. Na kweli *pump* iliyokuwepo imefunguliwa lakini imefunguliwa kwa sababu maalum, kwamba *pump* hiyo ilikuwa tayari imeshachakaa na tayari imefanya matatizo kwa sababu ilikuwa na ina-*shot* ambayo haiwezi kuhudumia kisima kile.

Mhe. Spika, ni kweli tumefunga *pump* ambayo ilikuwa haikidhi, lakini pia kwa nini tukafanya hivyo? Ni kwamba kulinga kulinganisha na muda huo *pump* iliyokuwepo na tukataka wananchi hao wafaidike na huduma hiyo kwa vyovyote itakavyokuwa lakini tuhakikishe kwamba tunafunga *pump* ambayo inaweza kuwahudumia wananchi hao. Kwa hiyo, tumefunga *pump* nyengine ni kweli huduma hiyo kwa sasa hivi haitoshelezi na wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji basi tayari imejiandaa kuongeza kisima chengine katika maeneo hayo na kuhakikisha kwamba wananchi hao wa maeneo ya Mtambwe ya Kusini wanapata huduma ya maji safi na salama ipasavyo. Nimuombe Mhe. Mwakilishi, avute subra wizara yangu inalisimamia suala hilo na itahakikisha kwamba tunaliweka katika hatua inayofaa kwa ajili ya kuwatumia wananchi.

Mhe. Spika, vile vile, kazungumzia kuhusu suala hilo hilo la maji maeneo ya Mtambwe ya Kaskazini. Mhe. Spika, ni kweli kulikuwa na matatizo maeneo ya Mtambwe Kaskazini katika kisima cha zamani ambacho kipo. Ni kweli palikuwa na kisima cha zamani ambacho kisima hiki kuna kipindi fulani kilitaka kusafishwa na Mamlaka ya Maji baada ya kupungua nguvu ya maji, kwa hiyo, tukahisi kwamba ipo haja ya kukifanyia kazi na kwenda kukisafisha kisima hicho. Ni kweli wenzangu wa Mamlala ya Maji wanalifuatilia tatizo hilo na wakienda kwenye maeneo ya kisima hicho na baada ya kufanya jitihada za kusafisha kisima hicho, kwa bahati mbaya sana *pump* iliyokuwemo katika kisima hicho ndani ya usafishaji *pump* hiyo imeingia ndani na *pump* hiyo haikupatikana na kisima hicho kikashindikana kutumika.

Lakini kwa jitihada za wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji Pemba kilichofanyika ni kuchimba kisima kingine. Kimechimbwa kisima chengine kipya na kisima hicho tayari kinatoa huduma nzuri ya maji kulinganisha na kisima

kilichokuwepo, basi kisima hiki kinatoa huduma ya maji vizuri zaidi kuliko kisima kile ambacho kilichokuwepo katika kipindi hicho cha nyuma.

Vile vile, kulikuwa na tatizo kidogo ambalo lilikuwa linatusumbua la umeme mdogo katika kisima hicho kipya. Nataka nimthibitishie Mhe. Mwakilishi, kwamba tayari ndani ya kisima hicho tunapata umeme wa kutosha na huduma hiyo kwa sasa hivi inapatikana vizuri zaidi kuliko pale awali ambapo ilikuwa wananchi wanasumbuka kutokana na kisima hicho kikongwe ambacho kilikuwa kinatoa huduma hiyo, lakini ilikuwa haitoshelezi huduma ambayo ilikuwa inatolewa na kisima hicho kikongwe.

Mhe. Spika, pia, kuna hoja ya Mhe. Abdi Mossi Kombo ya maeneo ya Kijini kwamba maji hayapatikani.

Mhe. Spika, mimi nataka nimuhakikishie tu Mhe. Mwakilishi, kwamba huduma hii tayari inapatikana na labda alipoleta hoja yake ilikuwa bado hajatembelea katika hayo maeneo, lakini kwa sasa hivi huduma hii katika maeneo ambayo aliyoyataja basi tayari huduma hii inapatikana. Aidha, ikiwemo hiyo Kijini wenyewe, Mbuyutende na maeneo mengine ambayo yako katika maeneo hayo, basi huduma hii sasa hivi inapatikana vizuri sana. Na ningemuomba zaidi aipongeze serikali kupitia wizara yangu pamoja na Mamlaka ya Maji kwa jitihada ambayo imefanya ndani ya kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani basi ajue wananchi hao watafaidika na huduma hiyo. Tayari sasa hivi wanaanza kufaidika lakini katika kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani watanufaika zaidi kwa sababu hiyo huduma tayari tumeshaisambaza na wananchi wanaanza kufaidika na huduma hiyo.

Namuomba sana ashirikiane na sisi na wananchi wake ili watumie huduma hiyo kwa salama, lakini pia ningemuomba sana kwamba huduma hii inataka uchunga, huduma hii ahakikishe kwamba inataka ulinzi wa nguvu kwa sababu tatizo linalotusumbua kupitia mamlaka yangu ya maji ni kwamba wapo baadhi ya wananchi huwa wanajiungia maji wenyewe kinyume na utaratibu, hili jambo linatusumbua sana, kwa sababu wanazitoboa miundombinu zetu bila ya kuwatafuta wataalamu, bila ya kufika mamlaka husika ambayo inahusiana na masuala yale.

Kwa hiyo, hili suala linatusumbua sana, tunatengeneza, tunajitahidi kuwashughulikia wananchi hawa na tunajitahidi kupeleka huduma, lakini tunapata matatizo ya aina hii kwamba wananchi wanajiunganishia huduma hii kiholela bila ya kupita maeneo ya sheria na wakaongozwa na wakatakiwa kwamba wasimamiwe huduma ile ili hii Mamlaka ya Maji iwashughulikie kwa kutumia wataalamu wake na kupata huduma hiyo kwa vizuri. Nawaomba sana wananchi na pia niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi, kwamba sisi wenyewe tuwe wachunga kama

viongozi inapaswa tuwe wachunga katika suala zima la kulinda miundombinu hizi ili huduma hii iwe ni huduma endelevu.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwamba mimi sitokuwa na mchango mkubwa, lakini naomba nimalizie suala moja ambalo limeletwa mapendekezo na Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira), vile vile na Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mussa linalohusiana na masuala ya Mji Mkongwe hususan katika masuala ya nyumba zetu zile za Mji Mkongwe. Mhe. Mussa, yeye alitaka kujua kwamba je, kuna nyumba ngapi ndani ya maeneo ya Mji Mkongwe ambazo nyumba hizi ni mbovu. Jibu: ni kwamba ni kweli zipo nyumba mbovu ndani ya maeneo ya Mji Mkongwe, lakini kwa tathmini ambayo tuliyoifanya sasa hivi tumeona kwamba ndani ya maeneo ya Mji Mkongwe kuna nyumba zisizopungua 26. Nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi, kwamba wizara yangu kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe inalisimamia suala hili na kuhakikisha kwamba nyumba hizo zinafanyiwa matengenezo haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, na pia kuna ushauri ambao umekuja kwa Mhe. Nassor Jazira, yeye alisema kwamba ipo haja Mamlaka ya Mji Mkongwe pamoja na Idara ya Nyumba kuweka vielelezo ambavyo vitaonesha nyumba hizo kuwa na alama maalum ambazo zitajitambulisha kwamba hizi ni nyumba za shirika au ni nyumba za Idara ya Nyumba na pia kuzifanyia matengenezo nyumba za Mji Mkongwe. Mheshimiwa, tunakushukuru kwa ushauri wako mzuri na wizara yangu kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe na Shirika la Nyumba ambalo litatangazwa si muda mrefu kwamba tutazishughulikia nyumba hizo na tutahakikisha kwamba tutaziweka nembo ambayo itakuwa ni nembo maalum itayozijuulisha kwamba nyumba hizi ni nyumba za Shirika la Nyumba Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hayo kama nilivyoeleza kwamba sitochangia mchango mrefu nataka nimuachie Mhe. Waziri, ili aweze kupambanua zaidi. Mhe. Spika, nakushukuru na nasema naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Ahsante. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Wakati huo huo nawahimiza Waheshimiwa Wajumbe, walioko nje waingie ndani ili tumalize kazi hii.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia na uzima wa afya nikasimama tena mbele ya Baraza lako hili tukufu kwa madhumuni ya kutoa ufafanuzi wa hapa na pale kwa ajili ya kuiwezesha wizara hii kuweza kutekeleza mambo yake katika mwaka huu unaofuatia wa 2015/2016.

Mhe. Spika, kwanza napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa michango mizuri kabisa tena yenye maana na yenye manufaa ya nchi hii ambayo Waheshimiwa Wajumbe, wameitoa katika kuzungumza madhumuni na sababu ya Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, wajumbe waliochangia kwa kueleza hoja mbali mbali katika Baraza hili ni 18, naomba niwatambue ambaye wa kwanza alikuwa ni Mhe. Marina Joel Thomas, huyu alichangia kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza lako tukufu.

2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Kazija Khamis Kona
5. Mhe. Musa Ali Hassan
6. Mhe. Hassan Hamad Omar
7. Mhe. Salim Abdalla Hamad
8. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
9. Mhe. Abdi Mosi Kombo
10. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
11. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
12. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
13. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali
14. Mhe. Nassor Salim Ali
15. Mhe. Hamza Hassan Juma
16. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
17. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Kazi na Utumishi wa Umma
18. Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Spika, vile vile, sikukosa kupata watu waliochangia kwa maandishi, aliyechangia kwa maandishi ni Mhe. Ali Abdalla Ali, Mhe. Fatma Mbarouk Said na Mhe. Hija Hassan Hija.

Hoja za Mhe. Hija Hassan Hija, zinahitaji kufanyiwa kazi pamoja na kuwa amezileta katika dakika ya mwisho. Lakini ni hoja nzuri nazo na kwa kweli zinahitaji kufuatiliwa.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba mazungumzo yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wawakilishi hapa ni lazima yazungumzwe hapa na hawawezi kuzungumza mahala pengine. Kwa sababu hili ndilo Baraza linalowakilisha wananchi wa Zanzibar, wamezungumza mazungumzo ya msingi sana. Kwa hivyo, nawashukuru sana kwa mazungumzo haya ya umahiri kabisa na kufanya kazi waliyojia kuifanya hapo walipochaguliwa kuja katika Baraza hili.

La pili, napenda nizungumze kwamba nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, wameuheshimu na wameuthamini sana utekelezaji wa watendaji wa wizara hii na ndio maana wote wamesema kwamba watendaji wa wizara hii safari hii wamefanya kazi nzuri sana. Kila aliyesimama amelitamka neno hilo na hakuna aliyesema kwamba wale hawakufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, watendaji wetu tumewapa moyo sana katika hili nashukuru sana na wameleta mafanikio. Katika kipindi hiki wizara hii imepitisha sheria nyingi sana kwa ajili ya kurekebisha matatizo mbali mbali yanayotokea katika utekelezaji wa masuala ya wizara hii. Kuna sheria zinazohusu nyumba, kuna sheria zinahusu masuala ya ardhi, kuna sheria inayohusu mafuta na pia masuala ya *ZURA* na bado mikononi watendaji hawa wanazo sheria nyengine za kufanikisha uletaji wa mafuta na mambo mengine katika nchi hii, ambayo kwa bahati hayakupata nafasi kuzungumzwa katika kipindi hiki, lakini nategemea watazileta katika kipindi kitakachofuata.

Kwa upande wa maji watendaji hawa safari hii wamefanya kazi nzuri sana na wamefanikisha malengo ya usambazaji wa maji katika maeneo mbali mbali. Mimi nawashukuru na ninawashukuru kwamba walinipa ushirikiano mkubwa sana na kuweza kufanya mambo haya vizuri kabisa.

Mhe. Spika, ile asilimia ambayo tulikuwa tuongeze katika maji wamefanikiwa nayo na nilikuwa nayo hapa ilikuwa imeeleza asilimia ngapi, lakini sitaki kupoteza wakati kuitafuta nikiiona baadae nitaizungumza kueleza kwamba mpaka sasa hivi wameshasambaza asilimia ngapi ya maji katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Kwa upande wa umeme ni kwamba katika kipindi hiki wenzetu duniani katika nchi zilizoendelea wao katika suala la usambazaji umeme nchi nyingi ziko kwenye asilimia 100, 95, 98, 99. Kwa upande wa hapa Tanzania wenzetu Bara katika suala la usambazaji umeme wamejitahidi sana, kutokana na asilimia ndogo waliyokuwanayo sasa hivi wanajitahidi, maana Bara ni nchi kubwa na vijiji ni vingi sana wako kwenye asilimia inayopindukia 30 sasa hivi kwa usambazaji umeme. Kwa Zanzibar ukichukua sensa ya watu *household* za Zanzibar ni kama nyumba moja ina watu sita, hiyo ni *average* katika sensa inavyoeleza. Ukichukua watu sita ukigawa kwa milioni moja na laki tatu ile ambayo tuliifanya sensa utakuta kwamba tuna nyumba mia nne na kitu kidogo katika Zanzibar.

Mhe. Spika, katika hizi tayari tumeshavuka asilimia 50 ya usambazaji umeme katika maeneo mbali mbali. Ni kazi nzuri inayofanywa na kwa kweli imesaidia sana kusambaza umeme kwa wananchi. Shabaha ni kwamba tufike katika asilimia mia moja kama nchi zinavyoendelea. Kwa hiyo, tunategemea kwamba kadri siku

zitakavyokwenda kwa sababu kuendesha serikali ni *system* na *system* iendelee kuwafikishia huduma wananchi katika maeneo mbali mbali ili waweze kupata huduma hizi na wao wapate maendeleo kama watu wengine wanavyopata maendeleo duniani.

Mhe. Spika, hili nalishukuru na kwa kweli tuko katika hali nzuri katika hili na jitihada inafanywa. Tukumbuke hapa kwamba umeme kwa wananchi wa Zanzibar kabla ya Mapinduzi ulikuwa haufiki hata asilimia 3, wakati alipokuja Mzee Karume hapa akajitahidi kupeleka umeme katika vijiji mbali mbali kama Makunduchi alimojenga zile nyumba tukapata angalau kwenye asilimia 5 mpaka 6 ya usambazaji wa umeme, alipokuja Mzee Aboud Jumbe na yeye akajitahidi kupeleka umeme katika maeneo yale tukapata angalau kwenye asilimia 10 ya usambazaji wa umeme, sasa tushukuru kwamba leo tuko kwenye asilimia zaidi ya 50. Kwa sababu alipokuja Mzee Idrissa Abdul-Wakili alikuta Mradi wa *NEREMCO*, kwa hivyo, umeme ukazidi kusambaa sana vijijini tukafika asilimia nzuri, sasa hivi tukawa tumeshavuka asilimia 50. Mhe. Spika, tumefanya kazi nzuri sana na tuna haki ya kujipongeza Zanzibar katika kuleta maendeleo ya wananchi hapa Zanzibar kusema kweli.

Mhe. Spika, niliona niyatangulize hayo na halafu sasa nianze kutoa ufafanuzi. Mhe Spika, hapa sijibu hoja hapa natoa ufafanuzi. Kwa sababu Wajumbe hawa wanachokitaka sio kujibiwa hoja wanachokitaka waliyoyasema yatekelezwe, hilo ndio wanalolitaka, sio kwamba wajibiwe hoja iwe kwamba umejibu hoja tu basi halafu umeondoka, isipokuwa wanayoyasema yatekelezwe. Kwa hiyo, mimi natoa ufafanuzi tu.

Mhe. Spika, kwanza Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi imetoa ushauri mzuri sana, wa kwanza umeshawahi kufanyika kwa ile *reform* ya kazi za Shirika la Umeme. Wizara imeupokea ushauri wa kamati na tayari serikali kupitia wizara yangu iliunda kamati maalum na kamati hiyo imeshawasilisha mapendekezo ya utaratibu wa kulifanyia mageuzi Shirika la Umeme, tayari hii tumeshafika hatua hii. Kamati imetoa ushauri kufuata utaratibu wa kutoa *units* za umeme kwa wafanyakazi badala ya kutoa posho maalumu. Wizara imepokea ushauri huo na utekelezaji utaanza katika mwaka ujao wa fedha.

Kamati imetoa ushauri kufanyiwa mapitio ya kodi za nyumba za serikali pamoja na mategemeo ya kuanzisha kwa Shirika la Nyumba kupelekea mapato kuongezeka. Ni kweli mapato yatokanayo na kodi za nyumba yameongezeka na inadhihirishwa na mapato yaliyoripotiwa katika hotuba yangu ya bajeti ambapo jumla hivi sasa tumekusanya shilingi 400,285,000 na tayari tumeshakusanya hadi kufikia Machi, 2015. Kwa hiyo, mapato yameongezeka ambapo kwanza kwa utekelezaji wa Shirika la Nyumba kutaongezeka zaidi na mapato na ubora wa makaazi ya

wananchi. Vile vile, kamati imeshauri wizara kulipatia ufumbuzi suala la madeni makubwa ya Idara ya Nyumba wanayodaiwa wananchi au taasisi za serikali. Jitihada zinaendelea kuchukuliwa na wizara yangu kupitia Idara ya Nyumba na Makaazi kwa kuwafuatilia wananchi na taasisi husika na pia kuwaandikia na kuwataka wasawazishe madeni hayo na baadhi yao Mhe. Spika, wameanza kusawazisha madeni hayo.

Kamati imeitaka wizara kuzingatia ukarabati wa nyumba za Kengeja na Mtemani. Hoja hii pia imechangiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Mheshimiwa, wizara hii itakachokifanya kwa mwaka ujao wa fedha kuifanyia matengenezo nyumba ya Mtemani ili iweze kurudi katika hali ya uzima na kuwa salama. Kwa upande wa jengo la Kengeja kwa kweli Mhe. Spika, lazima niseme kwamba, tunategemea kupata kwa fedha kwa ajili ya jengo la Kengeja. Kwa Mtemani tutajitahidi katika hiyo hiyo *OC* yetu kufanyia matengenezo jumba hilo, lakini kwa Kengeja tunategemea tupate fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo ya jumba lile.

Kamati imeshauri nyumba za Mazizini zifanyiwe matengenezo ili zipate kutumika na kuweka viongozi wakuu, kwani serikali inatumia fedha nyingi kuwakodia viongozi hao. Ushauri tumeupokea na tayari serikali imeanza kuchukua hatua za kuzifanyia matengenezo nyumba za Mazizini na kadri hali ya fedha itakavyokuwa nzuri matengenezo haya tutaendelea. Kadhalika shirika litakapoanza litakamilisha matengenezo ya nyumba hii.

Mhe. Spika, sasa nakuja katika hoja za Wajumbe nimemaliza za kamati. Wajumbe tunaanza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Muyuni, huyu amezungumza kwa umakini kabisa juu ya suala la ufutaji wa hati bila ya kutoa indhari.

Mhe. Spika, tunapofanya kazi ya uwaziri kwa kweli tunatakiwa tutizame sheria na tufuate sheria na hivi ndivyo tunavyofanya. Mhe. Rais wetu anatuhimiza sana kwamba nyinyi mawaziri someni Katiba kila mara na someni sheria zinazokuhusuni kila mara ili muzijue na mzifuate. Kwa hivyo, katika kutekeleza suala la kufuta ardhi tunatizama sheria, sheria inayowezesha kufuta ardhi ni Sheria Nam. 12 ya mwaka 1992, imeweka wazi taratibu za mazingira ya ufutaji wa hati ya matumizi ya ardhi, hili Waziri wa Ardhi hafungwi na kifungu kimoja wakati wa kufuta hati ya matumizi ya ardhi, ndivyo sheria ile ilivyo.

Mhe. Spika, kuna hili suala ambalo amezungumza Mhe. Jaku Hashim, suala la utoaji wa *notice*. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati amepewa hiari (*option*), ni hiari ya kutoa au kutotoa kwa *notice* kama kifungu kinavyoeleza, naomba kunukuu baadhi ya vifungu vya sheria husika, niruhusu nikisome kwa Kiingereza maana ndivyo kilivyoandikwa kama ifuatavyo:

Kifungu cha 60(1) kinasema hivi:

> *"Where the holder or a person right-fully acting on his behalf has failed over a period of two years to use for the purpose it was allocated, maintain or keep such land or buildings in proper and productive use and repair, the land described as part of the right of occupancy may be declared as idle."*

Kifungu cha 60(2) kinasema hivi:

> *"The minister may issue a notice requiring the holder to appear in person or by his agent to give reasons why the right of occupancy should not be terminated".*

Neno *"May"* maana yake ni *option,* wanasheria wamo humu ndani, hii ni *option* ambayo waziri anaweza kuitoa anaweza asiitoe. Katika suala la meizi 18 vile vile kifungu cha 60(3) kinasomeka hivi:

> *"The minister may, in his discretion, at the completion of the hearing, provide up to eighteen months during which time the interest holder must utilize the land in the manner for which it has been designated."*

Mhe. Spika, hivi ndivyo sheria inavyosema na kwa kweli sheria hii tunaifuata na kwa nini tunafanya hivi? Mhe. Spika, kuna watu wameweka ardhi miaka 12 hawajaitumia, kuna watu wameweka ardhi miaka minane hawajaitumia, kuna watu wameweka ardhi miaka 10 hawajaitumia, tena bado mtu anaweka ardhi miaka 12 unamwita unamwambia nakuongeza muda, yaani miaka 12 umekaa nayo ardhi hujaitumia bado unasema tukuongeze muda. Sasa hapa sheria hii imetoa *option* hiyo kwa sababu lazima tusiweke ardhi hivi hivi tu ikakaa bila ya kutumika kwa namna yoyote. Hiyo ndio hoja.

Mhe. Spika, hoja ya ufutaji inaweza kufanyika bila ya kutoa *notice* kwa mpewaji, sheria imeeleza wazi kuwa mwekezaji anaposhindwa kutimiza masharti juu ya ardhi aliyopewa ardhi hiyo itafutwa na kurudishwa serikalini kwa ajili ya kupangiwa matumizi mengine. Aidha, ifahamike kwamba endapo mwananchi ameshindwa kuendeleza ardhi aliyopewa kwa kipindi husika anapaswa kurudi serikalini na kueleza sababu za kushindwa. Hawaji hawa kuja kueleza sababu za kushindwa, hilo ni tatizo, wengine baadhi yao wanakuja lakini wengine hawaji, sasa wameweka tu ardhi haina kazi yoyote ya kufanya.

Vile vile, napenda kumfahamisha Mheshimiwa, kuwa lengo la wizara na serikali kwa ujumla ni kuendelezwa kwa maeneo wanayopatiwa wananchi na sio kuyaweka tu kiujanja ujanja kwa dhamiri ya kutafuta mtu wa kumuuzia. Hili

tunalikimbia kusema kweli, sio mtu aanze kuranda Ulaya huko atafute mtu wa kumuuzia ardhi huku ardhi imekaa pale *idle***,** huu ndio msimamo wa wizara yangu na ndio msimamo tunaoufuata kwa mujibu wa sheria, sio ikae tu ardhi hivi hivi *idle* haina kazi yoyote ya kufanya.

Mhe. Spika, naondoka hapo nakuja kwenye hoja ya Mhe. Kazija Khamis Kona, viongozi kuwa ni chanzo cha migogoro ya ardhi. Mheshimiwa, ni kweli kuwa wapo baadhi ya viongozi na sio wote, wapo baadhi ya viongozi wanaojihusisha na migogoro ya ardhi katika ngazi mbali mbali wakiwemo baadhi ya masheha na baadhi ya madiwani. Hata hivyo, kutokana na mikakati ya wizara yangu na kutoa elimu juu ya umiliki, matumizi, uhaulishaji na usajili wa ardhi, ninayo furaha kuliarifu Baraza lako tukufu ya kuwa hivi sasa wimbi la migogoro ya ardhi limepungua kwa kiasi kikubwa.

Hoja nyengine wananchi 12 wa Matemwe kutoridhika na fidia. Mhe. Spika, wizara yangu inapotoa hati ya uwekezaji jambo la kwanza inajiridhisha ikiwa mwekezaji amewalipa fidia wananchi aliyowakuta kwenye ardhi husika. Kwa hivyo, ile ardhi yote ya Zanzibar ni mali ya serikali, kinachostahiki kulipwa ni uendelezaji wa ardhi hiyo mfano vipando, nyumba na kadhalika. Kwa uelewa wa wizara yangu juu ya kadhia hii, wananchi hao awali walikataa fidia kutokana na mwekezaji kwa hisia kuwa ilikuwa ni ndogo. Hivyo, Wizara ya Kilimo na Maliasili ilitakiwa kufanya tathmini, uthamini wa mali ya mazao na matokeo ya uthamini huo kiwango kilishuka zaidi ukilinganisha na kile cha awali alichotaka kutoa mwekezaji, hatimaye mwekezaji huyo aliombwa kufanya mazingatio na hisani ili kiwango hicho kiwe kikubwa zaidi jambo ambalo mwekezaji huyo alilitekeleza kwa makubaliano ya wananchi.

Mhe. Spika, kwenye suala hili ukweli ni kwamba walipokuwa wanalipwa kwanza bila ya tathmini walisema hizi pesa ni kidogo tuongezwe, wakapelekwa kufanywa tathmini zikashuka. Sasa ziliposhuka mwekezaji akasema aa madhali tunatakiwa tuwafanyie hisani hawa wananchi maana hili eneo huku ni kwao lazima wafaidike na mradi huu na watafaidika zaidi na mambo mengine yatakayofuatia baadae. Kuna mtu pengine alifanyiwa tathmini ya kupata shilingi laki moja wamemlipa shilingi milioni mbili, kuna mtu wa kupata shilingi laki nne wamemlipa shilingi milioni tano, walizichukua hali kama hiyo, walifanya hiyo kazi namna kama hiyo na wako mashahidi pale Matemwe.

Mhe. Spika, kusema kweli waliridhika na fidia hizi na faida nyengine kwa ajili ya wananchi wa Matemwe inakuja, ajira zitapatikana kwa wananchi wa Matemwe, baadhi ya vijana sasa pale skuli wanaaza kupatiwa vyakula na ujenzi mwengine unaendelea, barabara hivi sasa inajengwa kule kwa ajili ya kuikomboa Matemwe

kule Kijini kuwe na njia ya kupita na nzuri kabisa kwa ajili ya kufikisha wananchi kule. Hii ndio nia ya faida tunayoipata kutoka kwa wawekezaji.

Mhe. Makame Mshimba yeye amesema tuwape mashirikiano ya upendeleo vijana wawekezaji wazalendo, hata Mhe. Mahmoud Mohammed, naye amelizungumza hili. Mhe. Spika, ni utaratibu wa wizara yangu kutoa kipaumbele kwa wazalendo vile vile kwa kulipa nguvu zaidi suala hili. Rasilimali ya sera ya ardhi imetoa mapendeleo maalum kwa wazalendo katika masuala ya uwekezaji mfano wa miradi ya wazalendo nataka niitaje hapa Mhe. Spika. *Amani Bungalows* Nungwi ni mzalendo huyu, *Smile Beach* Nungwi ni mzalendo huyu, *Mnarani Hotel* Nungwi ni mzalendo, *Natural Villa* Kendwa ni mzalendo huyu, *Sales Bungalow* Matemwe ni mzalendo, *Amani Kendwa Rocks* Kendwa ni mzalendo, *Ndame Beach In* Paje ni mzalendo, *Palm Beach In* Paje ni mzalendo, Ras Michamvi ni mzalendo, Pemba Misali Wesha ni mzalendo, *Vigor* Mangapwani ni mzalendo, *United Petrol in Group* Mangapwani ni mzalendo, hii kwa ajili ya mafuta. Hawa ni baadhi tu ya wazalendo ambao wameshapewa fursa hizo na wameshapata hati, yaani *lease* za kuyaendeleza maeneo haya, kwa bahati tu hawajatekeleza sasa hivi kutokana na tatizo la utekelezaji wa baadhi ya sheria hasa kwenye suala la mafuta.

Mhe. Spika, unajua kuna sheria ya *ZURA* lazima sasa hivi tunadhibiti masuala ya mafuta, lazima tuhakikishe kwamba mtu tunampa kwa mujibu wa sheria ilivyo ili tuweze kupima mafuta tuone kwamba mafuta yanakuja katika kiwango kinachohitajika.

Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Kazija Khamis Kona, Mhe. Abdi Mosi Kombo na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, wamezungumzia kuhusu mwelekeo wa ukuaji wa uendelezaji wa mji wa Zanzibar pamoja na sababu zinazopelekea wananchi kujenga kiholela. Kwa ufupi sababu kubwa ndizo zilizokuwa zikichangia ujenzi holela wa Zanzibar:

1. Kukosekana kwa mpango wa maendeleo *master plan,*
2. Kuwa na udhaifu katika mfumo wa utoaji vibali vya ujenzi na udhibiti wake, na
3. Migongano ya taasisi kuhusiana na utoaji wa vibali vya ujenzi na udhibiti wake.

Mhe. Spika, ili kuondoa kasoro hizo wizara yangu imefanya yafuatayo:-

Wizara tayari imeshatengeneza mpango wa matumizi ya ardhi ya kitaifa na miji minne ukiwemo mji wa Zanzibar *master plan* na serikali imesharidhia na kupitisha tarehe 26/4/2012 kwa ajili ya utekelezaji, hiyo *master paln* iko tayari.

Kwa suala la utoaji wa viwanja vya ujezi wizara imeshaunda chombo kipya, yaani *Urban Development control Unit* ambacho ndicho kitakuwa na jukumu la kutoa vibali vyote vya ujenzi katika eneo la *master plan.*

Aidha, napenda kuwajuilisha Waheshimiwa kuwa katika *master plan* mpya maeneo ya ujenzi yamiegawika katika sehemu tatu, eneo la ujenzi wa nyumba za ghorofa nyingi *high density***,** eneo la ujenzi wa nyumba zenye ghofa chache, yaani *medium density,* eneo la ujenzi wa nyumba za chini, yaani *low density*.

Napenda kumuhakikishia Mhe. Kazija Khamis na Wajumbe wote kuwa Sera ya serikali ni ujenzi za ghorofa na tafiti zimeshaanza kufanywa kwa kutumiza lengo hilo ambapo Mhe. Spika, tunagemea kuanzisha miradi ya nyumba kwa utaratibu wa ubia *PPPM* kwa vile sheria ya *PPP* imeshapitishwa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, huo ndio utararibu utakaofatwa katika kutekeleza hayo.

Aidha,  wizara kwa kushirikiana na *ZSSF* inaendelea na maandalizi ya mradi wa Ngambu tuitakayo, kuna mradi unaitwa "Ngambu Tuitakayo", kuhakikisha lile lengo la Mapinduzi lililoanzishwa na Marehemu Mzee Abeid Aman Karume linafanikiwa kuufanya mji wetu kuwa na nyumba za ghorofa. Sambamba na hilo Wizara ya Kazi imeshaanza kufanya kazi kwa kushirikiana na Tume ya Maafa kuhakikisha kwamba maeneo yote hatarishi yanajulikana yanatumza kwenye ramani na yalindwe ili yasitumike kwa matumizi yasiyostahiki.

Mhe. Spika, huu ndio utaratibu wetu wa ujenzi na Mwenyezi Mungu akitujaalia tunataka tuufate huu. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi waliopo na watakaokuja wafikirie kwamba tuna kazi kubwa sana ya utekelezaji wa *master plan* ya nchi hii.

Mhe. Spika, tuna dhana ya kudhani kwamba tumeshajenga, Mhe. Spika, hatujajenga Zanzibar tumejenga nyumba za kujistiri, tunajistiri tu katika hizi nyumba zetu za sasa hivi. Lakini kujenga ni haya mapendekezo yanayotolewa na Wajumbe hapa ambayo itabidi tuyasimamie. Linaweza likaja suala viwanja viko wapi. Mhe. Spika, viwanja ndio hivyo hivyo zilimo nyumba zetu ndio viwanja vyenyewe hivyo. Nakumbuka siku moja Mhe. Waziri wa Elimu alikuwa anaomba viwanja vya kujenga skuli zake za ghorofa nikamwambia bwana wewe mbona una viwanja vingi, akasema viko wapi mie sina.

Tukamwambia kwanza Muembeladu Skuli ni kiwanja kile, vunja mabanda madogo jenga nyumba ya ghorofa, Kidongochekundu Skuli ni kiwanja kile vunja mabanda yale jenga hiyo skuli ya ghorofa. Jangombe ni kiwanja kile vunja mabanda yale jenga hiyo skuli ya ghorofa. Mhe. Waziri wa Elimu hivi sasa hivi anatekeleza hivyo, kumbe alijua kwamba viwanja anavyo na nyumba hizi za maendeleo hizi

viwanja vipo kama alivyofanya Mzee Karume, tumemuuliza Mzee Karume viwanja viko wapi, yeye mzee alipotuita pale wanafunzi akatwambia tutajenga nyumba za ghorofa hapa, tunaanza tangu kwa Khamis Machungwa mpaka Michezani huko moja kwa moja, tutavunja viwanda vile tujenge nyumba za ghorofa, nafikiri ndio utaratibu wa kujenga nchi na dunia nzima ndivyo wanavyofanya, kunakuwa na makubaliano tu kwamba yule aliebomolewa nyumba alipwe nini.

Hilo ndilo suala la msingi na lifanywa na kutekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili hilo lifikiwe kwa mujibu wa masharti. Sio kwamba watasukumwa tu, haiwezekani kusukumwa watafanya na itatekelezwa.

Mhe. Makame Mshimba na Mhe. Abdalla Mohamed Ali, Mhe. Spika, Wajumbe hawa walitaka kujua kwa nini wazee wa Mahakama ya Ardhi malipo yao hayalipwi kwa wakati. Kujua kuhusu fununu za kuondoshwa kwa wazee wa Mahakama, kuhusu ufinyu wa nafasi katika Mahakama pamoja na suala la usafiri wa Mahakama ya Ardhi.

Mhe. Spika, kuchelewa kulipwa kwa wazee wa Mahakama kunatokana na utokaji mdogo wa kiwango cha fedha za matumizi ya kawaida, yaani *OC*. Hata hivyo, wizara hujitahidi kuweka kipaumbele katika kuwapati Mahakama kiwango kikubwa cha mgao ili kukidhi mahitaji kwa wazee wa Mahakama ya ardhi. Lakini tukiwa na mahitaji hayo, mahitaji hayo kuwa ni makubwa pamoja na wizara kutoa kipaumbele hicho bado kiwango hicho kimeshindwa kukidhi mahitaji ya matokeo yake ni kuwepo kwa madeni ambayo bado wazee hawa wa Mahakama wanadai. Hilo nakubali kabisa.

Wizara imezingatia sana umuhimu wa wazee hao kupatia malipo hayo ili kuwawezesha kufanyakazi kwa ufanisi na utulivu na tayari tumeandika barua ya maombi rasmi Wizara ya Fedha kwa ajili ya mahitaji haya na mara tu Wizara ikipatia fedha hizo wazee watalipwa madeni yao yote wanayodai.

Aidha, kwa upande wa Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba wizara inaendelea na jitihada za kumalizia deni hilo kwa utaratibu wetu wa ndani, yaani kwa kutumia STZ tutalilipa tu. Kuhusu wasi wasi wa kuondoshwa kwa wazee wa Mahakama hili ni suala la kisheria wazee wa Mahakama wapo kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya Mwaka 1984 na ikiwa itaonekana kuna haja ya kuwaondosha basi ni lazima sheria hiyo tuilete Barazani ifanyiwe marekebisho. Kwa hivyo, Mhe. Mohammed, hawataondoshwa, maana sheria imewaweka kwa mujibuwa sheria. Vile vile, kuhusu suala la Usafiri wa Mahakama ya Ardhi ni kweli Mahakama ya Ardhi inakabiliwa na tatizo la usafiri, hili ni kwa taasisi zetu zote za wizara tatizo kubwa linatokana na uwezo wa kifedha. Kuhusu suala la nafasi ni kweli kwa sasa

Mahakama ya Ardhi inakabiliwa na uhaba wa nafasi kwa wafanyakazi pamoja na wananchi wanaokuja kufatilia kesi zao katika jengo la Mahakama ya *Majestic*. Kwa pande wa Mahakama ya Ardhi ya Mkoa wa Mjini Magharibi wizara ina mpango kuihamisha Mahakama hiyo kwenye jengo linalotumika hivi sasa na kuihamishia Mahakama hiyo na kulipeleka kwa Mrajisi wa Vizazi na vifo Forodhani baada ya huyu mrajisi kuhama na kuhamia katika Afisi zao mpya hapo Mazizini. Nafasi ile itatutosha na tutaweka Mahakama pale. Aidha, katika jengo la Mkoa Kaskazini Gamba zinatarajiwa kuanza katika mwaka ujao na kwa Mkoa wa Kusini Unguja tayari Mahakama ishahamia Koani na inafanyakazi zake pale.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali anataka taaluma kwa wananchi kuwa ardhi ni mali ya serikali. Mhe. Spika, wizara inaendelea na Programu ya kutoa taaluma juu ya suala hili ambapo njia mbali mbali hutumika ili kuficha elimu hiyo kwa wananchi. Njia inayotumika ni pamoja na:-

(1) Semina kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Makatibu wa Halmashauri.Tunafanya hizo semina.

(2) Kwa njia za vipeperushi, semina na mikutano kwa Masheha na Shehia zote za Unguja na Pemba, tunafanya vile vile,

(3) Kupitia jarida la ardhi linalotolewa kila robo mwaka, tuna jarida pale tunaita "Ardhi" tunalitoa kila robo mwaka linaelimisha suala hilo, na

(4) Kupitia kipindi cha maagizo mbali mbali kama sasa hivi mnavyosikia kipindi cha Makombora kile kama ni Ujumbe maalum ambao unazungumzia juu ya suala la uhaulishaji wa ardhi kwamba lazima ufanyike.

Mhe. Hamza Hassan Juma, anazungumzia kuhamishwa watu wanaoanika madagaa. Mhe. Spika, watu wanaoanika madagaa wanatakiwa na serikali kuondoka katika eneo la Maruhubi. Baada ya utafutaji wa eneo mbadala wametengewa kupelekwa eneo la Kama kutokana na eneo hilo kuonekana linafaa kwa matumizi hayo.

Aidha, katika eneo hilo la Kama amejitokeza mwananchi kupitia kwa Mheshimiwa Mwakilishi na kulalamika kuwa anayo hati ya eka aliyopewa na serikali. Hata hivyo, kutokana na mazingira ya ardhi ya eneo hilo imebainika kuwa ni vigumu kutumika kwa matumizi ya kilimo, hivyo wizara ikithibitisha madai hayo itampatia sehemu nyengine itakayofaa kwa matumizi ya kilimo, hiyo kazi tutaifanya. Kama ulivyoniomba Mhe. Hamza Hassan Juma, suala hili nitajitahidi kuweza kulifatilia kwa kina na kulifanyia kazi.

Upungufu wa Mahakimu katika Mahakama ya Ardhi. Mhe. Spika, kwa sasa Mahakama ya Ardhi inayo Mahakamu sita kwa Unguja na Pemba na tayari wameshateuliwa Mahakimu wengine watatu ambao wanatarajiwa kuanza kazi mwezi wa Julai. Hivyo, ni matumaini yetu kwamba ongezeko la Mahakamu hawa litasaidia kuongeza kasi ya utoaji wa maamuzi.

Mhe. Spika, Sekta ya Maakazi, hii imehojiwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Mhe. Salim Abdala Hamad. Ni hoja kwamba wanataka kujua kuhusu nyumba ya Treni amekisikia kazi ya ujenzi amepewa *ZSSF*, je, taasisi husika zimeshirikishwa. Mhe. Spika, serikali imeamua kulifanyia matengenezo jumba ya treni kutokana na ubovu wa jengo hilo ili kunusu maisha ya wananchi wanaishi jengo hilo na wapita njia.

Mhe. Spika, *ZSSF* wameteuliwa na serikali kugharamia matengenezo ya jengo hilo kwa maana ya kuekeza kwa makubaliano na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Hivyo, wizara yangu imeshiriki kikamilifu pamoja na taasisi zake, yaani Idara ya Nyumba na Mamlaka ya Uhifadhi ya Uendelezaji Mji Mkongwe.

Aidha, mazingumzo baina ya wapangaji na wenye nyumba wamefanyika kwa njia ya maelewano juu ya utaratibu mzima wa hatua ya ukamilishaji wa matengenezo ya jengo hilo na tumewataka kwamba wanaoweza kuhama sasa hivi wahame taratibu kabla sisi hatujaingia kulifanyia matengenezo jengo lile.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, jimbo la Chambani anataka Idara ya Nyumba ina nyumba nyingi za serikali ambazo ziko katika hali mbaya sana na ametoa mfano ya nyumba za Mkoani na ameshauri ikibidi basi nyumba hizo ziuzwe. Ni kweli nyumba nyingi za serikali ni mbovu na ziko katika hali mbaya, lakini kutokana na upungufu wa bajeti ya kufanyia matengenezo nyumba, nyumba hizi inatarajiwa kuwa ni mtaji, yaani *asset* kwa shirika ambalo linatarajiwa kujiendesha kibishara. Ni mategemeo yetu kuwa litakuwa na uwezo mkubwa wa kulifanyia matengenezo nyumba hizo na kujenga mpya pindipo kutatokea mahitaji ya kuziuza baadhi ya nyumba hizo yatafanywa na Shirika la Nyumba litakuwa ndio wake.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla,  nafasi ya wanawake anasema wenzetu Tanzania Bara wameweza kujenga nyumba za mkopo nafuu ili wakopeshwe wafanyakazi. Je, swala hili tunajipanga vipi ili na wafanyakazi wa visiwani waweze kupata makazi bora. Mhe. Spika, wizara yangu inatambua umuhimu wa wananchi wa visiwa hivi kuwa na makaazi yaliyo bora na salama ambayo ni Sera ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Ni matumaini yangu kuwa Shirika la Nyumba litakapoanza utekelezaji litajihusisha kikamilifu na shughuli za ujenzi wa nyumba za maendeleo ili ziweze kukosha wananchi pamoja na wafanyakazi mwa serikali.

Mhe. Spika, napenda hapa nikumbushe kwamba maana ya Sheria ya *PPP* ni kutafuta wawekazi tukashirikiana nao, ndio maana yake. Kwa hiyo, tusiseme kwamba Shirika la Nyumba pesa litapata wapi, linatakiwa liwe na wafanyakazi mahiri na hodari watakaotafuta wawekazaji watakaoshirikiana nao katika kuboresha miji yetu hii ya Unguja na Pemba na kujenga nyumba zenye utaratibu mzuri.

Mhe. Mussa Ali Hassan, Koani lini Mhe. Waziri, atachukuwa hatua za haraka kuwahamisha wakazi wa jumba la treni ili kulinda maisha ya wananchi pamoja na wapita njia ya kuweza kulifanyia matengenezo jumba hilo. Mhe. Spika, tunapenda kumuhakikishia kwamba Mhe. Mwakilishi, kuwa tayari serikali kupitia Ardhi, Makaazi Maji na Nishati imeshachukuwa hatua za kukutana na wananchi wanaolitumia jumba la treni na kuwataka kuhama. Ni matarajio yetu kwamba muda wowote kuanzia hivi sasa harakati za kulifanyia matengenezo jengo hilo zitaanza baada ya kukamilika kwa taratibu la kukabidhi jengo kwa *ZSSF* ambao ndio watakaokuwa wanagharimu matenegenzo ya jengo kwa usimamizi wa Wizara ya Ardhi.

Mhe. Mussa Ali, vile vile, anataka kujua ni takwimu juu ya takwimu za nyumba mbovu za serikali katika eneo la Mji Mkongwe. Suala hili Mhe. Naibu Waziri ameshalijibu kwamba kwa mujibu wa ukaguzi wa nyumba mbovu umeonesha kuwa katika eneo la Mji Mkongwe kuna jumla ya nyumba 26 ndio mbovu sana ambazo hizo zimeshatajwa.

Mhe. Nassor Salum Ali wa Rahaleo anauliza Shirika la Nyumba ni majengemeo makubwa kwa wananchi katika hatua ya matatizo ya makaazi. Ametushauri tuzifanyie mpango mzuri wa kuziwekea namba. Mhe. Naibu Waziri ameshalijibu hili kwamba zitawekwa namba zijulikane.

Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Mtambwe anasema kwamba katika ukaguzi imebainika kwamba kuna nyumba za serikali katika eneo la Mji Mkongwe ni mbovu na zinahatarisha usalama wa wakazi wake. Wakati tunajua umuhimu wa Mji mkongwe kwa nini nyumba hizi zimefikia hali hiyo bila ya kutengeneza.

Mhe. Spika, jitihada za kufanyia matengenezo nyumba za serikali Mji Mkongwe zinachukuliwa kwa kushirikiana na wakaazi wa nyumba hizi ila ni vyema ieleweke kwamba nyumba za mji Mkongwe nyingi ni mbovu kutokana na uchakavu mkubwa mkubwa unaozikabili nyumba hizi na pia kwa muda mrefu hazikufanyiwa matengenezo yanayofaa kutokana na ufinyu wa bajeti ya matengenezo na halafu pia tujue kwamba ni nyumba za zamani sana, nyengine zimejengwa hata sisi hatujazaliwa tulipo hapa, udongo umeshachoka, chokaa imeshamaliza umadhubuti wake, hili nalo ni tatizo kusema ukweli.

Hivi sasa kwa nyumba zinazomilikiwa na serikali wizara yangu imeandaa utaratibu wa kuziuza nyumba mbili za Mji Mkongwe na kukodisha nyengine nane kwa lengo la kupata fedha zitakazotumika kwa matengenezo ya nyumba za Mji Mkongwe tu, matumaini yetu kuwa mpango huu utatusaidia kuzidisha uimara nyumba hizi.

Mhe. Hamza Hassan Juma, anauliza Shirika la Nyumba ni moja ya kumuenzi Marehemu Mhe. Abeid Aman Karume, anamuomba Mhe. Waziri, atafute mtu mwenye uwezo wa kuliendesha Shirka la Nyumba. Ushauri wake ni mzuri na kama tulivyosema kwamba atakaeongoza Shirika la Nyumba lazima awe mtu mahiri na shirika lenyewe liwe mahiri litafute wawekezaji na nadhani wakati huo ikifika Mhe. Hamza Hassan, atamleta yule muwekezaji wake tuingie kwenye *PPP* ya ujenzi wa nyumba hizi kama alivyosema. Shirika la Nyumba litakaloanzisha litarithi na maeneo yote ya ardhi yaliokuwa yakitumia na Idara ya Nyumba na Shirika la Nyumba litakuwa na fursa ya kutafuta ardhi kwa ajili ya miradi yake kwa mujibu *master plan* mpango wa matumizi ya ardhi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Muyuni, Sheria ya Mamlaka ya Uhifadhi Mji na Mazingira na yake. Je, nje ya Bandari ya abiria mazingira yake ni mazuri ameuliza swala hilo. Mhe. Spika, uimarishaji wa eneo hilo umeanza kushughulikiwa kupitia kamati maalum iliyo chini ya Mwenyekiti wa Mkuu wa Wilaya ya Mji inayoshirikisha Taasisi kadhaa ukiwemo Baraza la Manispaa, Shirika la Bandari, Mji Mkongwe, Idara ya Barabara na Idara ya Mazingira. Uimarishaji huo tayari umeanza kwa utengenezaji wa njia za kupita watu kwa kuweka nguzo mbembezoni zisiigeshe magari na mambo mengine yatafanywa baadae wakati kamati ikatopata nafasi.

Mhe. Spika, ujenzi ni kitu kinachokwenda kwa awamu hatuwezi tukasema mara moja tunaweza tukabadilisha pale. Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, alivyoomba nasema ni suala mahiri na tutalitekeleza pawe panapendeza kuliko palivyo hivi sasa hivi. Mhe. Jaku Hashim Ayuob, anasema ushauri wa utolawaji wa vibali nusu nusu unasumbua wananchi kama kuna uwezekano utolewe kwa pamoja.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim, kwamba vibali vya matengenezo madogo madogo vinatolewa kwa pamoja. Lakini kwa upande wa ujenzi mkubwa kama ujenzi mpya wa jengo vibali hutolewa kwa awamu, hatua kwa hatua na ikimaliza kila awamu husika kibali cha hatua nyengine kinatolewa ikiwa haukwenda kinyume na ujenzi huo, yaani anaambiwa jenga sehemi hii inafatiliwa na ametekeleza kama kilivyo kibali, anapewa kibali chengine anakwenda kwenye hatua nyengine imetekelezwa kama ilivyo kibali, anapewa ruhusa nyengine na

anaendelea na jengo lake kwa sababu jengo ni kubwa huwezi ukasema utajenga halafu yale makubaliano yote yaliokuwemo ndani ya mkataba ikawa hayakufatwa. Mhe. Spika, ushauri mwengine anasema Mhe. Jaku Hashim, kama ujenzi wa mawe ndani ya Mji Mkongwe unaleta usumbufu na ni gharama kwa wananchi. Mhe. Spika, Mji Mkongwe wa Zanzibar ni mji uliojengwa kwa mawe kwa tafsiri ya Kiengereza ni *Stone Town*. Ujenzi wa mawe ni wa asili. Hivyo, kwa mujibu wa taratibu za uhifadhi vifaa vinavyotumika kwa ujenzi ikiwa vinapatikana katika eneo lile hutumika kwa mawe kama vile mawe, boriti na kadhalika.

Mhe. Spika, kutokana na kasi ya ujenzi wa sasa unavyoendelea na ukiendelea kujenga bila ya kutumia mawe uasili huo utapotea. Lakini kwa sababu ya hoja ya Mhe. Jaku Hashim, ambayo hakuanza kuitoa leo hapa, amekuwa akiitoa, tumefikia makubaliano kwamba hivi karibuni kwenye mwaka 2012 kwamba hivi sasa hivi kuta za nje zijengwe kwa mawe na ndani yaendelee kujengwa kwa matofali, hiyo ndiyo makubaliano yetu mapya kwa ajili ya kupunguza hiyo gharama ya mawe na udongo.

Kuhusu kutotoa majibu kwa barua ya Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, inayohusiana na *Hansard* Nam. 49 ya tarehe 25/3/2015. Mhe. Spika, barua aliyoitaja Mhe. Jaku Hashim, iliyoandikwa na Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, yenye kumbukumbu namba hii hapa OMPR/WNAMMN.70/C1 VOl 24 ya tarehe 16/4 kupelekwa kwa Katibu Mkuu wa Ardhi na Makaazi ilihitaji utekelezaji na sio majibu, yaani vile ilivyojibiwa hapa wizara ifatilie na itekeleze kama ilivyobiwa hapa. Kwa hivyo, barua tumeipokea na tunaifanyia kazi.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, ukarabati wa jengo la Beit-el Ajaib umechukuwa muda mrefu sasa bila kuanza kwa ufadhili wa Oman kama haiwezekani basi serikali ingeamua kufanya.

Mhe. Spika, kufuatia ziara ya Mhe. Waziri wa Mambo ya Nje wa Oman alioifanya Zanzibar mwaka 2013 baada ya kuanguka kwa jengo, pamoja na mambo mengine alitembelea eneo hilo na kuagizo wataalamu wake kuja Zanzibar kukutana na wataalamu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe ili kufanya kazi za awali za kitaalamu za utarishaji wa ramani na gharama za matengenezo kusiwasilisha wizara husika nchi Oman.

Mtaalamu kutoka Oman ambaye ni Raia wa Italy walikutana na wataalamu wa Mji Mkongwe 2013 na kuikamilisha kazi hiyo na kuiwasilisha mwaka 2014. Baada ya hapo mamlaka haikupokea maoni yoyote kutoka Oman hadi mwanzo wa mwaka 2015. Hili ilitokana na kwamba yule mtaalamu Mheshimiwa, alipata maradhi, kwa hivyo, ikabidi lazima apelekwe kwao akauguzwe na akauguzwa, hapa halipokuja tena, kwa hivyo, utaona kwamba alifika Zanzibar na kukutana na Mamlaka ya Mji

Mkongwe mwanzo wa mwaka 2015 mtaalamu huyo ndio alifika tena hapa Zanzibar na kukutana na maeneo ya Mji Mkongwe na mapendekezo mapya na ambayo yamekubaliana kufanya makisio mapya ya gharama kwa ujenzi utakaokuwa wa awamu. Halafu yawasilishwe tena nchini Oman yale yaliokwishakupitwa na wakati sasa hivi wanafanya mapendekezo mapya.

Wazo la kuitaka serikali kujipanga kufanya matengenezo hayo kwa gharama zake wenyewe muda ukizidi bila ya mafanikio limepokelewa. Hoja jengo la Bwana Abdulhamid ni bovu sana na ni hatari kwa maisha ya wananchi, serikali ifanye maamuzi ya kulishughulikia jengo hilo. Mhe. Spika, wizara inakubaliana na hoja ya Mheshimiwa, juu ya hali ya jengo hilo. Hata hivyo, wizara na mamlaka tayari imeshafanya vikao kadhaa na muhisika na kutoa barua mbali mbali kwa bwana Abdulhamid ili kutakiwa kulifanyia matengenezo jengo hilo.

Aidha, ramani za matengenezo yaliyokusudiwa na vibali vya ujenzi vimetolewa tokea mwaka 2006 na hadi sasa Kampuni iliyokodi nyumba hiyo imeshindwa kuchukuwa hatua yoyote ya kulifanyia matengenezo na hata kuhifadhi lisianguke. Hivi sasa mamlaka inawasiliana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuangalia vipengele vya sheria vitakavyowezesha mamlaka kuchukua hatua za haraka. Itabidi sasa hivi twende huko, hatuna njia nyengine kwa sababu muda ni mrefu sana.

Kuna tetesi ambazo hatuwezi kuzithibitisha sisi zinazosema pengine muwezaji yule anategemea lile jengo lianguke na aanze kujenga upya kutoka chini. Sisi tusengependelea jengo la Mji Mkongwe lifanye hivyo. Kwa hivyo, Mwanasheria atatushauri tuchukuwe hatua gani za kisheria kuhusu suala hilo.

Mhe. Nassor Salum Ali wa Rahaleo, jengo la *People's Palace* lilivyoweka miega *support* kuzuia serikali kupitia wizara imejipanga vipi. Mhe. Spika, jibu ni kwamba wizara kupitia mamlaka imelifanyia ukaguzi wa kina jengo hili na kuthamini hali halisi ya ubovu na hivi  sasa linafanyiwa tathmini ya gharama za matengenezo yake. Ili serikali iweze kuinusuru kwa maeneo yaliyoathirika sana kwa hatua za awali na kuendelea baadae na kazi za umalizaji wa awamu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Sekta ya Maji Mhe. Jaku Hashim Ayoub, suala la ulipaji wa huduma za maji kwa mifereji ya nje.

Mhe. Spika, tunakubali kuwa kutakuwa na mifereji ya nje kwa wananchi ambao hawana mifereji ya ndani ambayo itakuwepo katika masafa maalum na huduma hiyo itagharamiwa na *ZAWA*. Hii tunakubali kabisa, na hapa ninataka niseme kwamba ni kweli katika mitaa yetu kuna watu wa karimu sana, wanapenda

kuwatolea mifereji watu wao nje kukinga maji, hatukatai mtu kutoa mpira akawapa watu kuteka maji nje. Lakini atakapokuwa anatoa mfereji anaweka nje ya nyumba kwa ajili ya watu kuja kuteka maji, ikiwa mtu huyo amewekewa mita pale mwanzo ya maji yanapoanza kuingia ndani, hilo hatuna tatizo nalo na tunajua maji yake atakuwa analipa kwa kutumia ile mita iliopo pale nje. Lakini kama hana mita, ni vizuri watu wa maeneo yale wakachukue maji katika ile sehemu itakayowekwa maalum na *ZAWA* kwa ajili kukinga maji hayo.

Kwa sababu mifereji ya nje ni mingi sana itasababisha upotevu wa maji kwa wingi sana na mifereji yenyewe mara inakuwa mibovu, inavuja, maji yanapotea. Kwa hivyo, tunakubaliana kwamba lazima uwepo mfereji wa wananchi nje mahala, lakini siyo mingi kwamba kila nyumba ina mfereji nje hiyo hututaki, isipokuwa kama tutakuwa tumemuwekea mita pale mwanzo wa bomba linaloingia ndani mwake, huyo muache aweke mfereji nje na muache atoe mipira na mambo mengine, sisi hatuna matatizo na hilo. Maana maji ni mali lazima tuyalinde.

Mhe. Spika, Mamlaka ya *ZAWA* kwa kuona umuhimu wa kupatia wananchi wa Zanzibar huduma ya maji safi na salama, tunatambua kuwa wananchi wengine inawapa ugumu kuweza kumudu gharama za uungaji maji katika nyumba zao na kupelekea kutegemea mifereji ya nje. Kwa kulitambua hilo, Wizara yangu kupitia *ZAWA* imeweka utaratibu mzuri wa kuunganishwa na mtandao wa maji kwa njia ya mkopo, mwananchi anatakiwa atoe kiwango chochote cha fedha, kilichobaki kitalipiwa kidogo kidogo wakati wa kulipa huduma hiyo mwisho wa mwezi kwa kukata asilimia 50.

Mhe. Kazija Khamis Kona, hili Mhe. Naibu Waziri, ameshalijibu. Mhe. Nassor Salim Ali na Mhe. Jaku Hashim Ayoub hoja ya kurudisha huduma ya maji kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhani ikiwemo Kijiji cha Michamvi, kuimarisha miundombinu ya maji katika nyumba No. 3 na 4 Michenzani.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji ina utaratibu maalum katika kuimarisha huduma ya maji hasa katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani na inapobainika eneo lina upungufu wa huduma ya maji, wananchi hupatiwa huduma hii kwa kutumia magari ya maji. Utaratibu huu Mhe. Spika, tutaendelea nao tena katika mwaka huu mwezi wa Ramadhani keshokutwa utakapoaanza, tutawapelekea maji. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Michamvi kwa bahati nzuri wao sasa hivi wameanza kupata ile *distillation water* ya maji yale yanayochujwa kutoka chumvi kuwa ni maji kuwa maji ya kunywa na ule mradi ushaanza kutoa maji kidogo kidogo. Sasa iliyobakia ni kuwajengea tangi ili maji yale yanaingia katika tangi maalum baada ya kufanyiwa *distillation* ili wananchi wapate maji ya kunywa kutoka katika tangi lile. Utaratibu huu tutaufanya kwa ajili ya Michamvi. Lakini hata hivyo kwa

Ramadhani inayokuja keshokutwa gari la maji tutalipeleka Michamvi watu wapate maji kama walivyoomba Waheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, halafu moja katika suala hili hili ni kwamba Mamlaka inaendelee na zoezi la utambuzi wa maeneo yote ya mijini yenye ukosefu wa maji unaotokana na uchakavu wa miundombinu na kuyatatua kwa kadri ya uwezo kifedha unaporuhusu. Miongoni mwa maeneo hayo ni maeneo ya Michenzani na Rahaleo ambayo yamo katika mradi wa uimarishaji wa huduma ya maji mjini *(ADF 12).*

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kaniuliza uendelezaji wa mradi wa Kipandoni baada ya kuchimbwa kisima na ujenzi wa matangi. Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kitope kuwa mradi huu ni miongoni mwa kazi zinazofanywa na mfadhili wa Ras el Khaimah ambapo kwa awamu ya kwanza ilikuwa ni uchimbaji wa visima na ujenzi wa matangi na kulaza mabomba makubwa. Kuchimba visima na kujenga matangi ambapo kazi hiyo imekamilika. Hivyo, kazi inayoendelea sasa kwa Serikali kupitia Mamlaka ya Maji ni kuunganisha kutoka katika mabomba makuu, kwenda katika mabomba ya watumiaji. Kazi hiyo imeanza na inaendelea, tayari wananchi wa Machui, nimeliruka suala hili Mhe. Spika, unajua sitaki kukupotezea wakati wako mrefu kabisa. Hili ni suala ambalo ameliuza Mhe. Mussa Ali Hassan, juu ya suala la Machui na kwengineko.

Kwa ufupi ninasema ni kwamba miradi hii mipya ya Matemwe, Koani, kule Mkorogo, matangi yale tayari yana maji hivi sasa na maji yake yanaingia katika mabomba makubwa. Sasa kazi inayotaka kufanywa na *ZAWA* ni kuyachukua mabomba yale kutokana na maji yale kwenye mabomba makubwa kuyatia katika mabomba madogo, ndiyo kazi wanayotaka kuifanya ambayo sasa wanaendelea nayo kazi hiyo. Kazi hii itakapokamilika maeneo mengi yanayohusu maji yale ya miradi hii mipya ya matangi makubwa wananchi watakuwa wanapata maji. Hicho kwa ufupi ndicho nilichotaka kukisema ambapo Mhe. Mussa, umeuliza, tunafanya kazi hiyo hivi sasa.

Kwa hivyo, wacha wananchi wawe na ustahamilivu kidogo *ZAWA* inaendelea kuunga maji kutoka kwenye mabomba makubwa kwenda katika yale mabomba ambayo ni madogo madogo ambayo yapo pale. Na pale ambapo itakuwa mabomba hayapo jitihada zitafanyika ili kutafuta mabomba kupeleka mabomba kupeleka katika maeneo yale ambayo mabomba hayapo, tunataka asilimia ya upatikanaji wa maji iongezeke.

Mhe. Hassan Hamad Omar, kutokuunganishwa kwa huduma ya maji katika Kijiji cha Gombeume. Naomba kumjibu Mhe. Spika, kama ilivyo katika maeneo mengine yaliyopitiwa na miradi mipya. Kijiji cha Gombeume ni miongoni mwa

kijiji vilivyobahatika kuwemo katika mradi wa maji vijijini Mchangamdogo, Kambini ambacho kwa sasa yanasubiri kuunganishwa kwa mtandao kwenda kwa kuwatumiaji na kwa sasa kazi hii imeshaanza.

Mhe. Kazija Khamis Kona, hoja ya ulazaji wa mabomba kuwa ni endelevu mfano wa Kijiji cha Kijini. Mhe. Naibu Waziri, ameshajibu, Kijini tayari mabomba yameshapelekwa na hivi sasa watu wa Kijini wanaanza kupata maji bila ya tatizo lolote.

Kutokuwepo kwa baadhi ya wananchi waliokuwa hawajalipwa fidia kupitia mradi mkubwa wa maji vijijini, kuna utaratibu gani uliotumika kulipia fidia baadhi ya wananchi hao? Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa, kwamba utaratibu wa ulipaji wa fidia unakwenda sambamba na maeneo yaliyofanyiwa tathmini awamu kwa awamu kwa kuanzia na maeneo ya ujenzi wa matangi, maeneo ya uchimbaji wa visima na uchimbaji wa misingi ya kulaza mabomba, hayo ambapo madai ya fidia yaliyobakia sasa ni yale yaliyofanyiwa tathmini katika maeneo yaliyoathirika kwa kazi ya uchimbaji wa misingi ya ulazaji wa mabomba, kuchelewa kukamilisha malipo kwa waliobakia ni kutokana na hali ya upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, Serikali ipo katika utaratibu wa kukamilisha malipo hayo.

Mhe. Spika, mradi wa Kwaeshangwe utakamilika lini. Mhe. Spika, mradi wa Kwaeshangwe tayari umeshakamilika na hatua ya kulaza mambo makubwa na baadhi ya wananchi wanafaidika na huduma ya maji safi na salama. Kazi inayoendelea ni kuunganisha mtandao wa mabomba madogo ili wananchi waliobakia nao waweze kufaidika na maji. Mhe. Abdi Mosi Kombo, hilo ni suala lako.(*Makofi*)

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, kwa nini mita zinaendelea kufungwa wakati Mhe. Rais ameagiza kuondosha mita *TUKUZA*. Mhe. Spika, ninapenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi, kwamba mita zilizokusudiwa katika kipengele hichi cha nambari 38 ni mita za maji za wateja wanaofungiwa katika majumba yao, lakini katika vianzio vya maji mita zote zimeondoshwa hakuna iliyobakishwa hivi sasa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Jimbo la Mtambwe, Mhe. Naibu Waziri, ameshajibu. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, ni sababu zipi zilizopelekea kuharibika kwa kisima cha Chambani. Mhe. Spika, ninapenda kumjuulisha Mheshimiwa, kuwa kisima cha Chambani ni miongoni mwa visima vinavyochimbwa kupitia mradi wa *Ras el Khaimah*. Aidha, kuharibika kwa kisima katika kazi ya uchimbaji ni masuala ya kawaida ambayo yanachangiwa na sababu mbali mbali za kiufundi na kimaumbile ya ardhi. Hata hivyo, tayari mkandarasi ameweza kuchimba kisima chengine katika eneo hilo na tayari kimekamilika na

matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa kina maji ya kutosha kama kile cha awali, tumefanikiwa katika hili.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali, tatizo la kutokukamilika kwa mradi wa Wambaa kukamilisha kilomita saba. Ninakubaliana na Mheshimiwa, kwamba awali mradi wa *AfDB* ulipanga kulaza mabomba urefu wa kilomita kumi na saba kwa eneo hilo. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa fedha za mradi zimeweza kujengwa kilomita kumi. Eneo lililobakia ni kilomita saba katika mradi huo. Ni miongoni mwa eneo yaliyoingizwa katika programu ya maabara ya kukuza maeneo ya utalii na tayari limeshaainishwa na kukubalika. Ni matarajio yetu ni kuwa mradi huu utakamilika mwaka ujao wa fedha wa 2015/2016.

Mhe. Abdi Mosi Kombo, wewe umeuliza suala la baadhi ya Matemwe, Kijini, Kigomani Juu, Mbuyutende na maeneo jirani, je, maji yatafika lini katika maeneo hayo. Umeshajibiwa na Mhe. Naibu Waziri, kwamba Kijini tayari na humu mwengine tutaendelea kukufanyia kazi. Ni kazi yetu endelevu, siyo kazi ambayo tutaimaliza mara moja.

Mhe. Hamza Hassan Juma, kufanywa ukaguzi wa bomba linatokea Welezo kupitia Kwamtipura hadi Michenzani. Mhe. Spika, naomba kumshukuru Mhe. Mwakilishi, kwa ushauri wake na tumeupokea. Aidha, tayari Mamlaka imeshaufanyia ukaguzi bomba hilo na limeshaingizwa katika programu ya ukarabati kupitia mradi wa maji mijini chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB 12).* Bomba hili ni aina ya *asbestor* na litabadilishwa lote, litang'olewa litatiwa bomba madhubuti la kukaa pale. (*Makofi*)

Aidha, kwa kupitia Baraza hili tunaomba wananchi wasijenge ndani ya mita sita kutoka katika bomba kubwa la maji la zamani na mapya kwa maeneo yote ya Unguja na Pemba, ili kuhifadhi miundombinu ya maji na kuepuka uchafuzi wa maji.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ameuliza kuwa Idara ya Nishati ishirikishwe katika upangaji wa bei ya mafuta kwa nia ya kuongeza udhibiti wa bei ya biashara. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, ninapenda kumuhakikishia Mhe. Mshimba, kwamba Wizara kupitia yake ya *ZURA* ambayo imeshateuliwa Mkurugenzi inaanza kazi. Inatarajia kufanya kazi hiyo kwa mashirikiano na Wizara ya Fedha kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha taasisi hiyo kwa nia ya kukamilisha malengo ya Serikali.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Jaku Hashim Ayoun na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, kuwapa nafasi wawekezaji wazalendo katika kuwekeza *depot* nchini pamoja na Mhe. Mahmoud yumo katika suala hili. Mhe. Spika, na

Waheshimiwa Wajumbe, ushauri huo umepokelewa na unafanyiwa kazi na Wizara yangu.

Aidha, ninapenda kutoa taarifa kuwa ni kweli kabisa Wizara yangu ilipokea ombi la mwekezaji aliyetajwa. Hata hivyo, kwa vile uwekezaji wa aina hiyo unakuwa na masharti mbali mbali yanayohusiana na muda wa uwekezaji, mapato, utaalamu, ujenzi na viwango kuzingatiwa, masuala ya mazingira na kadhalika. Kwa hivyo, inahitaji Serikali kujipanga katika kuangalia hayo ikiwa ni pamoja na kuiweka vizuri kisheria na uwezo wa kitaalamu wa kusimamia miradi ya aina hiyo.

Isipokuwa ushauri huu umepokelewa na kuyazingatia haya yote kwa mashirikiano ya pamoja na sehemu nyengine kama vile *Zanzibar Bureau Standard*. Masuala haya ingawa yanahitaji mazingatio ya kina, lakini ni kweli kabisa wazalendo wanahitaji nafasi katika uwekezaji huo na mara baada ya Serikali kujipanga vizuri katika hilo, wazalengo watapewa vipa umbele kwa kadri inavyowezekana, ikiwemo mwekezaji aliyetajwa baada ya kutimiza masharti ya viwango vitakavyowekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tuwaombeni wastahamili kidogo ili tukamilishe mambo yetu, tusifanye mambo kwa haraka haraka, halafu tukaja tukajuta tukapata mafuta maji hapa, si vizuri kusema kweli.

Mhe. Salim Abdalla Hamad, mchango mdogo wa Serikali katika kuchangia utekelezaji wa mradi wa nishati mbadala wa asilimia 16. Mhe. Spika, ninakubaliana na Mhe. Salim Abdalla Hamad, kuwa michango ya Serikali na wahisani ilikuwa midogo hadi kufikia mwezi Machi. Hata hivyo, ninaomba nitamke kuwa katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali ilitupa mchango mkubwa lakini kwa bahati mbaya kazi zilizokusudiwa kutekelezwa katika kipindi hicho zilichelewa kidogo kutokana na kuchelewa kulipa vifaa vya kazi hiyo kutoka nje. Asilimia kubwa ilikusudiwa kutumika baada ya kuwasili kwa vifaa vya ujenzi wa minara ya kupimia upepo na jua baada ya mwezi wa Machi ambavyo kwa sasa vimeshafika na kazi zimeshaanza kutekelezwa.

Aidha, asilimia ndogo ya mchango wa asilimia 16 ni kwa sababu ndiyo gharama halisi za ununuzi wa vifaa vya kazi hadi kufikia mwezi wa Machi hii ni kusema kuwa fedha zilizotolewa katika kipindi hichi zimetosheleza. Hapa ninataka kulisema Mhe. Spika, tunalo tatizo...

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, inaonekana umebakia sehemu ndogo tu.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Eeh! imebakia sehemu ndogo sana.

**Mhe.Spika:** Sawa basi malizia kwa dakika kama tano.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Hapa Mhe.Spika, ninataka kusema jambo moja.

Mhe.Spika, tunapojenga minara ya utafiti, Waheshimiwa Wawakilishi, tusaidieni tunapata tatizo. Hivi sasa tunataka kujenga mnara wa utafiti Micheweni wananchi hawataki kuusikia na ule mnara unatazama unataka kupima upepo pale na unataka kupima kiwango cha *radiation* ya jua, wananchi hawautaki ule mnara. Hebu tusaidieni tuwafahamishe wananchi wakubali, kwa sababu ndiyo utafiti wenyewe unaoendelea hivi sasa, tujenge kule mnara wa kuweza kufanya utafiti. Ule mnara si wa kuwapeleka Wazungu kama wanavyosema wenyewe, ni mnara wa kupima kiwango cha *radiation* pamoja kiwango cha upepo pale kwa kitaalamu. Hili naona nilisema Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, umenihimiza na ninaona nina karatasi tatu. Sasa ninaona kuna watu sitowajibu na nisingependelea kuwa nisiwajibu, lakini sasa sina la kufanya itabidi nifanye maarifa wengine tuwaelewane mimi na wao. Lakini kuna jambo moja ninataka kulizungumza.

Kuna suala la Kisiwa cha *Latham Island,* yaani Kisiwa cha Fungu Mbaraka. Mhe. Spika, hapa ninachotaka kusema ni kwamba Kisiwa cha Fungu Mbaraka kimo eneo la Zanzibar. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Kisiwa cha Fungu Mbaraka ni mali ya Zanzibar. Katika kukata zile *blocks* tu ikatokezea kwamba Zanzibar tulizungumzia zaidi *block number nine* mpaka *number twelve; nine, ten, eleven and twelve,* hatukuzungumzia *block eight*. Wakati *block eight* ndiyo iliyokichukua kile Kisiwa cha Fungu Mbaraka. Tunajua kwamba *jurisdiction* ya *TPC* ilikuwa ni wao ni kutoa leseni kwa meneo ya kule Tanzania Bara kwa sasa hivi na wametuachia sisi kuongejea itakapokuwa tayari kwa ajili ya maeneo yetu.

Sasa *block eight* walikuwa wameshalitoa idhini. Lakini katika mazungumzo tunayoendelea nayo sasa hivi, tuna hakika tutaelewana na nina hakika Kisiwa cha Fungu Mbaraka kitarudi Zanzibar na eneo lile litarudi Zanzibar, hakuna wasi wasi. (*Makofi*)

Kama tulielewana kwenye masuala ya bahari kuu, kwa nini tusielewane katika jambo dogo kama hili la eneo tu na sisi tukafaidika na maeneo yale. Hili Mhe. Spika, lipo na tunajua kabisa ninathibitishia kwamba kile Kisiwa ni mali ya Zanzibar na tutaelewana na mazungumzo na Tanzania tunao utaratibu wa kuelewana katika mambo mbali mbali. Watanzania siyo watu tunaoingia katika migogoro kwenye masuala haya, tuna vikao tunayazungumza na tunatafuta

ufumbuzi. Kwa hivyo, ni kisiwa cha Zanzibar na tutafikia ufumbuzi, kama tulielewana kwenye bahari kuu, tutaelewana kwa kisiwa cha Fungu Mbaraka.

Mhe. Spika, naomba kwamba kuna suala la Fumba limezungumzwa hapa ambalo Mhe. Mahmoud, amelizungumza nalo, ninataka nalo nilizungumze. Fumba ni katika eneo ambalo sasa hivi limebahatika sana, kwa sababu Fumba watapata nyumba za kisasa kabisa katika eneo lile. Mazungumzo yanaendelea na *ZIPA* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Sasa hivi siyo ndoto, sasa ni hakika kwamba kule kutapatikana nyumba za kisasa kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, na wananchi wa Fumba wasiwe na wasi wasi kabisa na wala kwa sasa hivi zile nyumba zao ziliko kule hatuzikugusi kwa sasa, wataendelea kukaa kule sisi tunajenga huku. Maana tutafanya kama alivyofanya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Mzee Karume alianza kujenga pale Kikwajuni, halafu akenda Kilimani ndiyo akawaondoa Michenzani akawapeleka Kilimani.

Kwa hivyo, na kule sisi kule nyumba za Fumba hatutozigusa na huku kwenye nyumba za Bweleo hatutozigusa, tutajenga kati kati katika sehemu ambayo iko wazi na wale sasa tutawa-*compensate* nyumba zao ndani ya *apartment* tutakazozijenga Fumba na wataishi katika maisha ya kileo, wasiwe na wasi wasi kabisa. Nchi hii inahitaji kujengwa na inahitaji kufanywa maisha ya watu kuwa mazuri kabisa. Kama vile anavyokwenda Mhe. Hamza Hassan Juma, China akaona *apartment*, basi na huku tutaanza kidogo kidogo. Tunazungumza na fadhili, na tayari sasa hivi ukenda sehemu za hapa katikati baina ya Fumba na Kombeni, Nyamanzi tayari kuna ujenzi umeshaanza pale wa nyumba za chini lakini za kisasa. Hivyo ndivyo tunavyotaka kwenda. Tumepata mfadhili mwengine pale anafanya kazi hiyo. Tunafanya kazi nzuri, Mhe. Spika. (*Makofi*)

Naomba wale ambao hawakusikia majina yao, maana majina mengine yamekuja haraka haraka hapa siwezi kuyasema na Mhe. Spika, umeshanihimiza wanisamehe, sina nia mbaya, ninayo yote hapa majina yao, lakini sina nia ya kuwaacha na wasione kwamba labda Mheshimiwa, ametupuuza pale majibu yetu, ninayo yote hapa na majibu yao ninayo sikuwahi kuyasoma kutokana na wakati. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja baada ya maelezo hayo.(*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri, ninajua mengine mengi kama ulivyotangulia kusema unayachukua na kuyafanyia kazi. Maana hawa hawakutaka kujibiwa Waheshimiwa Wajumbe, ila wanataka vitendo vifanyike. Waheshimiwa Wajumbe basi sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka 2015/2016 wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliomo humu ndani wote wamekubali. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara za SMZ:** Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali Hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishat, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

## KAMATI YA MATUMIZI

## UTARATIBU

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunakabiliwa na mambo muhimu ya kuyajadili kwa faida ya wananchi, na suala hili nilikuuliza hata katika semina, tunaingia katika programu mpya hii, nafikiri halikupatikana jawabu katika semina. Labda hapa litapatikana jawabu. Mhe. Mwenyekiti, kama mtu ana hoja tatu katika kifungu kimoja, je, kanuni itawekwa kando?

**Mhe. Mwenyekiti:** Sijakuelewa Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, kama mimi nina hoja tatu au nne katika usimamizi wa upangaji wa ardhi au Mji Mkongwe ninaweza nikazieleza kwa mfululizo? Maana yake asija akafika pale mtu akaanza kutoa hoja ya kwanza, hoja ya pili, hoja ya tatu ukajakumzuwia mtu. Kwa hivyo, nataka utufahamishe mapema kwamba mtu asimamie hoja zake zile tatu kwanza au moja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Hebu tuone hizo hoja zako zikoje. Twende tuone hizo hoja zikoje tutatoa maamuzi pale itakapokuja hoja. Hatuwezi tukatoa maamuzi wakati hakuna hoja hadi sasa.

## FUNGU N01 - WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI

Kifungu 01 Ofisi Kuu Pemba Shs. 262,507,000
Kifungu 05 Mamlaka ya Hifadh na Uendelezaji wa Mji Mkongwe

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim, hii ni sehemu ya mapato, una wasi wasi kuhusu mapato. Tuendelee.

| | |
|---|---|
| Kifungu 05 Mamlaka ya Hifadh na Uendelezaji wa Mji Mkongwe | Shs.26,114,000 |
| Kifungu 07 Idara ya Ardhi na Usajili | Shs. 3,758,222,000 |
| Kifungu 08 Idara ya Nyumba na Makaazi | Shs.624,480,000 |
| Kifungu 11 Msajili wa Ardhi | Shs.13,625,000 |
| Kifungu 13 Idara ya Upimaji na Ramani | Shs.101,733,000 |
| Kifungu 16 Idara ya Ujenzi | Shs.12,944,000 |
| **Jumla Kuu** | **Shs.4,799,625,000** |

**FUNGU N01 - WIZARA YA ARDH, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI**

**KIFUNGU P01 - PROGRAMU YA MIPANGO NA UTAWALA WA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI**

Programu Ndogo S01 Mipango na Sera za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, pale Mhe. Jaku Hashim, alipotaka kuparaza buti ulimwambia tupo katika mapato. Sasa tumeshaondoka katika mapato, maana yake unajua haya mabuku mapya. Sasa tujuwe kama tumeshaondoka kwenye mapato, tunakwenda kwenye uendeshaji. Tulikuwa tunataka taarifa tu kabla hatujapiga buti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Hoja ni nini sijafahamu. Mapato tumemaliza, tuko kwenye ukurasa wa 618 kwa ajili ya matumizi, pale kuna muhtasari na upande wa pili 619 ndio kuna vifungu vyenyewe, Programu na Programu Ndogo. Sasa kama zile hoja ziko mtaa huu basi tumsikie mwenye hoja katika hapo. Ukurasa wa 619 ndio kwenye Programu Kuu na Programu Ndogo.

| | |
|---|---|
| Programu Ndogo S01 Mipango na Sera za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati | Shs.161,884,000 |
| Programu Ndogo S02 Utawala na Maendeleo ya Rasilimali Watu | Shs.804,252,000 |
| Programu Ndogo S03 Uratibu wa Shughuli za Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Pemba | Shs.1,018,229,000 |
| **Jumla Kuu** | **Shs.1,984,365,000** |

Kifungu P02

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Nilimsikiliza sana Mhe. Waziri. Kwanza nitowe shukrani zangu za dhati kabisa kumshukuru Mhe. Waziri kwa umakini wake wa hali ya juu, jinsi alivyofafanua hoja baada ya hoja kwa

ufanisi, kwa ufundi na kwa ustadi wa hali ya juu. Hii inatokana na watendaji wake wako makini sana, wakiongozwa na Katibu mahir Ali Khalil Mizar.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu ufutaji wa ardhi. Sheria aliyosema waziri, Sheria Nam. 12 ya mwaka 1962, hivyo tafsiri yake kisheria inaweza kutofautiana mfano kufuta kiwanja bila ya kumpa mtu *notice* ni sawa na kumnyima haki ya kusikilizwa. Haki ya mtu kusikilizwa ni haki ya kikatiba, kifungu cha 12(6)(a) cha Katiba, ingawa Sheria ya Ardhi humlazimisha waziri, lakini Katiba inamlazimisha mtu asikilizwe kwa kutoa nafasi sawa kumpa mtu asikilizwe.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuisoma Katiba ya Zanzibar ninayo hapa, Kifungu cha 12(6)(a);

Kifungu cha 12(6)(a);

> "Wakati wa haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uwamuzi wa Mahakama au chombo chengine kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa..." Naomba nirudie tena, "...mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa na pia haki ya kupata kitulizo chenginecho kisheria kutokana na maamuzi ya Mahakama ya chombo hiki."

Mhe. Waziri, Katiba ipo chini ya sheria. Sasa nilikuwa nataka maelezo yako kuhusu ufutwaji wa ardhi. Hii Katiba ipo chini ya sheria, je utafuata Katiba?

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, umemfahamu. Hebu tupe maelezo.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Jaku Hashim, ni hoja ya msingi. Lakini kila jambo lina kiwango, kiwango kikishapita, nafikiri itakuwa tena mnachelewa katika kutekeleza mambo yenu. Wale ambao wamepewa ardhi wamekaa nayo kwa miaka miwili, miaka miwili imemalizika hawajajenga wako kwenye mwaka wa tatu, umemalizika unastahamili, umeshaingia mwaka wa nne imemalizika hawajajenga, bado unaendelea kustahamili, unaingia mwaka wa tano hawajajenga bado unaendelea kustahamili. Ikishafika miaka 10 Mhe. Mwenyekiti, imeshapita kiwango maana yule amedhorotesha maendeleo.

Pia, kuna suala la kujenga maendeleo ya nchi. Kwa hivyo, mimi nakubaliana na yeye, kwa wale waliokuwa kwenye kipindi hiki huwa tunawaita na tunawapelekea *notice* na kuwasikiliza. Lakini kwa wale waliokwishakuvuka, mtu ana ardhi miaka 12, miaka 14, wengine miaka 20, kweli huyo ana nia ya kujenga na wala hajaja hata kutujulisha. Kila jambo Mhe. Mwenyekiti, kwa mawazo yangu mimi naona yana kiwango, yakipita kiwango ndugu zetu Wanyamwezi wanasema kinehe tena.

Ahsante sana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini anapotoa hicho kitu tofauti na wenzetu duniani. Nilimwambia jana kati ya mawaziri waliotembea mmoja ni yeye, *Mashaallah Alhamdulillah* keshatembea sana. Leo unampa mtu kiwanja miundombinu hakuna, maji hayapo, barabara haipo, umeme haupo, huku si kumuonea Mzanzibari. Hapana miundombinu, maji akayachukuwe wapi Paje na akajenge Tunguu.

Isitoshe kama hapo hapatoshi Mhe. Mwenyekiti, mimi nina shamba langu nimeliuza kwa mwekezaji, kama dola milioni moja au milioni mbili. Lakini mwekezaji yule hakwenda serikalini kuwekeza, leo anakuja kupokonywa *lease* yake kwa msingi gani? Kweli tunataka wawekezaji waje wawekeze? Miundombinu hujapeleka, umeme hakuna, maji hakuna, barabara hakuna, ardhi ile kwenda kumfutia Mzanzibari, kweli tumemtendea haki, peleka ile miundombinu halafu ujenge hoja, tusiende hivi.

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie Botswana kiwanja unapewa, umeme unapelekewa, maji unapelekewa, mpaka *line* ya simu unapewa katika maeneo hayo. Sasa tusifukuzie kufuta tu, kufuta kwa huyu ukampelekea huyu, kwa misingi gani? Miundombinu hamna, maji hayapo, barabara hakuna. Mhe. Waziri, nataka ufafanuzi wako.

**Mhe. Mwenyekiti:** Una maelezo zaidi Mhe. Waziri? Kama nimemfahamu sawa sawa anategemea kwamba iende miundombinu kwanza. Nadhani ndivyo nilivyomfahamu mimi.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, ninachosema kwenye suala hii, ni kwamba sheria haikumzuwia waziri kutoa kiwanja kwa sababu hapana miundombinu. Hata hao wanaotaka viwanja hawatakuwa tayari kuwa wasipewe viwanja kwa sababu hapana miundombinu, watataka wapewe viwanja na wenyewe wanashirikiana hata na serikali kuomba kufikishiwa miundombinu, ndivyo tulivyofanya na ndivyo tunavyofanya katika miradi mingi inayojengwa. Tunawapa viwanja hakuna miundombinu, wakianza ujenzi na sisi tunahamasika, tunawaambia watu wa umeme pelekeni umeme pale kuna mradi mzuri, pelekeni maji kuna mradi mzuri. Ananunua maji wakati anapoanza mradi, lakini hawahi kumaliza mradi maji tayari yamefika pale. Kwa hivyo, sheria haikumzuwia waziri asitowe kiwanja kwa sababu hapana miundombinu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim, nadhani umempata vizuri Mhe. Waziri.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini sheria ipo chini ya Katiba, Katiba ndio yenye nguvu. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nashukuru kusema kwamba tuendelee. Katika hali ya kawaida kupeleka miundombinu pahala ambapo hapana mtu, wakati kuna wahitaji wengine, watu watasema hivi huyu waziri na yeye anafanya nini. Anapeleka huduma pahala hakuna mtu wa kutumia. Tuendelee. *(Makofi)*

**KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UPANGAJI WA MATUMIZI YA ARDHI**

| | |
|---|---|
| Programu Ndogo S01 Utawala wa Ardhi | Shs.1,11,941,000 |
| Programu Ndogo S02 Upangaji wa Miji na Matumizi ya Ardhi | Shs. 270,055,000 |
| **Jumla ya Kifungu** | **Shs.1,281,996,000** |

**KIFUNGU P03 - PROGRAMU YA UHIFADHI WA MJI MKONGWE URATIBU NA USIMAMIZI WA UJENZI**

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nina dogo sana, naamini Mhe. Waziri, alikuwa anataka kunijibu, lakini dakika zako kidogo zilimzuwia. Niliulizia zile *documents* mbili nilizompa, namshukuru sana kwamba ile moja inayohudu ile ardhi ya yule mwananchi wa kule Mangapwani amenijibu vizuri. Lakini pamoja na kunijibu nitaomba yule muhusika nimpeleke kwa Mhe. Waziri, ili akapate muongozo kama lile eneo lake litachukuliwa.

Hoja yangu hapa ile *document* ya pili ambayo ilikuwa inahusu ile kesi ambayo ilikwishakuamuliwa na Mahakama ambayo Mkurugenzi wa Mamlaka ya Nyumba kama sikosei ndiye aliyeshtakiwa pamoja na wenzake. Sasa hili naamini jawabu atakuwa nalo kutokana na muda tu hakuwahi. Ni hivyo tu Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma, ile ya kwanza, kwenye ile ardhi ambayo kuna mtu amedai kwamba ni eka yake, kama alivyosema mwenyewe nitaendelea kulifanyia kazi na hata mtu huyo akimleta nitaendelea kuulizana na yeye na kujua hali ile. Pia, kama nilivyosema tutafanya jitihada ya kumtafutia sehemu nyengine, kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo. Hayo mambo nakubaliana na yeye na nitayafanya.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ile hoja niliyokuwa sikuijibu ya ile kesi iliyokwenda Mahakamani, tuliitizama vizuri ile kesi. Kesi haikurejesha ule mlango kwa wale

wahusika, kwa Mahakama imechukua uwamuzi wa mlango ule kuurejesha Idara ya Nyumba. Kwa hivyo, tumerejesha Idara ya Nyumba. Sasa suala la nani tutampa sasa, ni uwamuzi wa wizara sasa hivi, baada ya kuwa lile suala limerudi kwenye Idara ya Nyumba. Lakini wale kwa mujibu wa kesi na siku ile nilimfuata, nikamwambia nipe ile hukumu akanipa nikaiangalia na nikawapelekea wanasheria wakaisoma, wakasema kesi hii imerejeshwa kwa Idara ya Nyumba.

Kwa hivyo, nafikiri sasa hivi ni kutizama tu uwezekano wa nani kumpa kipaumbele cha kumpa ule mlango, maana mlango sasa hivi ni mali ya Wizara ya Nyumba moja kwa moja, ndio maana tukauweka pale. Tuliwahi kuupangia hata matumizi, kwamba sasa hivi ule mlango bora utumike na Idara ya Nyumba kwa ajili ya kutukusanyia mapato ya nyumba, kwa sababu sasa wanaanzisha Shirika la Nyumba. Hata hivyo, hiyo haitufungi kufikiria jambo jengine kwa kutizama ile historia ya mlango ule namna ulivyokwenda. Ahsante sana.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri, pamoja na timu yake kwa kuwa makini kwa hoja ambazo tunazoziwasilisha, sasa kwanza nilikuwa nina ushauri pale ukipaangalia kwamba kwa sasa hivi wameamua kuweka kama Ofisi ya Ukusanyaji wa Mapato, si busara sana kwa watendaji wetu mtu ametoka nyumbani na suti yake kumpeleka pale akapigwa magunia na wachukuzi.

Sasa mimi nafikiri kama alivyosema kwa kuwa umerejeshwa Serikalini, namuomba sana Mhe. Waziri, kama kawaida yake atumie sana busara ya nani wa kumpa eneo lile sitaki kumuingilia kati nikamwambia mpe fulani, lakini naamini atatumia busara kama kawaida yake. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu P03

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, niendelee tena kumpongeza Mhe. Waziri, kwa umakini wake na alipokiri barua aliyoandika Mhe. Mohammed Aboud inatakiwa utekelezaji hilo amekiri, lakini utekelezaji wake ni wa muda mrefu hii barua ninayo mimi hapa kama kiambatanisho, anijibu tu Mhe. Waziri, hiyo ruhusa ataitoa lini? Kesho, keshokutwa, hii barua imekaa muda mrefu bila ya ufumbuzi wowote, sijui kama ilikuwa inaandikwa *heading* moja moja haijesha mpaka hii leo.

La pili, hoja yangu Mhe. Waziri, yeye ni mzoefu wa muda mrefu, hivi sasa tunakuwa na wakati ulipokuwa Waziri mwanzo ulipewa gari ya mchele, baadae ikabadilishwa ukapewa cressida hivi sasa una Prado hivi ndio hali inavyokwenda, utumizi wa mawe Mji Mkongwe hivi sasa unahatarisha vianzio kwetu, na wengine kuruhusiwa wajenge matofali matupu sheria unaruhusu vipi. Mawe hivi sasa yameshakuwa taabani wakulima wetu mabigili yao yameshakuwa na shida huko

vijijini, hasa haya majimbo ya shamba, tutamke tu hakuna haja ya kujenga kwa matofali wakati matofali wanajenga wenzetu, waliojengea mawe wakati huo shida, ilikuwa dhiki hakuna matofali mtoto akizaliwa haendi mbio hutambaa akaweza kwenda na wakati tuna simu za mikononi.

Yale mawe ulipokuwa unajengwa wakati huo Mji Mkongwe ni shida, ile ni dhiki, hakuyataka, hivi sasa kuna matofali hakuna sababu, tunajenga maeneo mengine yakijengwa kwa matofali matupu na yapo mpaka hivi sasa Waziri naomba atamke kuwa mambo ya mawe sasa katika Mji Mkongwe sasa basi, na hoja ya hii barua lini ije ichukuliwe kibali chake cha huyu mjenzi anayetaka kujenga.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri Mhe. Jaku, lakini maneno yangu nilisema kama tunataka tuendelee katika masuala ya urithi wa Kimataifa, hivi sasa hivi Mheshimiwa jiwe hatulijengei udongo, na zipo nyumba pale Mji Mkongwe zimeshajengewa mawe, lakini hawakutumia udongo wanatumia mchanga na saruji, ambayo inakuwa madhubuti na inakuwa madhubuti kweli kweli na ile sifa ya kwamba lile eneo la Mji Mkongwe ni *Stone Town* bado linabakia jina liko pale pale kama ni *Stone Town*.

Sasa mimi namuomba tu ilikuwa unajenga nyumba nzima kwa mawe, na wala sisi hatukusema basi utumie na udongo. Zile sehemu za nje jenga kwa jiwe, ndani kata matofali yako fanya *partition* yake, wewe *aluminum* kama unataka humo ndani, lakini nje ukuta uwe kama ukuta wa jiwe, na nyumba ipo katika *Stone Town* silioni ugumu wake, na kwa sababu anajenga ukuta wa nje tu sidhani kama anatumia mawe mengi sana, ndani mwache ajenge matofali atie na vitu vyengine. Nyumba yake iwe kama ile nyumba ya yule Malkia yule Balkis kwa inavyong'ara mle ndani, si tatizo hilo Mheshimiwa, lakini kuta za nje azijenge kwa mawe.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ilikuwa hoja zangu mbili ya mwanzo ndio kaijibu hivyo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Umemfahamu vizuri lakini.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Sina tatizo na alivyojibu nimemfahamu sana tu, ilikuwa hoja zangu ni mbili.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ili jina *Stone Town* libaki basi huku nje kuwe na jiwe, haya twende!

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hoja hii nimeikubali wala haina matatizo yoyote, lakini hoja ya hii barua aliyoandika yeye kama ni Waziri sasa, kama yeye ni Waziri sijui kama kasaini Mkurugenzi au Katibu, nani mkubwa

kati yao. Barua hii mpaka muda wa leo haijafanyiwa utekelezaji, ikiwa barua hii kaandika yeye kama ni Waziri kwa watendaji wake mpaka leo haijapata maamuzi.

Leo kakiri kwamba ataifanyia maamuzi namshukuru sana Mhe. Waziri, lakini lini maamuzi yake? Kesho, kesho kutwa ili mtu aje kuchukua kibali chake cha ghorofa ya tatu, ni hilo tu nafikiri litakuwa halina ubishi Waziri atalikubali, nafikiri ataniambia kama kesho au kesho kutwa Mwenyewe Mhe. Waziri kwa niaba ya Mhe. Mohammed Aboud kuhusu ghorofa tatu, lini atatoa? Kesho au kesho kutwa hiyo barua.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, barua ilikuwa ni ripoti anayotukabidhi Mhe. Mohammed Aboud, anatukabidhi *Hansard* na anatwambia hivi mlipojibu swali tarehe kadhaa nilizungumzia masuala haya ambayo ni ya kisheria, kwa hivyo ninakuleteeni hii *Hansard* muisome ili mutekeleze kwa mujibu wa Sheria inavyoeleza katika hii *Hansard,* na kaambatanisha na *Hansard* pale, ambayo ndani yake mlikuwa na mambo mengi sio hilo tu, kuna mambo mengine ilikuwa mimi na Mhe. Jaku tufuatane tukatizame nyumba zilizopita urefu, kuna masuala mengine mle ndani; ya kwamba tuhakikishe nyumba zinatizama zinalingana kwa mujibu wa urefu wa kwenda juu, imo ndani ya ile *Hansard*, ukitizama *Hansard* imo namna alivyojibiwa lile suala.

Mimi nadhani sina hakika lakini mwenyewe anaweza akanithibitishia katika makubaliano ya ujenzi wa nyumba ambayo anaishughulikia, yeye amekubali kufuata utaratibu huu huu wa kujenga nje kwa mawe ndani kukata kwa matofali, sasa kuna matatizo ya nini, na akamilishe ujenzi wa ile nyumba, Mheshimiwa hatuna tatizo katika hilo sisi na tumeshamkubalia. Sisi tumeshamkubalia atafute mawe ajenge kwa nje, na ndio maana ukipita hiyo nyumba utaona iwazi mle pembeni, apite afanye kazi hiyo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tumalizie Mhe. Jaku.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:**Mhe. Mwenyekiti, suala si mawe mimi nafikiri nisome hii *Hansard.* Hichi chombo kipo kwa niaba ya wananchi;

> "Sheria ya hifadhi ya Mji Mkongwe wa Zanzibar zimekuwa kikomo mwisho wa idadi ya ghorofa kwa majengo yaliyojengwa na kukadiriwa ghorofa tatu, hivi karibuni tumeshuhudia majengo zaidi ya ghorofa tatu yakijengwa katika mji huo".
>
> a) Wizara kazi yake kusimamia sheria au kuvunja sheria kutokana na ujenzi huo kufanyika na viongozi dhamana wanaoshughulikia.

b) Kwa nini wafanyabiashara wakubwa na wawekezaji wanaruhusiwa kujenga zaidi ya ghorofa tatu nawananchi wanyonge wakikatazwa na sheria hii, hivyo kitendo hicho si cha ubaguzi kwa Katiba ya Zanzibar inayosema binaadam wote ni sawa mbele ya Sheria.

c) Kufanya vitendo hivyo bila ya uongozi dhamana kuchukua hatua tunajenga msingi wa utawala bora.

Mheshimiwa, kakiri humu na naomba kuisoma kwa haraka haraka, Mhe. Spika, mimi nilichokizungumza nimezaliwa shamba nimesoma shamba, nimekuwa shamba na hivi sasa nusu mjini sasa hawezi kuja kunidanganya mtu kwa hili, ikishindikana hapa hili suala litakuwa nalileta Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi naomba niongeze majibu kwa Mhe. Jaku kama ifuatavyo.

Mheshimiwa nilivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Makaazi kwamba Serikali inaendeshwa kwa mujibu wa taratibu za kisheria zinazotokana na Katiba, nifupishe pale ambapo eneo lipo tupu ujenzi unaruhusiwa ghorofa tatu Kiswahili ninachozungumza, pale ambapo eneo tupu la ujenzi linaruhusiwa ghorofa tatu.

Chombo kama hichi kinatoa maamuzi ndani ya chombo hichi, wengine kuruhusiwa wengine ghorofa tano wengine nne chombo kama hichi, barua ya *Hansard* ipelekwe kwa watekelezaji huu, utekelezaji hauna jawabu wanaogopa kujibu kwa suala hili hiki kitu kiko wazi, hizo nyumba ziko jirani yake ghorofa tatu pale pale yeye acha akae Wizara ya Ardhi, Wizara ya kilimo ina ghorofa tatu. *PBZ* pale ina ghorofa tatu sasa hili suala alikubali tu hili halitaki tochi.

Mhe. Waziri utakaa Waziri wa Ardhi kukaimu Wizara unayokaa ina ghorofa tatu au nini maana ya ghorofa tatu, ikiwa barua kama hii hakuna jawabu lake inashindwa kujibiwa mpaka muda wa leo, haiwezekani, tuwe makini katika utendaji.

Barua hii hapa ya *Hansard* na hili suala nimeliomba kwa muda mrefu Mheshimiwa Waziri niliahirishe nimeahirisha, lihairishe naahirisha natii amri yako na hilo tukubali.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa kuna maelezo zaidi.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:**Mhe. Mwenyekiti, tunacho-*determine* hasa katika masuala ya ujenzi wa Mji Mkongwe ni *height*, kama *height* ya nyumba zilizoko pale ambapo anajenga jengo lake liko kwenye ghorofa tatu; *height* zilizomzunguka pale na yeye anataka kujenga ghorofa tano, wako watu pale

pale Mji Mkongwe hawakuongeza *height* lakini wamejenga ghorofa tano lakini *height* haikuvuka, ni aina ya *ceiling* na *floor*, uki-*determine* hivyo unapata hata ghoroga tano.

Lakini sasa ukitaka ile *height* ya kawaida ambayo jumba likachomoza juu pale Mji Mkongwe hulingani na majumba ya wenzio, ingelikuwa tuna nafasi ya kuendelea na nafasi ya kutosha ningemchukua Mhe. Jaku nikampeleka *Saint Petersburg* pale nikamuonesha *heritage city* ya *Saint Petersburg*, haivuki urefu ule, hata kama itakuwa ghorofa saba, lakini haivuki *height* ile, utafikiri zimekatwa kwa mkasi. Hata ukienda Muscat ananiambia Mhe. Juma Duni haivuki katika urefu ule na ndivyo tunavyotangaza *master plan* nyumba za eneo hili ghorofa tatu, nyumba za eneo hili ghorofa kumi, nyumba za eneo hili ghorofa hamsini, inategemea na lile eneo ulilotaka, ndivyo tunavyopanga miji.

Waheshimiwa wanisaidie tupange mji, hicho ndio kitu muhimu kusema kweli, kuna maeneo utachukua ghorofa tatu, kuna maeneo utachukua ghorofa tano, sasa wewe kama umepewa ghorofa tano na wewe mwenyewe unataka ziwe saba punguza *ceiling* ili utapata hizo ghorofa unazotaka, alimradi tu Mhe. Spika, ni *height* na kule juu kunakuwa kile kipaa kidogo cha kunywea kahawa kutizama mandhari, unajenga kule juu kijipaa kidogo, kizuri, hakina vyumba, unakaa kule unawatizama watu wa Mjini, gari zinavyopita unazihesabu, ndio raha yenyewe hiyo Mheshimiwa! Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nadhani Waziri aliweka uwazi sana, kwamba suala kubwa muhimu katika Mji Mkongwe mbali ya habari ya jiwe ni *height*, kama *height* inasema ziwe mita kwa mfano mita ishirini, basi wewe zitumie mita ishirini kwa kujenga ghorofa unazotaka, ndio anachosema Waziri, ilimradi isipitize ile *height* inayokubalika katika Mji Mkongwe. Nadhani Mhe. Jaku hili sasa uliangalie ili tupate kuendelea.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Waziri, nimuombe tu kama mimi na yeye baada ya muda mrefu kupanga safari zetu mimi na yeye zikawa hazitekelezeki katika chombo hichi hichi, ni lini twende pale tuchukue na wataalamu tukapime ili kuhakikisha ninachozungumza ni cha ukweli au cha uongo. Kesho au kesho kutwa, lakini anipe kauli hao tu ameshanipatia chombo hichi hakuna safari hata moja tuliyokwenda, twende mimi na yeye na watendaji akaone ukweli na uhalisia ukoje.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku hebu hayo shirikiana na Mhe. Waziri, pamoja na Wizara ili mkatekeleze hayo ambayo mnaona, lakini tena tusianze kufanya vitimbwi ndani ya chombo hichi, utakwenda Wizarani ili mkakubaliane!

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia hotuba hii nilitaka nipate maelezo kuhusu hatima ya wakaazi waliomo katika Majumba ya Mji Mkongwe jumla ya Majumba 129 ambayo yamo katika hali mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aliposoma kitabu chake katika kifungu cha 46 kifungu kidogo cha 5 alisema kuwa;

> "Pia katika ukaguzi ulifanywa katika Nyumba za Serikali Mji Mkongwe Zanzibar imebainika kuwa nyumba 26 ziko katika hali mbaya na zinahitaji matengenezo makubwa na ya haraka. Hatua tayari zimechukuliwa za kuwajulisha wapangaji juu ya ubovu wa majengo hayo na hatari ya kuendelea kuyatumia majengo hayo".

Mimi binafsi kwanza nishukuru kwa kufanya utafiti na kuona hii hali, lakini sikuridhika kuwa hizi ndio hatua za Serikali za mwisho kwa kujali maisha ya wananchi, kwa sababu nyumba si hizi 26 tu, kuna na nyengine za Kamisheni ya Wakfu, kuna nyumba za Watu binafsi na jumla ya nyumba 129 na zote zimo katika hali mbaya zinahatarisha sana maisha ya wakaazi ambao hatujui watakwenda wapi.

Nilitaka kujua, Wizara hasa ina msimamo gani juu ya matengenezo ya nyumba hizi na watu hawa wamefanyiwa mpango wa kuhamia wapi ili nyumba zitengenezwe warudi waweze kuishi katika hali ya usalama na amani lakini sikupata jibu, naomba maelezo.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:**Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe amezungumza kwa usahihi kabisa, kwamba katika Mji Mkongwe kuna nyumba za Serikali moja kwa moja zinamilikiwa na Idara ya Nyumba, kuna nyumba za Wakfu na Mali ya Amana, kuna nyumba za watu binafsi zote zimo ndani ya Mji Mkongwe, Wizara yangu inashughulikia kwa nguvu zaidi kwa zile nyumba za Serikali, kwa sababu nina mamlaka nazo kwa sababu ni zangu, kwa hivyo hizi nazishughulikia.

Katika suala la nyumba ya Wakfu tunawasiliana na watu wa Wakfu kuwaambia kwamba nyumba fulani tumeikagua nayo mbovu itengenezeni, inahatarisha maisha ya wananchi. Na wao wanatakiwa watafute vifungu vyao wakaifanyie matengenezo nyumba ile, katika watu binafsi tunawaandikia, nyumba yako hii ni yako wewe lakini inahatarisha usalama wa watu wa *round* hii hebu ishughulikie hii nyumba uitengeneze hiyo kazi tunafanya.

Kwa hizi nyumba zetu 26 nimesema mimi katika hotuba yangu tumeshakubaliana hatuna pesa nyumba mbili tuziuze, tutaziuza zile nyumba mbili tutapata pesa za kuweza kufanya matengenezo nyumba zitakazobakia pale, katika ishirini na tano, unaacha hii ya *chalk building* ambayo ndio ya 26, mbili tunaziuza, nne

tunawakabidhi watu kwa njia ya *PPP*, ili wao watengeneze kwa kushirikiana na Serikali, ili kuzilinda zile nyumba zisizidi kuendelea na ubovu zaidi, hizo ni mbovu sana, zilizobakia tukipata pesa hizi tunategemea kufanya matengenezo zile nyumba nyengine, tutakachotakiwa kufanya kuwaomba wale waliokuwemo mle watoe nafasi zile nyumba tuzifanyie matengenezo.

Kwa sababu wasipotoa nafasi hazitengenezeki Mhe. Mwenyekiti, majumba ya udongo hawezi kukwambia mtu mimi nakaa ndani na wewe tengeneza huko nje, udongo unaweza ukalitoa jiwe pale chini likashuka lote, hiyo ndio hatari! Ndio maana tukawa tunazungumza habari ya *chalk building* hapa itabidi watu watoke watupitishe mle tutengeneze, baadae tukawa na makubaliano ya kurudi watu wale wale.

Kwa hivyo, kwa hawa watu binafsi ndio kama ninavyomjibu utaratibu uliopo ni kuzungumza nao, wazitengeneze nyumba zao hawaziwezi waziuze wawape watu wanaoweza kuzitengeneza. Wakfu nao washughulikie nyumba zao, watengeneze na zetu tunazishughulikia sisi wenyewe, hivyo ndio tunavyokwenda nao, na ndio maana sisi tumefika sisi wenyewe kwa zile za Serikali zimeshafikia hatua nzuri. Nimeshazungumza na *ZSSF* wameshakubali kutengeneza *chalk building*, wameshaamua kuuza nyumba moja kubwa tu itatupatia pesa nyingi tu ambazo tutapata fedha za kuanzia ujenzi katika maeneo haya na kukusanya kodi, na pia tutakwenda kwenye *PPP* kutengeneza nyumba angalau nne hivi.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata jibu lakini nina maswali mawili madogo. Suala la mwanzo Mheshimiwa pamoja na maelekezo mazuri ya Mhe. Waziri aliyoyatoa kuhusu hatma ya matengenezo ya nyumba zile kwa namna alivyoona inafaa, lakini kitabu chake kimeandika kuwa hatua tayari imeshachukuliwa ya kuwajulisha wapangaji juu ya ubovu wa majengo hayo na hatari ya kuendelea kuyatumia majengo hayo.

Anazungumza hivyo lakini wamo na wameshasema kuwa ni mabovu na ni hatari kuyatumia. Je, Mhe. Waziri, hakuona kuwa kuna umuhimu wa kuchukua hatua za dharura kwa vyovyote kama inawezekana hawa watu wahamishwe, tungojee haya matengenezo halafu kurudishwe kulivyokuwa, kuliko kuachwa hivi hivi tokea ukoloni hivi ikaja ikatokea hatari hapo baadae, hilo ni suala la mwanzo.

Halafu la pili kwa sababu hii ni Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, na hizi nyumba nyengine ziwe za Wakfu au ziwe za watu binafsi, lakini ni nyumba zinazokaliwa, na Wizara yake ni hii sasa kama hawana mamlaka ya kuona kuwa wao ndio wenye uwezo wa kuyatengeneza.

Je, Mhe. Waziri, kwa kutumia hao watu wanaohusika anachukua hatua gani za haraka ili kama ikitokezea hatari yoyote wajue pa kushika? Kuliko kuwa keshatoa taarifa tukaendelea na maisha haya wakati anahatarisha amani.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, hii kazi tunapoifanya matumaini yetu ni kwamba tutapata mashirikiano na wale wanaohusika, yaani wananchi wanaokaa mle ndani. Tunategemea tutapata mashauriano, tutapata mashirikiano na tutakubaliana. Tusingependa sisi tufikie hatua ya kumuhamisha mtu kwa lazima kwa kutumia mtutu wa bunduki. Si vizuri katika nchi ambayo watu wenyewe wamejitawala. Kwa nini tufikie katika hatua hiyo, tunawaomba watupe ushirikiano. Wafanye maarifa nyumba tuzipate tuzifanyie matengenezo, kulikoni kumtoa mtu mle kwa mtutu wa bunduki. Kwa nini tufanye hivyo? Hatuna sababu ya kufanya hivyo. Tunataka mashirikiano kutoka kwa wananchi.

Na wale wenye majumba nao tunataka na wao watupe mashirikiano katika kazi hii. Tusingependa sisi tutumie vishindo tuwatoe kwa virungu na nini, tukimwambia Mhe. Haji Omar Kheri, akipeleka watu mle. Ya nini yote hayo, haina haja ya kufanya hayo, tupewe ushirikiano na wananchi wanaohusika tutengeneze majumba yale. Mimi naona ndiyo vizuri tuwe hivyo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nafikiri maelezo Mheshimiwa yapo wazi sana na anavyosema inafahamika vizuri. Nadhani tuendelee.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru maelezo yako wazi sana, lakini mimi sikuridhika na jibu kutokana na umuhimu wa kuenzi maisha ya wananchi, tuendelee.

**KIFUNGU P03 - PROGRAMU YA UHIFADHI WA MJI MKONGWE URATIBU NA USIMAMIZI WA UJENZI NA NYUMBA ZA SERIKALI**

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi na Nyumba za Serikali | Shs.757,854,000 |
| Kifungu S02 Programu Ndogo ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe | Shs. 360,047,000 |
| **Jumla Kifungu** | **Shs.1,117,901,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P04 PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA UZALISHAJI NA USAMBAZAJI WA NISHATI NA MAJI**

Kifungu S01 Programu Ndogo ya Usimamizi na Usambazaji wa Huduma za Maji na Nishati

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni ndogo sana na nasimama kwenye H(14) kwenye kulijengea uwezo Shirika la Umeme.

Mhe. Mwenyekiti, Kulijengea Uwezo Shirika la Umeme ni pamoja na kuiweka salama miundombinu ya Shirika hilo. Mhe. Waziri naomba kidogo anielimishe, nilimuhoji kwenye maandishi yangu kwamba *transformer* iliyopo Mlandege imejengewa uzio wa ukuta.

Jambo ambalo *transformer* ile ikitokezea bahati mbaya kuripuka *ZECO* wala Zimamoto hawatapata namna ya kuzima moto ule. Wakati Shirika limetanga bilioni 11 kujenga uwezo, lakini uwezo wa Miundombinu ya *ZECO* inabanwa kwa kiasi kile. Naomba kujua ni agizo la *ZECO* kujengwa ukuta au ni Mji Mkongwe wamejenga ukuta au nani ametoa kibali. Naomba hilo tu.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nalichukua swali lake kama ni rai ambayo tunatakiwa tukaifanyie kazi, kwa kushirikiana na *ZECO* kwenda kulifanyia kazi suala hilo sio kumpa jibu kwenye suala hili.

Mimi nimeona katika maandishi yake. Nikasema kwa ghafla hii, maana kama ningekuwa nimepata nafasi tangu juzi ningelifanyia kazi, lakini nimelipata leo asubuhi. Kwa hivyo nimelichukua kuwa ni rai tutakwenda kulifanyia kazi na *ZECO.* Ahsante sana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, sitaki nipingane na Mhe. Waziri lakini nimkumbushe tu kwamba jambo hili limezungumzwa zaidi ya bajeti nne nyuma. Ukiangalia kwenye kumbukumbu ya *hansard* zako jambo hili la *transfomer* hii imezungumzwa zaidi ya miaka mitatu nyuma kwamba ile *transformer* ipo ndani ya uzio wa ukuta.

Kwa hivyo, ingekuwa ni rahisi tu kuambiwa kwamba ni agizo la *ZECO* tukaendelea mbele. Lakini mimi ninavyoamini kwamba *ZECO* hawawezi kuwa rahisi kukubali *transformer* ikazingirwa ukuta wa matofali kwa usalama wa miundombinu ya *ZECO,* naamini haiko rahisi kuweza kulikubali hilo.

Sasa mimi nilitaka kujua tu huyo aliyetoa kibali kwamba *transformer* yenye umeme mkubwa chini ya makaazi ya watu ikajengewa ukuta wakati iko katika mji wakati sio Sera ya *ZECO* ilikuwa niambiwe. Kama ni rai mimi sioni kama ni rai, naona ni jambo la msingi wala sikusudii kutoa rai, mimi nakusudia kwamba niambiwe, huyo aliyetoa kibali ni nani? Ni *ZECO* ndiye aliyeruhusu kwamba ile *transformer* ihifadhiwe au mfanyabiashara au Mji Mkongwe au Idara ya Ujenzi, hilo tu nisaidiwe, hilo tu!

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, nimesema nakubaliana na yeye labda ana wasi wasi wa utekelezaji. Mungu akipenda Mhe. Hija Hassan atarudi kwenye Baraza hili atakuja kuiona hiyo hali *Inshallah*, aniachie.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, naomba Mwenyezi Mungu atujaalie turudi mimi na yeye ili nimkumbushe *Inshallah* na mapema mwezi wa 11 tukifika. Tuendelee.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri. Lakini itakuwa sikumfanyia haki Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji, na watendaji wake wote kwa jitihada, na kwa muda niliokaa nao kwa mashirikiano makubwa kwa jimbo la Muyuni kuhusu Sekta ya Maji. Niwashukuru Bwana Iliyasi, Mkurugenzi Mkuu Mustafa, Maulidi na Mshika fedha Ali Tamimu kwa mashirikiano waliyonipa. Lakini bado Waziri umenijibu sana lakini kuna kitu cha kusikitisha sana kuwa unasema haiwezekani mifereji ya nje itachangishwa. Si kitu kizuri na tokea ukoloni hicho kitu kipo. Lakini kwa kuweka *hansard* sawa jimbo la Muyuni kama kuna kazi iliyofanyika imefanyika kazi kubwa ikiwa ni pamoja na mimi na serikali. Lakini bado nataka itoke kauli kwa jimbo la Muyuni kwa mifereji ya nje isije ikaguswa. Maana yake hata vile vichwa vya juu nakwenda kuhangaika mimi kuvitia sio *ZAWA* wanaopeleka kule, nahudumia mimi kama Mwakilishi. Kwa hivyo Waziri nataka aweke *hansard* sawa kwa mifereji ile isije ikaguswa. Nataka kauli kutoka kwa Waziri.

La pili Mhe. Waziri ulipokuwa unajibu umesema Fungu Mbaraka ni mali ya Zanzibar, hapa hapa unajibu hata nusu saa haijafika. Halafu tena unasema pana uwezekano wa makubaliano yaliyokuwepo. Sasa unajibu nini? Kama Fungu Mbaraka ni mali ya Zanzibar pana makubaliano gani tena na wenzetu.

Ukishasema Fungu Mbaraka ni mali ya Zanzibar, kuna makubaliano gani tena na wenzetu? Lakini unasema hatukosani na wenzetu. Nani mwenzetu katika Fungu hili? Fungu Mbaraka ni mali yetu, sasa unasema hatukosani na wenzetu. Nani katika ushirika huu? Hebu twambie? (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la mifereji ya nje nimemsikia, lakini mifereji ikiwa mingi mahala pamoja ya nje tutaipunguza. Lakini kwa kiasi ya kuweka mfereji kwa watu waliokuwepo maeneo yale ambao hawatopata huduma ya maji hiyo tutaendelea nayo. Mifereji hii itahudumiwa na *ZECO*, na wala hawatochangishwa wananchi hiyo namueleza wazi sina sababu ya kumficha.

Suala la Fungu Mbaraka Mheshimiwa Tanzania sisi hatuna tabia ya kugombana baina ya Bara na Zanzibar, tunaimarisha Muungano wetu. Matatizo yaliyokuwemo ndani ya Muungano tunayatatua kwa umoja wetu kwa kukaa katika vikao tukashauriana.

Mhe. Said Ali Mbarouk alikuwa ni Waziri wa masuala ya Uvuvi, alikuwa ana tatizo la Uvuvi wa Bahari Kuu, mbona tumefika mahala tumeelewana. Tunajua atakapovuliwa samaki asilimia ngapi. Mafuta tumeyaondoa kwenye Katiba, ipitishwe Katiba hii mpya, tukishakuyaondoa tunazungumzia ni wapi na wapi sisi petu.

Hawa wenzetu wamekwenda pale, kwa sababu tusijekusahau kwamba tulipeleka *jurisdiction* ya kutoa leseni kwa *TPDC* hatuwezi kui-*abuse jurisdiction* ambayo tuliitoa kikatiba, lazima tuitengue kikatiba vile vile. Iondoke kwenye Katiba iwe yetu, turingie maeneo yetu na tutaelewana. Msitegemee kwamba hatutoelewana katika hili. Tusitake kuingia kwenye vurugu tukasema kwamba labda leo tunakwenda kuchukua, kufukuza meli.

Hapana, mimi nawasifu sana vijana wetu wa *KMKM* tulipowaambia mbona tuna wasi wasi kwamba kuna meli kule walikwenda na wakaomba kuingia ndani kwa lugha zao za kijeshi,wakaelewana, wakaingia ndani, wakahojiana na askari wenzao. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa tunataka tumsikie Waziri anasema nini, kwa hiyo haya makofi haya hebu tuache kwanza tumsikie.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Wakaeleza *documents* zilizowafanya waje pale, wakaziona *documents* zilizowafanya waje pale. Wakasema sasa mnataka tufanye nini? Wale wakauliza. Je, tuwatimue? Wakaambiwa hapana, leteni hizo *documents* tuzithibitishe. Wakaja na *documents* huku na tukaziona na tukaanza kuchukua hatua ya kuandikiana Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kukumbusha mazungumzo yaliyokuwepo baina ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, na hilo ndilo linaloendelea sasa.

Sisi hatuna tabia ya kuingia kwenye migogoro kama wanavyofanya majirani zetu, na hatupendi tuingie hapo kwenye migogoro Mheshimiwa. Tutaelewana katika hili mimi sina wasi wasi. Kila sehemu yetu ya Zanzibar kwenye mafuta na gesi itabakia kuwa ni mali ya Zanzibar, hilo sina wasi wasi nalo kwa uhakika kabisa! (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub tunataka kuendelea.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Sawa sawa Mhe. Mwenyekiti, tuko ukingoni tena kumalizia sasa hivi. Mhe. Waziri, mimi madogo tu mawili nataka unifahamishe.

a) Ni kigezo gani cha kutaka kuing'oa mifereji ile wakati tayari imeshakuwa ipo na tayari imeshakuwa wananchi inawahudumia. Huwapi masafa marefu sasa hivi wananchi kufuata huduma hiyo ya maji.

b) Na utatoa utaratibu gani kutaka mita ngapi hata mfereji wa wananchi iwepo nje.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, namwambia tena kwa utaratibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, afahamu, kama mfereji uliowekwa nje umetoka katika nyumba ambayo chanzo chake cha kuingia maji ndani kimewekewa mita, mfereji huo hatuung'owi. Lakini ikiwa mfereji uliotoka ndani ya nyumba umewekwa nje chanzo chake ni kwamba yule aliyetoa ule mfereji hana mita, bora tuuondoe kuliko kuwaambia wananchi wachangie. Si vizuri kufanya hivyo. Lakini tutaweka eneo *reasonable*, kwamba hapa pana nyumba 15 au 20 ndivyo vijiji vyetu vilivyo, tunawawekea mfereji mmoja huo hapo, aliyekuwa hana mfereji ndani aje ateke maji hapa. Hatuna matatizo katika hilo na itahudumiwa na *ZAWA*.

Narejea tena kusema hiyo ndiyo hali halisi itakavyokuwa. Hatuwezi kuacha kila mtu katia ndani mfereji katoa nje mfereji, hapana, hiyo sio nzuri kusema kweli. Sasa tunataka hivyo kama mtu kaweka mita na tunafanya kazi ya kuweka mita. Tukishaweka mita na asambaze mifereji, lakini kama mfereji kauchukua katika bomba la serikali kasimamisha mfereji pale huu itabidi ungojee kwenye kile kioski tutakachokiweka cha maji pale. Hivyo ndivyo tutakavyofanya, huo ndio utarati utakaofaa. Hatutomnyima mwananchi maji, maji ni sadaka. Na hilo Shirika la *ZAWA* litabariki zaidi ikiwa wanatoa pesa kidogo kuhudumia ule mfereji uliokuwepo pale pembeni, hapo ndio itapatikana hiyo baraka inayokusudiwa. Atuachie Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tufanye hiyo kazi katika sura hiyo, hatutomtaabisha mtu kufuatia maji mbali, tutaweka *reasonable,* mfereji mmoja kwa wote, hivyo ndivyo tutakavyofanya na waliokuwa ndani watatumia maji yao ndani hatuna tatizo nao watalipia kama kawaida.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tunakushukuru Mhe. Waziri sasa tunaendelea. Kuna Mhe. Salim, ndiyo, nadhani tuanze na Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mheshimiwa Salim ulipata kidogo hebu samahani. Mhe. Kazija Khamis Kona.

**Mhe. Kazija Khamis Kona:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi. Mhe. Mwenyekiti, nilimsikiliza sana Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, aliponijibu kuhusu wananchi wa Kigomani.

Mhe. Mwenyekiti, sikuridhika na majibu yake, sasa naomba aniridhishe majibu yaliyokuwa sahihi, kwa sababu baada ya kufuatilia suala la kuhusu Hoteli ya Azanzi na wananchi wa Kigomani, tulichokigundua pale yule muwekezaji aliyaziba maji kwa kutumia zege. Leo ananambia maji tu yaliziba taka taka sio kwamba yalizibiwa zege.

Lakini kama hilo halitoshi Mheshimiwa ile miundombinu ya maji imejengewa juu pale, alijenga hasa juu. Kwa maana hiyo hata ikitokea athari kwamba maji yamepasuka mpaka abomoe ile sehemu. Sasa hebu Mhe. Waziri anifahamishe, je, yeye alipofuatilia aligundua maji yaliziba tu au mimi na wananchi wa Kigomani tunasema kitu sio cha kweli kwamba alituziba kwa kutumia zege.

Lakini hapo hapo nishukuru baada ya kulichangia suala hili siku mbili tatu hizi wamepatiwa maji, mwaka mzima baada ya kufuatilia hilo hawajapata maji. Sasa Mhe. Waziri atueleweshe hapa sio atusikilize tu. Yeye alifuatilia kwa kina na mimi nilifuatilia kwa kina, tulichokigundua muwekezaji ameziba kwa kutumia zege. Mwananchi atafaidika vipi hapo naomba anifahamishe.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Naibu Waziri, hebu mridhishe Mhe. Kazija Khamis Kona. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia vizuri maelezo ya Mhe. Kazija Khamis, lakini kama nilivyojibu hapo awali tumepata taarifa hii kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwamba kuna tatizo la Wananchi wa Kigomani kwamba hawapati huduma ya maji safi na salama.

Baada ya kuipata taarifa hiyo mimi mwenyewe nikawaita watu wangu wa Mamlaka ya Maji na tukafanya ziara na Mhe. Kazija pamoja na Mhe. Abdi Mosi kwenda kutafuta nini ambacho kinachosababisha hivyo pamoja na wenzetu wa Mamlaka ya Maji. Katika kufanya uchunguzi hatukugundua kwamba miundombinu hiyo imezibwa kwa zege kama hilo suala halipo. Kama nilivyojibu hapo awali ni kweli ilikuwa imeziba kwa mazingira ya kawaida tu ya taka, lakini sio kama Muwekezaji kaiziba kwa zege, tofauti kabisa.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba nilivyomjibu ndivyo sahihi, na watu wangu wa Mamlaka wamefanya kazi baada ya kuona kile ambacho kilichokuwepo na wakafanya jitihada wakahakikisha kwamba wananchi wa Kigomani wanapata huduma hiyo ya maji safi na salama kwa muda mfupi baada ya kuliondoa hilo tatizo.

**Mhe. Kazija Khamis Kona:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, sisi hatulumbani, bali tunachokisema hapa tunawatetea wananchi walio wanyonge. Muwekezaji ana uwezo wa kununua maji, leo unanijibu vile vile kwamba muwekezaji hakuziba kwa zege. Muwekezaji ninasema mimi kama Mwakilishi wa maeneo yale ameziba kwa zege, lakini pia hapo hapo ameyavuta maji kwa kutumia pampu kuingiza katika hoteli yake.

Sasa leo unanijibu hivi, mimi jibu hili sijaridhika nalo. Lakini sasa kama siku zote hizo unasema maji yameziba tu kwa taka, basi hata vichuruzi churuzi yasiende kule Kigomani, si mtihani huu?

asa naomba Mhe. Naibu Waziri suala hili anikubalie kwamba ni kweli muwekezaji aliziba kwa zege, lakini Wizara yangu itafuatilia na itahakikisha suala hili halirejei tena. Akiri hivyo tu basi, tuhakikishe wananchi wetu wanapata maji. Lakini tukiendelea kulumbana hapa hatutengenezi Mheshimiwa. (*Makofi*)

Kwa sababu kupitia chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi wananchi wanatusikiliza, Naibu Waziri alivyozungumza wanasikiliza na mimi kama Mwakilishi wao wananisikiliza jinsi ninavyozungumza. Je, ikitokea tena hapa wananchi wakichukua maandamano kumuendea muwekezaji huyu atasema nini? (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi namshukuru sana na nampongeza sana Mhe. Kazija Khamis Kona kwa kuwa mkakamavu kwenye suala hili na ni wajibu wake. Na wanawake kutetea maji ndiyo wanaotakiwa wafanye hasa, maana wao ndio wanaotutekea maji, wakatutelekea, wakatupikia, kwa maji. Kwa hivyo wanahitaji wapate maji ya uhakika! (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi namwambia kama hilo suala lipo na limeshaondoka namuahidi kwamba hilo suala halitorejea. *ZAWA* itafanya ufuatiliaji wa karibu kabisa na halitorejea tena. Isipokuwa tunapata tatizo moja Mhe. Mwenyekiti, tatizo tunalolipata ni kwamba pale Kiashangwe ilikuwa tuchimbe visima vinne kwa bahati tumebahatika kuchimba visima viwili. Tangi lililokuwepo Kiashangwe linachukua maji ya lita milioni tatu. Sasa kwa visima vile viwili halijai mara moja, kwa hivyo kuna siku wale hufunga maji ili kuyadunduliza yajae, na ikifika siku

wanayafungua ndio yanatumika. Kwa hivyo, kweli zinaweza zikatokea siku maji hayafiki kabisa kule mwisho Kigomani, kwa sababu zile siku ambazo wao wamefunga kwa muda kwa ajili ya kulijaliza lile tangi, ingekuwa visima vinne tatizo hili lisingekuwepo. Kwa hivyo, atuachie tunalishughulikia asiwe na wasiwasi katika hilo, na kafanya kazi yake na kafanya wajibu wake hakuna wasiwasi wowote. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Kazija Khamis Kona:** Baada ya maelezo ya Mhe. Waziri nami ninaridhika nayo kwamba atalishughulikia na atafuatilia, lakini na mimi ninamuahidi nitafuatilia ikiwa bado nitapiga hodi katika wizara yake mpaka nihakikishe maji yanaenda ipasavyo.

Ahsante Mwenyekiti tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Naona sasa tumeridhika, na Mhe. Salum sasa tuachie zile hoja tatu kama Kanuni inavyosema zimekwisha tumalize sasa.

| | |
|---|---|
| Kifungu A01 Programu ndogo ya Usimamizi na Usambazaji Huduma za Maji na Nishati | Shs.31,565,238,000 |
| **Jumla ya Kifungu** | **Shs. 31,565,238,000** |
| **Jumla Kuu ya Fungu** | **Shs. 35,949,500,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko.

Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2015/2016 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutukutanisha tena, ili kujadili mambo muhimu ya maendeleo ya nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze ili tuweze kutekeleza kazi hii kwa hekima na busara, na atuwezeshe kufanikisha malengo yetu kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako lipokee, lijadili na hatimaye likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Kwa vile nimepanga kutoa muhtasari wa hotuba kitabu ambacho kimeshagaiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe, kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa wizara yangu kwa mwaka 2015/2016, ninaomba maelezo ya kitabu hicho kuanzia ukurasa wa kwanza hadi ukurasa wa 88 yaingie kwenye *hansard* ya Baraza letu Tukufu.

Mhe. Spika, kwa furaha kubwa naomba kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuiongoza vyema nchi yetu. Uongozi wake uliojaa hekima na busara umesaidia sana kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na katika ustawi wa jamii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua fursa hii pia kumpongeza Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuzipatia ufumbuzi changamoto mbali mbali zinazowakabili wananchi. Aidha, napenda kuwapongeza kwa namna wanavyonipa ushauri na maelekezo katika kuiongoza Wizara yangu.

Mhe. Spika, vile vile, napenda kukupongeza kwa dhati wewe binafsi, kwa umakini wako katika kuliongoza vyema Baraza letu. Pia pongezi hizi ziende kwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza lako kwa namna wanavyokusaidia katika kazi zako.

Pia, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa michango na ushauri wanaonipatia kila ninapowasilisha taarifa za Wizara yangu.

Aidha, napenda kumpongeza kwa namna ya pekee Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari Mheshimiwa Mlinde Mabrouk Juma pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kutusaidia na kutushauri ipasavyo katika kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Mhe. Spika, naomba pia kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Gando kwa mashirikiano mazuri wanayonipa katika kutekeleza utumishi wangu kwao.

**MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2010-2015).**

Mhe. Spika**,** mara baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 iliundwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo iliyopewa dhamana ya kusimamia maendeleo ya Sekta hizo. Madhumuni ya sekta hizo kuwekwa pamoja ni kutokana na maumbile ya kutegemeana katika shughuli zake.

Lengo kuu ni kukuza sekta hizo na kuubeba utalii kwa kutilia manani kwamba Zanzibar ni visiwa vyenye vivutio vingi vya Utalii kama vile fukwe, viumbe mbali mbali vya baharini na ardhini, maeneo ya kihistoria pamoja na urithi wa kimataifa wa Mji Mkongwe.

**SEKTA YA HABARI**

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano (5), Wizara imeweza kufanya mageuzi makubwa katika vyombo vya habari vya umma na vya binafsi kwa kuvipa uhuru na haki ya kuhoji, kutafuta, kupokea na kuchapisha habari pamoja na maoni bila ya woga. Ndani ya kipindi hicho cha miaka mitano redio, televisheni na magazeti yametumika kama vyombo vya kubadilisha mawazo badala ya kutumiwa kama vyombo vya kuwasilisha mawazo.

Jumla ya Redio saba (7) za *FM* na Televisheni nne (4) zimeanzishwa. Radio na televisheni hizo ni Mtegani *FM, Voice of Istiqama FM,* Tumbatu *FM,* Redio Jamii Mkoani *ABM FM,* Marhaba *FM,* Bahari *FM, ZUKU Satellite TV, Star Media TV, Coconut TV* na *Azam TV.*

Mhe. Spika, Mfumo wa ufuatiliaji vipindi *(Monitoring System*) umeanzishwa ambapo hivi sasa vipindi vyote vinarikodiwa, kuhifadhiwa na kufuatiliwa. Mfumo huu unatoa nafasi kwa Serikali kujua na kufuatilia programu za redio zinazorushwa nchini zinafuata kanuni za vyombo vya habari.

Mhe. Spika, mafunzo ya kuwaendeleza wanahabari mbali mbali yametolewa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Jumla ya waandishi 35 wameweza kupatiwa mafunzo katika ngazi tofauti zikiwemo Stashahada, Digrii

na *Master*. Aidha, taaluma mpya ya teknolojia ya dijitali imetolewa kwa mafundi, watayarishaji vipindi na viongozi wa vituo vya utangazaji vya Serikali na Binafsi vilivyopo Zanzibar.

Mhe. Spika, Vyombo vya Habari vya Zanzibar vimeimarishwa sana kwa kuanzisha kisheria Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) kwa kuunganisha Idara ya Televisheni (*TVZ*) na Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar (*STZ*), Kujenga studio mbili za kisasa ya *TV* Unguja na Pemba, kurusha vipindi vya Baraza la Wawakilishi moja kwa moja (*live*) kwa wananchi badala ya kipindi cha masuala na majibu ilivyokuwa mwanzo, kuanza majaribio ya ZBC 2 Televisheni, kuunganisha ZBC kwenye *satellite* na kuiwezesha kuonekana katika nchi zote za Afrika ya Mashariki na Kati, kuanzisha Kampuni ya Maudhui ya matangazo yenye channel 20 zinazoenekana kwenye Shehia zote za Zanzibar, kuanzisha gazeti la pili katika Shirika la Magazeti ya Serikali na kurusha vipindi vya *ZBC TV* na Radio kwa muda wa saa 24 kwa siku badala ya saa 18 hapo awali.

Mhe. Spika, wizara pia imeweza kuimarisha matangazo ya utangazaji kwa kuhamisha mnara wa masafa ya kati (*medium waves*) kutoka Chumbuni kwenda Bungi. Kuhamishwa kwa mnara huo kunarahisisha utuaji wa ndege zinazoingia nchini kwa usalama.

Pia, Ofisi na nyumba mbili (2) za kisasa za wafanyakazi wa familia nne zimejengwa katika eneo hilo la Bungi ili kuimarisha ufanisi. Kazi ya utengenezaji wa mnara wa mawimbi mafupi (*short waves*) nayo imefanyika, inayowezesha *ZBC* Redio kusikika hadi nchi za Mashariki ya Kati.

Mhe. Spika, Chuo cha Uandishi wa Habari kimeimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya kufundishia na kuajiriwa walimu wenye ujuzi. Katika kuimarika kwa chuo hicho, hivi sasa uchukuaji wanafunzi umeongezeka kutoka wanafunzi 75 mwaka 2009/2010 hadi kufikia wanafunzi 180 kwa mwaka 2014/2015. Chuo hicho kimeweza kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuanzisha mafunzo ya lugha ya kichina na kuimarisha ushirikiano wa karibu na Redio ya Kimataifa ya *Deutsche Welle (DW)* ya Ujerumani kupitia taasisi yake ya *(Deutsch Welle Academia)*. Chuo kinamalizia ujenzi wa Chuo chake hapo Kilimani.

## SEKTA YA UTAMADUNI

Mhe. Spika, hatua za kuendeleza harakati za ufufuaji wa maeneo ya kihistoria zimekua zikifanyika ili kutoa mchango mkubwa wa kuongezeka kwa vivutio vya utalii. Mradi wa ufufuaji na uhifadhi wa maeneo ya kihistoria *(Restoration and Conservation of historical Project)* umeanza kutekelezwa.

Mhe. Spika, kumefanyika utafiti wa uchimbaji wa Ngome ya Mazrui, Chwaka, Tumbe kwa ufadhili wa *MACEMP*/DAMA pamoja na utafiti wa kiaikolojia katika eneo la Ngome Kongwe, Forodhani Unguja chini ya Udhamini wa "*African Archaelogy Network*" na DAMA. Katika uchimbaji huo kuligunduliwa vigae vya vyungu, '*Kwale pottery'* vya karne ya kwanza.

Mhe. Spika, aidha, matengenezo yamefanyika kwa jengo la makumbusho la Hamamni Baths ili kulirudisha katika hadhi yake ya awali na kuweza kuenzi historia yetu. Wizara imeweza kuyafanyia matengenezo majengo ya Mangapwani kwenye Mahandaki ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, ujenzi wa ofisi, choo na kuchimba kisima cha maji katika Chemba ya Watumwa Mangapwani pamoja na mnara wa maeneo ya kihistoria ya Kizimbani na Hamamni.

Mhe. Spika, jumla ya *video* za nyimbo na *CD* 12,644 za sanaa mbali mbali zimekaguliwa ili kuhakikisha mila, silka na utamaduni wa Kizanzibari hauathiriwi na tamaduni za kigeni.

Mhe. Spika, Sheria ya Baraza la Sanaa na Sheria ya Bodi ya Sensa zimechanganywa na kufanya sheria moja ya Sanaa na Sensa za Filamu ili kuleta ufanisi mkubwa. Katika kuufanya Utamaduni uwe na tija zaidi, hatua zimechukuliwa kukamilisha mchoro wa ramani ya Utamaduni katika shehia za Unguja na Pemba. Pamoja na Utafiti wa Urithi wa Utamaduni usioshikika katika mikoa mitano ya Zanzibar na hatimaye kuhifadhiwa na kutangazwa Kimataifa kwa kuingizwa katika orodha ya "*UNESCO*" ya tamaduni zinazohifadhiwa.

Mhe. Spika, makamusi matatu ya Lahaja za Kiswahili ambazo ni Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi yametungwa. Aidha Kamusi la Kiswahili sanifu limetungwa.

**SEKTA YA UTALII**

Mhe. Spika, Wizara imeweza kuimarisha shughuli za utalii kwa kufanya marekebisho makubwa ya sheria ya Kamisheni ya Utalii. Mabadiliko hayo ya sheria yameweza kutekeleza kwa kiwango kikubwa Sera ya Utalii na kuanzisha awamu mpya ya uendelezaji wa utalii kwa kusisitiza kauli mbiu mpya ya UTALII KWA WOTE.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha utekelezaji wa dhana ya Utalii kwa Wote, imeanzishwa Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Utalii (*Tourism Development Programme*) ambayo imetokana na matokeo ya Maabara ya Utalii (*Tourism Lab*). Programu hiyo inategemea kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (2014/15 hadi 2017/18).

Mhe. Spika, jumla ya vielelezo vya kuutangaza utalii 60,000 vimetengenezwa, na sasa Kamisheni ya Utalii inashiriki maonesho 7 ukilinganisha na maonesho 5 iliyokuwa ikishiriki mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, Kamisheni imekaribisha waandishi wa habari kutoka Oman, Dubai, China, Misri, Sweden, Uturuki, Malaysia, Marekani, Australia, Ukraine na Uingereza kwa ajili ya kuitangaza Zanzibar nchini mwao. Hivi sasa mashirika ya ndege yanayoleta watalii yamefikia 10 ukilinganisha na mashirika 7 yaliyokuwa yakileta watalii mwaka 2009/2010, na mafanikio ya jitihada hizo yamezaa matunda makubwa ambayo ni kuongezeka idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar kuanzia 2010 hadi 2014. Kutoka watalii 132,836 mwaka 2010 hadi watalii 311,891 mwaka 2014. Hii ni ongezeko la karibu asilimia 240.

Mhe. Spika, katika kuendeleza utalii wa ndani, hatua zimechukuliwa za kushajiisha ziara za wanafunzi kutoka skuli za msingi na sekondari kutembelea maeneo ya kihistoria.

Aidha, wananchi wameshajiishwa kuanzisha Matamasha ya Utamaduni katika maeneo yao. Hadi sasa matamasha tofauti yaliyoanzishwa licha ya kuwepo kwa Tamasha la Mzanzibari, miongoni mwa matamasha hayo ni Matamasha ya Kiislamu na Mangapwani kwa Unguja na Kojani kwa Pemba. Hivi sasa kumekuwa na ongezeko la vikundi vya watu kutoka Mikoa na Wilaya mbali mbali za Tanzania Bara kufanya matembezi ya kuja Zanzibar kama ni sehemu ya Utalii wa ndani kwa uenyeji wa Kamisheni ya Utalii ambapo watalii wa ndani 2014/2015 wamefikia 111,000 ukilinganisha na watalii wa ndani 83,000 kwa mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, katika kuongeza kuwavutia watalii wengi wa hadhi ya juu *(First class tourists*) kuja kutembelea Zanzibar na kuongeza tija katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi, *Kamisheni* ya Utalii kwa kushirikiana na Hoteli ya *Manta Reef* iliyopo Makangale Pemba walizundua Chumba cha chini ya bahari *(Under water room*) ambapo kuzinduliwa kwake kunawavutia watalii wengi wa hadhi ya juu kutembelea Zanzibar na kuongeza pato la nchi.

Mhe. Spika, jitihada za kuainisha idadi ya hoteli zinazofaa kuwekwa madaraja zimechukuliwa. Aidha, wataalamu wawili tayari wamepatiwa mafunzo ya uwekaji wa madaraja hayo. Tayari uhakiki huo umeshafanyika na hoteli 74 zimefikia vigezo vilivyowekwa na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kati ya hizo hoteli za nyota tano ni 16, hoteli za nyota nne ni 9, hoteli za nyota tatu ni 43 na hoteli za nyota mbili ni 6.

Mhe. Spika, Hatua zimechukuliwa katika kuimarisha miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Chuo hicho kimeendelezwa kwa ujenzi wa jengo la ghorofa moja la madarasa na ofisi za Chuo. Aidha, ujenzi wa vibanda vya kusomea na kupumzikia wanafunzi ambapo hivi sasa vinatumika na kuwaletea faraja kubwa wanafunzi umekamilika.

Pia, Chuo kimejenga ukuta kwa ajili ya kukiwekea haiba na kuzuia mifugo pamoja na watu kupita katika maeneo ya Chuo mara kwa mara bila kazi. Aidha, Chuo kimewekewa samani katika jengo jipya.  Katika kutoa taaluma bora ya Utalii, Chuo kilichukua wanafunzi 250 kwa mwaka 2014/2015 ukilinganisha na wanafunzi 147 kwa mwaka 2009/2010.

**SEKTA YA MICHEZO**

Mhe. Spika, mabaraza ya michezo ya Wilaya zote yameimarishwa na kujengewa uwezo kwa kuyapatia mafunzo juu ya namna ya kuendesha na kusimamia shughuli za michezo katika ngazi za Wilaya.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa Zanzibar inaimarisha miundombinu ya tasnia ya michezo, Wizara imeimarisha miundombinu kwa kufanikiwa kuweka nyasi bandia katika uwanja wa Amani Unguja nainamalizia kuweka mpira kukimbilia katika Uwanja wa Gombani Pemba. Ukumbi wa Pemba *Budocan* uliojengwa huko Gombani unatumika vyema kwa michezo ya judo, karati pamoja na michezo mingine ya ndani.

Mhe. Spika, maandalizi tayari yameanza ya kutengeneza uwanja wa *Mao Tse Tung* uliopo mjini Unguja ili uweze kutumika kwa shughuli mbali mbali za michezo. Kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, michorona usanifu wa ujenzi huo inakamilishwa ili kuanza utekelezaji wa mradi huo.

Mhe. Spika, hatua zimechukuliwa za kuendeleza na kuimarisha vipaji vya wanamichezo kwa kuwapatia mafunzo ya utawala na uendeshaji viongozi 20 na walimu 150 wa michezo. Kuendesha semina za mafunzo kwa makatibu na wenyeviti na makocha wa Wilaya.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ya Habari Utamaduni, Utalii na Michezo ilikadiria kupata shilingi 15,366,575,000/=. Kwa kazi za kawaida ni shilingi 9,371,200,000/= na shilingi 400,000,000/= kwa kazi za

maendeleo pamoja na shilingi 5,595,375,000 kwa utekelezaji wa programu ya Maabara ya Utalii.

Aidha, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,671,000,000/= zinazokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 2,421,250,000/= zinazokusanywa na kutumiwa na Taasisi husika.

Mhe. Spika, jumla ya Shilingi 7,029,341,618/= zilipatikana kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 75 na Shilingi 121,754,270/= kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 30 na shilingi 476,745,730 sawa na asilimia 9 kwa kazi za Maabara ya Utalii.

Aidha, Wizara ilikusanya shilingi 1,537,098,269/= sawa na asilimia 92 zilizoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 1,246,437,222/= sawa na asilimia 51 ambazo zimekusanywa na kutumiwa na Taasisi za Wizara. (Tafadhali angalia kiambatanisho nambari 1A)

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2014/2015**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 wizara imefanikiwa kutekeleza miradi ifuatayo:-

i. **Uhifadhi wa Sehemu za Kihistoria na Mambo ya Kale.**

Mhe. Spika, lengo la mradi huu ni kuwa na maeneo ya kihistoria yaliyo endelevu kwa vizazi vya leo na vijavyo kwa maendeleo ya nchi. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na uhifadhi wa mambo ya kale na sehemu za kihistoria, kukusanya na kusambaza taarifa za kiakiolojia katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba na kuweka mabango yenye taarifa katika maeneo ya kihistoria. Mradi huu unategemewa kuingiziwa jumla ya shilingi 150,000,000/= ambapo hadi kufikia Aprili 2015 shilingi 41,754,270/= ziliingizwa sawa na asilimia 28.

Utekelezaji wa Mradi huu unaonekana katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 11.

**UTEKELEZAJI**

Mhe. Spika, kazi zilizofanyika ni utengenezaji wa Makumbusho Unguja Ukuu, ambao umehusisha uwezuaji, upandishaji wa ukuta na uwekaji wa paa jipya katika Kumbusho hilo. Aidha, Wizara imepata fedha kutoka Shirika la "World Monument Fund" katika kusaidia marekebisho ya matengenezo ya jengo la Kihistoria la Mkunazini ili kutekeleza ahadi ya Serikali.

ii. **Programu ya pamoja ya kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Utalii.**

Mhe. Spika, katika jitihada za kuimarisha na kukuza utalii nchini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianzisha Programu ya Maabara ya Utalii ili kuendelea kuchangia pato la nchi na kuinua hali ya uchumi na kijamii sambamba na kuimarisha sekta zote zilizopo nchini. Lengo kuu la programu hii ni kuimarisha utalii wetu na kufikia utalii wa daraja la juu kama inavyoelezwa katika Sera ya Utalii na Mipango Mikuu ya Serikali.

Mhe. Spika, Programu hii imepangiwa kutekeleza shughuli tofauti ambazo zimegawika katika maeneo makuu sita (6) nayo ni: Bidhaa za Utalii na Huduma, kuimarisha harakati za Utangazaji wa Sekta ya Utalii, kuongeza Ulinzi na Usalama kwa watalii na wawekezaji pamoja na mali zao, kuimarisha Miundombinu ya Utalii, kuimarisha Mazingira na faida ya Utalii kwa jamii na kuimarisha Utawala katika Sekta ya Utalii.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 5,595,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha na Kuendeleza Utalii na hadi kufikia Aprili, 2015 wizara ilipatiwa jumla ya shilingi 476,745,730 wa ajili ya utekelezaji wa programu za maabara ambapo fedha hizo ni sawa na asilimia 8.52 ya fedha zilizoidhinishwa. Maelezo zaidi ya Mradi huu yanaonekana katika kitabu cha pili.

Mhe. Spika, Programu hii ya Maabara ya Utalii imejumuisha miradi midogo midogo 35 ambayo inatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu, 2015/2017. Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 miradi 17 ambayo imejumuisha shughuli mbali mbali imefanikiwa kutekelezwa. Utekelezaji halisi wa shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka wa fedha wa 2014/ 2015 kiwizara unapatikana katika kitabu cha pili.

## MAENEO YA VIPAUMBELE VYA KISEKTA KWA MWAKA 2015/2016

Mhe. Spika, wizara imeweza kujipangia maeneo muhimu ya utekelezaji kisekta na kuwa ni vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Vipaumbele hivyo ni kama vinavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 13 na 15.

## SEKTA YA HABARI

Mhe. Spika, mambo muhimu ambayo imejipangia katika Sekta ya Habari kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama yafuatayo:-

i. Kuendelea kufunga vifaa vya kisasa katika studio za kurikodia vipindi vyenye kutumia mfumo wa dijitali.

ii. Kuanzisha mitandao ya kijamii kwa ajili ya wananchi kupata habari kwa urahisi popote walipo kupitia simu na intaneti.
iii. Kutoa taaluma ya kutumia vifaa vya Teknolojia ya Utangazaji wa dijitali.
iv. Ujenzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasilano ya Umma.
v. Kuwapatia wananchi huduma bora za habari na kwa wakati kwa njia ya magazeti, redio na televisheni.

## SEKTA YA UTAMADUNI

Mhe. Spika, maeneo muhimu ambayo tumeyawekea kipaumbele katika Sekta ya Utamaduni kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama yafuatayo:-

i. Kuhifadhi na kuimarisha maeneo ya kihistoria pamoja na kuyatangaza ndani na nje ya nchi.
ii. Kutangaza na kuendeleza Lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na usahihi wake ndani na nje ya Zanzibar.
iii. Kukuza kazi za sanaa pamoja na kuendeleza matamasha na maonesho ya filamu na muziki.
iv. Kufunga vifaa vya kisasa katika Studio ya kurikodia muziki na filamu.

## SEKTA YA UTALII

Mhe. Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika sekta ya Utalii mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama yafuatayo:-

i. Kutangaza Utalii kwa kutumia teknolojia ya kisasa ikiwemu mitandao.
ii. Kuaanda utafiti utakaowezesha kufahamu nafasi ya Zanzibar katika masoko yake ya sasa na yale yanayochipukia.
iii. Kukijengea uwezo wa kitaalamu na kitaaluma Chuo cha Maendeleo ya Utalii (*ZIToD*) ili kutoa rasilimali watu kulingana na mahitaji ya soko la utalii.
iv. Kuimarisha miundombinu ya Hoteli ya Bwawani ili kuvutia wageni wengi.

## SEKTA YA MICHEZO

Mhe. Spika, maeneo muhimu yaliyopewa kipaumbele katika Sekta ya Michezo mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama yafuatayo:-

i. Matengenezo na ujenzi wa viwanja vya michezo vya Uwanja wa Amaan, Gombani na kiwanja cha Mao Tse Tung.

ii. Kuviimarisha vilabu vya michezo kwa kuvipatia mafunzo, vifaa vya michezo na fursa za michezo ya majaribio ili kuviwezesha kushindana katika mashindano ya kimataifa.
iii. Kuwezesha vilabu kuandaa na kushiriki mashindano ya ndani na nje.

**MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imetengewa jumla ya shilingi 13,052,200,000/=. Kati ya fedha hizo shilingi 10,072,200,000/= kwa matumizi ya kawaida, shilingi 480,000,000/= kwa miradi ya maendeleo na shilingi 2,500,000,000/= Kwa Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Utalii (*Tourism Development Program*). (Tafadhali angalia Kiambatisho namba 1E)

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

Mhe. Spika, malengo tuliyotekeleza kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa kila Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

**IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI**

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi ni kusimamia shughuli zote za utawala, utumishi (rasilimali watu), maendeleo, wajibu na maslahi ya wafanyakazi wa wizara. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, idara ilipanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 16.

i. Kuwa na mazingira bora ya kazi kwa kuipatia Wizara vitendea kazi vyenye ubora vitakavyowezesha Wizara kufanya kazi kwa ufanisi.
ii. Kuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi wenye ujuzi na utaalamu kwa kuwapatia wafanyakazi nafasi za masomo ndani na nje ya nchi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Wizara.
iii. Kuwa na mashirikiano mazuri na endelevu ya Uendeshaji na Utawala kwa kutembelea Taasisi zilizo chini ya Wizara, kushiriki katika semina na mikutano ya kitaifa na kimataifa.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo yake ya mwaka wa fedha 2014/15 kama ifuatavyo.

i. Katika kujenga mazingira bora ya kazi Idara imesimamia na kuimarisha upatikanaji wa huduma mbali mbali za Ofisi ikiwemo ununuzi wa samani za Ofisi, kompyuta za mezani (*desk top*) mbili na laptop tatu kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ili kurahisisha utendaji wa kazi zake za kila siku. Aidha, vifaa vya kuandikia kwa ajili ya matumizi ya Ofisi vimepatikana. Vile vile Idara imegharamia upatikanaji wa vifaa vya mawasiliano ya internet, fax na simu za ndani za Ofisini, ulipaji gharama za maji, umeme, ununuzi wa mafuta na vilainishaji pamoja na matengenezo madogo madogo ya gari na kulipia posho za kukaimu, malipo ya wafanyakazi baada ya saa za kazi na stahiki zao nyengine.

ii. Katika kuwaongezea wafanyakazi ujuzi, utaalamu na maarifa, Idara imegharamia masomo kwa wafanyakazi 14, wanawake (8) na wanaume (6) kati ya hao wafanyakazi watatu (3) ni wa Shahada ya Pili (*Master*), watano (5) Shahada ya Kwanza, na wanne (5) Stashahada (*Diploma*) na mmoja Cheti. Lengo ni kuwaongezea ujuzi, maarifa na ubunifu ambao utapelekea kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Mafunzo pia yametolewa kwa watendaji wa taasisi nyengine zilizomo katika Wizara. (Tafadhali angalia kiambatisho namba 2).

iii. Katika kujenga mashirikiano ya uendeshaji na utawala, Idara imefanya malipo ya safari kwa viongozi wa Wizara katika kufuatilia shughuli za utendaji ziliopo Pemba na Dar es Salaam. Vile vile, Idara imewagharamia watendaji wa Wizara kushiriki katika mkutano wa kimataifa nchini India, Ujerumani na Omani.

iv. Idara imendelea na hatua ya pili ya ujazaji wa taarifa za wafanyakazi "*Database*" ya Wizara inayotumia mfumo wa kielektroniki ambayo itakuwa na taarifa zote zinazomhusu mfanyakazi.

v. Pia, Idara imewezesha Zanzibar kushiriki katika mashindano ya *NSSF* yaliyofanyika Dar es salaam yaliyozishirikisha timu za vyombo vya habari vya Tanzania, ambapo timu ya mpira wa miguu kwa wanaume ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imepata ushindi wa kwanza na kuchukua kombe katika mashindano hayo ya mwaka 2015.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015. Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,437,446,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 945,228,142/= sawa na asilimia 66. Na kwa rasilimali hizi zilizopatikana imefanikiwa kutekeleza malengo yake ya mwaka wa fedha 2014/2015 kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 17 na 18.

## IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kupanga, kutayarisha, kukagua, kuratibu na kutathmini mipango ya maendeleo ya wizara, kupitia sera, kufanya tafiti mbali mbali na kusimamia utekelezaji wake. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 19.

i. Kuwa na Mipango bora ya kisekta na Sera kwa kutayarisha na kuzipitia Sera za Wizara.
ii. Kuwa na "*database*" ya takwimu sahihi ya taarifa zinazokusanywa na Wizara.
iii. Kuwa na wafanyakazi wenye ujuzi na utaalamu katika fani ya Takwimu, Teknolojia ya Habari na Mipango.

## UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Idara hii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Imefanya mapitio ya Sera ya Michezo ya 2007 kwa kuwashirikisha washirika wa michezo Unguja na Pemba pamoja na kuingiza michango na mawazo ya washirika hao kwa lengo la kupata Sera itakayoweza kukidhi mahitaji ya michezo. Rasimu ya Sera hiyo ya 2015 ipo katika hatua za mwisho za uchapishaji na kuratibu matayarisho ya Sera ya Urithi wa Utamaduni ya 2015.
ii. Idara imeandaa taarifa za utekekelezaji kwa malengo ya Wizara pamoja na Miradi ya Maendeleo na kuwasilisha katika vikao vya Mhe, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ikulu.
*iii.* Kufuatilia utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara katika maeneo ya kihistoria ili kuona maendeleo ya miradi hiyo. Pia Idara imefanikiwa kutoa mafunzo kwa watendaji wa Wizara kuhusu utaratibu mpya wa kutayarisha bajeti kwa muundo wa programu *"Program Based Budget – PBB".*
iv. Kuzipitia taarifa za utafiti na uchambuzi wa kuangalia kuwa Zanzibar tuna rasilimali ambazo hatujazitumia ambazo ni muhimu kwa kuwavutia watalii nchini kwetu.
v. Idara imegharamia mafunzo wafanyakazi wake watatu (3) katika fani tofauti, mmoja (1) Shahada ya Kwanza katika fani ya Takwimu, na wawili (2) Shahada ya Pili katika fani za Maendeleo ya Uchumi na Teknohama.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 82,949,000/= kwa Matumizi Mengineyo na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 42,798,064/= sawa na asilimia 52 na idara hii imetekeleza shughuli zake kama zinavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 19 na 20.

**OFISI KUU PEMBA**

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Pemba ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara Kisiwani Pemba. Ofisi hii ni kiunganishi katika kuhakikisha majukumu, malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa upande wa Pemba. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, ofisi hii ilipanga kutekeleza malengo yake kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 21.

i. Kuwa na mipango bora ya kisekta na sera kwa kutayarisha na kupitia sera za wizara, kuwa na "*database*" ya takwimu sahihi ya taarifa zinazokusanywa na wizara.
ii. Kuwa na wafanyakazi wenye ujuzi na utaalamu kwa kuwapatia wafanyakazi nafasi za masomo ndani na nje ya nchi.
iii. Kuwa na masirikiano mazuri na taasisi za Wizara Pemba kwa kutoa na kujenga mazingira bora yatakayowezesha Ofisi Kuu Pemba kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, Ofisi Kuu imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

i. Ofisi Kuu imeratibu Tamasha la Utamaduni na Michezo lililofanyika Kojani ambalo lilishirikisha vikundi vya ngoma za utamaduni na Mpira wa miguu kati ya timu ya Jamhuri na Shaba ya Kojani.
ii. Ofisi Kuu imeratibu ujenzi wa Jengo la michezo ya ndani (*Multi in door game*) litakalotumiwa na wanamichezo wa fani tofauti wa Wilaya nne za Pemba. Jengo hilo ni ufadhili wa Serikali ya Japani kupitia balozi wao aliyepo Tanzania.
iii. Wafanyakazi watano (5) wamepatiwa mafunzo muda mrefu (1) Stashahada ya Manunuzi, (1) Stashahada ya *IT* na (1) Cheti fani ya Uwekaji Kumbukumbu (1) Shahada ya Uzamili ya Utawala na (1) Stashahada ya Rasilimaliwatu.
iv. Kusimamia kazi ya kuweka mpira wa kukimbilia (*Tartan*) katika uwanja wa Gombani.
v. Kuwapatia wafanyakazi stahiki zao za likizo, malipo ya baada ya saa kazi na posho la kukaimu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015. Ofisi Kuu Pemba iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,344,313,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 1,214,143,650/= sawa na asilimia 90. Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 21 na 22.

**SEKTA YA HABARI**

Mhe. Spika, Sekta ya Habari imeundwa na taasisi tano ambazo ni Shirika la Utangazaji Zanzibar, Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali, Tume ya Utangazaji, Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (*ZMUX*) na Chuo cha Uandishi wa Habari. Majukumu ya msingi ya taasisi hizi ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha jamii, kuratibu uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi na kutoa taaluma kwa waandishi wa habari.

**SHIRIKA LA UTANGAZAJI (*ZBC*)**

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Shirika ni kutoa habari, kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Shirika hili lilijipangia kutekeleza malengo yake kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 23.

i. Kuhakikisha *ZBC* inatoa habari na vipindi vyenye ubora kwa jamii, kwa kuendelea kuweka vifaa vya kisasa vitakavyoweza kuandaa vipindi na kukusanya habari zenye viwango.
ii. Kuwa na mazingira bora ya kazi ili kuliwezesha Shirika kutoa huduma bora na zenye ufanisi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, Shirika la Utangazaji limefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Shirika limesimamia shughuli zake za kila siku za uendeshaji kwa ajili ya uandaaji vipindi mbali mbali vinavyorushwa na Shirika hilo kwa lengo la kuelimisha jamii. Pia ununuzi wa vifaa vya dijitali vya studio umefanyika.
ii. Shirika limenunua gari mbili (2) kwa lengo la kufuatilia kazi zake za kila siku ambazo hurahisisha katika urushaji wake wa vipindi kwa wananchi.

iii. Shirika limewalipa wafanyakazi wasioajiriwa (*Freelance*), kutoa malipo ya likizo na muda wa ziada kwa wafanyakazi ili kuongeza hamasa na ari ya kufanya kazi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Shirika la Utangazaji liliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,739,536,000 /= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 1,348,709,552/= sawa na asilimia 78. Shirika lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 300,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 277,415,538/= sawa na asilimia 92. Na kwa upatikanaji huo wa rasilimali Shirika la Utangazaji limefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 23.

**IDARA YA HABARI MAELEZO**

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Idara ya Habari Maelezo ni kutoa elimu kwa maendeleo mijini na vijijini, kuimarisha uhusiano mzuri kati ya serikali na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi, kutayarisha na kutoa vielelezo katika mfumo wa picha, sinema na majarida kuhusu shughuli za serikali na kusimamia Sheria ya Habari Zanzibar.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo makuu kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 24.

i. Kuhakikisha wananchi wanapata taarifa muhimu kupitia njia za habari na mawasiliano
ii. Kuweka mazingira bora ya kazi yatakayo wezesha Idara kufanya kazi kwa ufanisi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

i. Idara imefanikiwa kukusanya na kusambaza taarifa 600 za kijamii, kiuchumi na kisiasa katika Vyombo vya Habari na "*Blogs*" pamoja na uchapishaji wa vitambulisho 114 vya Waandishi wa Habari kwa lengo la kutoa taarifa kwa wananchi.
ii. Idara imetoa machapisho 3,200 ya Baraza la Mawaziri, pamoja na usafishaji wa picha za matukio mbali mbali na kuweka katika "display boards" kwa lengo la wananchi kuweza kufahamu kinachoendelea katika nchi yao.

iii. Idara imefanikiwa kufanya mkutano mmoja kwa lengo la kupitia maombi ya usajili wa magazeti, wafanyakazi wanne (4) wamepatiwa stahiki zao za likizo na wafanyakazi wanane (8) wamepata stahiki zao za muda wa ziada. Aidha, katika kuweka mazingira bora ya Ofisi, Idara imenunua vifaa vya usafi, matengenezo ya gari, ununuzi wa vipaza sauti, vifaa vya kuandikia, huduma ya umeme na mafuta na wafanyakazi watatu (3) wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya Stashahada ya Uhasibu, Kutunza Kumbumbu na Habari.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 338,807,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 198,358,529/= sawa na asilimia 59. Idara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 19,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 7,255,500/= sawa na asilimia 38. Na kwa rasilimali hizo zilizopatikana idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 24 na 25.

## SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Shirika la Magazeti ya Serikali ni kusimamia uchapishaji wa magazeti ya Serikali Zanzibar, kuelimisha wananchi ili kukuza uelewa wao wa mambo, kutoa habari zenye kuhamasisha jamii na kushiriki kwenye harakati za maendeleo ya nchi.  Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Shirika la Magazeti ya Serikali lilipanga kutekeleza malengo yake kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 26.

i. Kuwa na magazeti yenye makala na habari za kielimu ambazo zinalenga kuondosha umasikini nchini na kuishajiisha jamii kushiriki katika mipango ya maendeleo ya nchi kwa kuchapisha na kusambaza magazeti ya kila siku na kila wiki.
ii. Kuwa na miundombinu bora ya ofisi na vitendea kazi na kuwaongezea ujuzi na uwezo wafanyakazi wa Shirika.

## UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako kuwa, Shirika limeweza kutekeleza kwa kiasi kikubwa shughuli zake kwa mwaka 2014/2015 kama ifuatavyo:-

i. Shirika limefanikiwa kuchapisha Magazeti kwa wingi na kuyasambaza katika mikoa tofauti ya Zanzibar na Tanzania Bara. Jumla ya nakala 546,000 kwa gazeti la kila siku (Zanzibar Leo) na nakala 72,000 kwa gazeti la wiki (Zaspoti) zimechapishwa. Aidha, Shirika limefanikiwa

kuanzisha tovuti yake (*website*) kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa habari kwa jamii na kuwafikia wananchi wengi kwa muda mfupi, pamoja na kuandaa mafunzo ya wafanyakazi wote kuhusiana na mabadiliko ya kiutendaji kazi.

ii. Shirika la Magazeti ya Serikali limendelea kuwalipia ada ya masomo wafanyakazi wake katika fani tofauti, mmoja (1) Shahada ya Pili ya Uhasibu na mmoja (1) Shahada ya Kwanza ya Uhandisi, mmoja (1) Shahada ya Kwanza ya Uandishi wa Habari na mwengine kumlipia gharama ya mafunzo ya Udereva katika Chuo cha Taifa cha Usafiri (*National Insitute of Transport*).

iii. Aidha, Shirika limefanya mafunzo ya upigaji picha bora kwa ufadhili wa "Tanzania *Media Fund*" (*TMF*) kwa lengo la kupata wafanyakazi wenye uwezo mkubwa.

iv. Katika kuweka mazingira bora ya Ofisi, Shirika limewalipa wafanyakazi stahiki zao za likizo, muda wa ziada na waandishi waliojitegemea walioko Unguja, Pemba na Mikoa kadhaa ya Tanzania Bara na kulipatia Shirika vifaa vya kutendea kazi kama laptop, desktop, camera ya dijitali, simu na kufanya malipo ya huduma za *TRA*, intaneti, umeme na mafuta ya petrol na dizeli.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015. Shirika liliidhinishiwa jumla ya shilingi 587,726,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 limefanikiwa kupata shilingi 468,461,900/= sawa na asilimia 80. Shirika lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 500,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 268,864,325/= sawa na asilimia 54. Na shirika limeweza kutekeleza kwa kiasi kikubwa shughuli zake kwa mwaka huu kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 26 na 27.

**TUME YA UTANGAZAJI**

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Tume ya Utangazaji ni kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi vinavyoanzishwa nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Tume ya Utangazaji ilipanga kutekeleza malengo yake kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 28.

i. Kuwa sekta ya utangazaji iliyoimarika inayokwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya kisasa.

ii. Kuwa na mazingira bora ya kazi yatakayoiwezesha Tume kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa kuipatia huduma, vifaa na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

## UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Utangazaji imeweza kufanya mambo yafuatayo:

i. Katika kuhakikisha redio zilizopo nchini hazikiuki maadili ya utangazaji, Tume imeweka mfumo maalumu (*Monitoring System*) wa kudhibiti hali hiyo na kufanya utafiti wa wasikilizaji kwa lengo la kupata maoni ya wananchi juu ya shughuli za utangazaji zinavyowafikia. Aidha, Tume kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji la Ujerumani (*DW*) imetoa mafunzo kwa taasisi za utangazaji kwa lengo la kujadili changamato na mafanikio ya Sekta ya Habari Zanzibar.

ii. Aidha, Tume ya Utangazaji kwa kushirikiana na *TCRA* imeandaa mkutano wa siku moja wa Sekta ya Utangazaji kuhusu kanuni za utangazaji wakati wa uchaguzi. Pia, Tume Imesimamia miongozo katika kuhakikisha redio zinafuata sheria na kanuni za utangazaji na kununua "*Software*" kwa ajili ya kurikodia vipindi vya redio vinavyorushwa nchini.

iii. Tume ya Utangazaji imenunua gari moja kwa lengo la kuimarisha ufuatiliaji wa shughuli zake za kila siku. Pia, Tume imefanya manunuzi ya vitendea kazi vya Ofisi vikiwemo Vifaa vya kuandikia na vifaa vya usafi kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya Ofisi.

iv. Aidha, Tume imeendelea kuwapatia stahiki zao za likizo na muda wa ziada wafanyakazi kwa lengo la kuongeza hamasa ya kazi. Vile vile Tume imefanya safari za kikazi ya ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Tume iliidhinishiwa jumla ya shilingi 196,499,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 176,349,399/= sawa na asilimia 90. Tume imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 52,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 30,248,894/= sawa na asilimia 58. Kwa rasilimali hizo Tume ya Utangazaji imeweza kufanya shughuli zake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 28 na 29.

## KAMPUNI YA UUNGANISHAJI MAUDHUI (*ZMUX*)

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Kampuni ya Uunganishaji Maudhui ilipanga kutekeleza majukumu yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 29.

i. Kupitisha matangazo ya televisheni na redio kwenye miundombinu yake inayotumia mfumo wa dijitali.

ii. Kuwa na mazingira bora ya kazi ili kuiwezesha Kampuni kutoa huduma bora na zenye ufanisi.

## UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kampuni ya *ZMUX* imetekeleza shughuli zufuatazo:-

i. Kampuni imeweka chaneli ya mpira (*canal*+) ambapo hivi sasa watumiaji wa king'amuzi cha *ZMUX* wanapata fursa ya kutazama ligi mbali mbali za Ulaya.
ii. Katika kukabiliana na kukatika kwa matangazo kwa Pemba, tatizo hilo limepungua kwa kufanyiwa marekebisho ya kifaa kinachoitwa "*microwave*".
iii. Ili kuwa na mazingira bora ya kazi na kuiwezesha Kampuni kutoa huduma bora na zenye ufanisi, Kampuni imenunua kifaa cha *AVR* katika kituo cha Pemba baada ya cha awali kuungua, vifaa vya kuandikia, malipo ya umeme kwa vituo vyake kwa Unguja na Pemba pamoja na ununuzi wa mafuta kwa ajili ya majenereta.

Mhe. Spika, Kampuni ya Uunganishaji Maudhui kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 140,000,000/= na imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 72,272,000/= sawa na asilimia 51 hadi kufikia Aprili, 2015. Na kwa utekelezaji huo Kampuni ya *ZMUX* imetekeleza shughuli zake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 30.

## CHUO CHA UANDISHI WA HABARI

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Chuo cha Uandishi wa Habari ni kutoa mafunzo ya taaluma ya uandishi wa habari na mawasiliano kwa ngazi ya Cheti na Diploma kwa kuzingatia matakwa ya soko la ajira sambamba na kufanya tafiti mbali mbali na kutoa ushauri unaotokana na matokeo ya tafiti hizo kwenye tasnia hiyo. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Chuo cha Uandishi wa Habari kilipanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 31.

i. Kuimarisha kiwango cha raslimali watu katika taaluma ya habari na mawasiliano kwa kuimarisha Mtaala wa kufundishia na mafunzo kwa ajili ya kuongeza uwezo wa utoaji habari.
ii. Kuwa na mazingira mazuri ya kazi na kujifunza na kusimamia tafiti za wanafunzi, kutoa ushauri elekezi pamoja na kuandaa na kushiriki mijadala ya kimafunzo.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Chuo cha Uandishi wa Habari kimefanya shughuli zifuatazo:-

i. Chuo kimeandaa ripoti ya kitaalamu kuhusu mahitaji ya kimafunzo ili kuongeza utaalamu unaokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje. Aidha, Chuo kimechambua maombi ya udahili wa wanafunzi wapya na kutoa udahili kwa jumla ya wanafunzi wapya 100 ambapo kati ya hao 45 ngazi ya Cheti na 55 *Diploma*.
ii. Jumla ya wanafunzi 128 wamehitimu kwa mwaka 2014/2015, kati ya hao Diploma 53,Cheti 48 na Msingi 27.
iii. Katika kukuza taaluma za watendaji wake, Chuo kimewalipia ada wafanyakazi wake waliopo masomoni katika ngazi ya Shahada ya Pili na kulipa stahiki za likizo na muda wa ziada kwa wafanyakazi wake kwa lengo la kuimarisha utendaji.
iv. Chuo kimefanya mapitio na mabadiliko ya sheria ya Chuo ili kukifanya kilingane na mahitaji ya sasa na baadae
v. Chuo kimeandaa makongamano mawili ya kitaaluma yalioainisha changamoto na mahitaji ya jamii katika tasnia ya habari na mawasiliano. Pia Chuo kimefanya ziara za kiutendaji Dar es Salaam kwa ajili ya kuimarisha mashirikiano ya kitaaluma na taasisi ziliopo huko.
vi. Katika kuhakikisha wanafunzi wanapata mafunzo ya vitendo (*practical*) Chuo kimenunua kamera tano za digitali kwa lengo la kupata wanafunzi wenye ujuzi wa kutumia vifaa hivyo katika sehemu zao za kazi. Pia Chuo kimefanya malipo ya huduma za internet**,** umeme**,** maji, simu, magazeti na matangazo kwa ajili ya kurahisisha huduma za mawasiliano.
vii. Katika kuweka mazingira bora ya Ofisi, Chuo kimewalipia fedha za kujikimu walimu wawili (2) walioko masomoni, ngazi ya *PhD* mmoja nchini Uturuki na mmoja (1) nchini China. Aidha, kimewalipia ada wafanyakazi watatu (3), Diploma mmoja (1) na ngazi ya *Master* wawili (2).
viii. Chuo kimewapatia fedha za likizo wafanyakazi 9, kuwapatia stahiki walimu na wafanyakazi na kulipia walinzi. Pia Chuo kimezipatia Ofisi zake huduma za internet, maji, umeme, magazeti, simu, matangazo na ada ya benki.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015. Chuo kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 237,810,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 229,138,251/= sawa na asilimia 96. Chuo kilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 126,250,000/= na hadi kufikia Aprili, 2015 shilingi 93,451,300/= zimekusanywa sawa na asilimia 74. Na Chuo cha Uandishi wa

Habari imefanya shughuli zake kama zinavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 31 hadi 33.

**SEKTA YA UTALII**

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii inajumuisha Kamisheni ya Utalii, Chuo cha Maendeleo ya Utalii na Hoteli ya Bwawani. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kupanga mikakati, kusimamia, kuendeleza Utalii na kuitangaza Zanzibar ili Sekta hii iende sambamba na Sera na Mikakati ya Serikali katika kufikia malengo makuu ya kuimarisha uchumi wa Taifa na kupunguza umasikini.

**KAMISHENI YA UTALII**

Mhe. Spika, jukumu la msingi la Kamisheni ya Utalii Zanzibar ni kupanga mikakati, kuratibu, kusimamia, kuendeleza na kutangaza shughuli za utalii ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha wa 20142015, Kamisheni imepanga kutekeleza malengo kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 34.

i. Zanzibar kuwa kituo bora cha utalii katika ukanda wa Bahari ya Hindi.
ii. Kutekeleza dhana ya utalii kwa wote ili uwe na tija zaidi kwa wananchi.
iii. Kujenga mazingira bora ya kazi yatakayoiwezesha Kamisheni ya Utalii kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Kamisheni ya Utalii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Katika kuutangaza Utalii kitaifa na kimataifa, Kamisheni imechapisha kalenda (5000), *DVD* (5,000) na majarida (8000) ili iwe rahisi kwa watalii wengi kupata taswira ya Zanzibar na vivutio vyake. Aidha, Kamisheni imefanya utafiti wa vivutio vipya vya Utalii kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini.
ii. Kamisheni imeanzisha kituo cha utangazaji Utalii nchini India (*Zanzibar Tourism Promotion Centre*), kwa kutumia kampuni ya uwakala inayojulikana kwa jina la *JHIL EXTERPRISES* (India), kwa lengo la kuongeza wigo wa masoko pamoja na ukuaji wa idadi ya watalii kutoka Asia.
iii. Kwa lengo la kuitangaza Zanzibar katika maonesho ya utalii ya kimataifa na kitaifa Kamisheni imeshiriki katika maonesho ya *WTM – London, CTTM – China*, *ITB* Ujerumani na *INDABA* Afrika ya Kusini. Aidha, Kamisheni imeshiriki katika maonesho ya Mswahili (*Swahili Expo*) yaliyofanyika Dar es Salaam.

iv. Katika kuhakikisha ubora wa Hoteli zinazofanya kazi Zanzibar Kamisheni imekagua miradi ya kiutalii zikiwemo Hoteli kwa lengo la kuhakiki ubora wa huduma zinazotolewa nchini kwa wawekezaji wa Sekta ya Utalii. Aidha, Kamisheni imewasilisha kanuni ya Utalii katika Kamati ya Uongozi ya Wizara ili kupata michango. Hatua inayoendelea hivi sasa ni kuingiza marekebisho yaliyopendekezwa na vikao hivyo kabla ya kuipeleka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua za kuichapisha.

v. Katika kukuza dhana ya utalii kwa wote, Kamisheni imeadhimisha Siku ya Utalii Duniani katika maeneo ya Nungwi kwa upande wa Unguja na Micheweni Pemba. Aidha, Kamisheni imerusha hewani jumla ya vipindi 36 kupitia *ZBC Redio* na *ZBC TV* kwa lengo la kutoa elimu na kuwashajiisha wananchi umuhimu wa Sekta ya Utalii na jinsi ya kutumia fursa zilizopo kwa maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

vi. Kutoa mafunzo ya utalii kwa wanafunzi wa Skuli ya Umbuji katika Wilaya ya Kati Unguja. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uelewa kwa vijana ili waweze kutumia fursa za utalii zilizopo pamoja na kujenga tabia ya kutembelea vivutio vya utalii.

vii. Kamisheni imefanya vikao vya Makamishna kama ilivyo katika sheria kwa nia ya kujadili mafanikio na changamoto ya Sekta ya Utali.

viii. Katika kuweka mazingira bora ya Ofisi, Kamisheni imefanya matengenezo madogo ya Ofisi Kuu iliyopo Amaan na Ofisi ya mauzo iliyopo katika Hoteli ya Bwawani. Aidha, Kamisheni imelipia huduma za Ofisi kama umeme, maji, posta, simu pamoja na ununuzi wa vifaa vya kuandikia na petroli na dizeli kwa ajili ya kusimamia shughuli za utalii nchini.

ix. Kamisheni imewagharamia masomo wafanyakazi wake nane (8) katika fani na kozi tofauti, Stashahada ya Habari na Mawasiliano wawili (2), Shahada ya Kwanza ya Uongozi wa Utalii wawili (2), Usimamizi wa Biashara na Uhasibu wawili (2), Shahada ya Pili ya Usimamizi wa Biashara mmoja (1), Ugavi na Manunuzi mmoja (1) na mafunzo ya muda mfupi nchini Ujerumani. Aidha wafanyakazi wamepatiwa stahiki zao kwa lengo la kudumisha na kuongeza ufanisi wa kazi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kamisheni iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,389,200,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 250,000,000/= kwa kazi za maendeleo na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 935,832,863/= sawa na asilimia 67 kwa kazi za kawaida na shilingi 80,000,000/= sawa na asilimia 32 kwa kazi za maendeleo.

Aidha, ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,340,000,000/= katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kufanikiwa kukusanya shilingi 1,427,291,516/= sawa na

asilimia 107. Katika rasilimali hizo Kamisheni ya Utalii imetekeleza shughuli zake kama zinavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 34 hadi 36.

**CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII ZANZIBAR**

Mhe. Spika, jukumu la msingi la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar ni kutoa taaluma itakayowezesha kujenga rasilimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya kimataifa ili kuimarisha Sekta ya Utalii Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kilipanga kutekeleza malengo yake kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 37.

i. Kuendeleza upatikanaji wa rasilimali watu watakaoweza kutoa huduma bora zenye viwango katika shughuli za utalii.
ii. Kuandaa mazingira bora ya kazi, ufundishaji na usomaji kwa kuimarisha shughuli za taaluma pamoja na kuwajengea uwezo wakufunzi na wafanyakazi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimeweza kutekeleza yafuatayo:-

i. Katika kuongeza rasilimali watu watakaotoa huduma bora zenye viwango katika shughuli za utalii, Chuo kimefanikiwa kudahili wanafunzi wapya 244 wakiwemo Stashada 82 na Cheti 162, kati ya hao wanaume 137 na wanawake 107. Aidha, Chuo kimeimarisha shughuli za taaluma ikiwemo mitihani, kuongeza vipindi vya mafunzo ya vitendo (*practical session*) pamoja na kuchapisha vyeti vya wahitimu 182 na kutunuku Vyeti na Stashahada kwa wahitimu 182, wanaume 125 wanawake 57.
ii. Kutoa mwamko wa utalii kwa wote kwa wanafunzi wa Skuli nane (8) za Sekondari Unguja na Pemba kwa kuoneshwa shughuli zinazofanywa na Chuo cha Maendeleo ya Utalii kwa lengo la kuwashajiisha kujiunga na Chuo.
iii. Chuo kimefanya utafiti mdogo wa kukusanya taarifa za uchambuzi kwa hali halisi (*situation analysis*) kwa kuangalia uwezekano wa kufungua Chuo kingine cha Utalii kisiwani Pemba.
iv. Katika kuweka uhusiano wa karibu na wawekezaji wa Mahoteli, Chuo kimefanya mikutano miwili na Hoteli za Kitalii na Taasisi nyengine zinazotoa huduma za kitalii.
v. Chuo kimeendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watano (5) wakiwemo mmoja (1) ngazi ya Shahada ya Kwanza fani ya

Utalii na Usafiri, mmoja (1) ngazi ya Stashahada fani ya Uongozi wa shughuli za Utalii na Ukarimu, mmoja (1) ngazi ya Stashahada fani ya Mapishi (*Culinary Arts*), mmoja (1) ngazi ya Cheti fani Utunzaji Kumbukumbu na mmoja (1) ngazi ya Shahada Pili ya fani ya Uongozi wa Fedha katika vyuo tofauti.

vi. Kuzipatia ofisi vitendea kazi kwa mujibu wa mahitaji, kugharamia huduma za uendeshaji na kuimarisha usalama katika eneo la Chuo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 414,029,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 289,129,001/= sawa na asilimia 70. Chuo kilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 360,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 297,348,014/= sawa na asilimia 83. Na kwa rasilimali hizo zilizopatikana Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimeweza kutekeleza shughuli zake kama zinavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 38 hadi 39.

## HOTELI YA BWAWANI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Hoteli ya Bwawani ilipanga kutekeleza malengo yake kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 39.

i. Kuwa na idadi kubwa ya wageni wa daraja la juu katika Hoteli ya Bwawani.
ii. Kuwa na mazingira bora ya kazi kwa kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana kwa uhakika.

## UTEKELEZAJI HALISI

i. Ili kuhakikisha Hoteli ya Bwawani inapokea idadi kubwa ya wageni wa daraja la juu Hoteli imefanya matengenezo ya ukumbi wa mkutano wa "*roof top*", vyumba, ubadilishaji wa vyoo na uwekaji wa dawa katika Hoteli. Pia Hoteli imeendelea kufanya malipo kwa mawakala wanaoleta wageni.
ii. Katika kutoa huduma bora za ukarimu kwa wageni wanaofika hapo, hoteli imefanya manunuzi ya bidhaa za vyakula na vinywaji ili kutosheleza mahitaji ya wageni.
iii. Huduma za upatikanaji wa maji katika maeneo ya hoteli zimeimarishwa kwa kufunga mashine tatu (3) za kusukumia maji, kuimarisha miundombinu ya umeme pamoja na kufanyia matengenezo mashine za kufulia, kupigia pasi na kuimarisha huduma za jikoni pamoja na manunuzi ya vitendea kazi vifaa vya Ofisi na kufanyia usafi kwa ajili ya Hoteli.

iv. Katika kuhakikisha Hoteli ina watendaji wenye uwezo na ujuzi wa hali ya juu, Hoteli imeendelea kuwalipia masomo watendaji wake (14), Stashahada wanne (4) fani ya Hotel Management & Hospitality, Cheti 9 fani ya House Keeping (3), *Food Preparation & Beverage* (5) na *Front Office Operation* (1) pamoja na Shahada ya Kwanza mmoja fani ya Sheria. Aidha Hoteli imewalipa wafanyakazi wake stahiki zao za likizo na muda wa ziada pamoja na malipo ya ulinzi kwa kampuni ya "*Idumu Cooperative Society*" ili kuweka usalama wa wageni wafikao hapo Hotelini.

Mhe. Spika, Hoteli ya Bwawani kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 995,000,000/= na imefanikiwa kukusanya shilingi 237,086,045/= sawa asilimia 24 hadi Aprili 2015. Katika mafanikio haya Hoteli ya Bwawani imeweza kutekeleza shughuli zake kama zinavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 39 na 40.

**SEKTA YA UTAMADUNI NA MICHEZO**

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imeundwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, Baraza la Kiswahili, Baraza la Sanaa Sensa ya Filamu na Utamaduni na Baraza la Taifa la Michezo. Taasisi hizi zimepewa jukumu la kusimamia, kuratibu, kufufua, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za Utamaduni na Michezo Zanzibar.

**KAMISHENI YA UTAMADUNI NA MICHEZO**

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ni kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni na michezo hapa Zanzibar kwa kushirikiana na Idara na Mabaraza yaliyo chini yake. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ilipanga kutekeleza malengo yake kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 41.

i. Kuwa na maendeleo ya Utamaduni na Michezo kwa kuanzisha Programu ya bonanza za Utamaduni na Michezo, kuwezesha kushirikishwa Timu katika Mashindano ya Kitaifa na Kimataifa, kuendeleza Nyumba ya Sanaa na kufanya tafiti za Utamaduni.

ii. Kuwa na mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi nafasi za masomo na kuipatia Ofisi vitendea kazi ili kuleta ufanisi zaidi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Katika kuhakikisha timu zinashiriki mashindano ya kitaifa na kimataifa Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imewagharamia wanariadha kushiriki katika mshindano ya Afrika nchini Moroco. Aidha, Kamisheni imefanikisha timu za Zanzibar kushiriki kwenye mashindano mbali mbali.
ii. Katika kuimarisha viwanja vya michezo Kamisheni imerekebisha mfumo wa maji katika Uwanja wa Amaan pamoja na kugharamia hati miliki ya Kiwanja cha Michezo kilichopo Nungwi.
iii. Kamisheni imewawezesha wasanii 25 kushiriki katika Tamasha la Utamuduni nchini Oman kwa lengo la kukuza mashirikiano na kuutangaza Utamaduni wetu Kimataifa. Pia Kamisheni imeratibu siku ya mazoezi kwa kushirikiana na washirika wakubwa wa mazoezi *ZABESA* kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kuwa na mazoezi ya viungo kwa ajili ya kuimarisha afya zao.
iv. Kamisheni imeifanyia marekebisho Sheria ya Ngoma na Sheria ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho Zanzibar kwa kuziunganisha pamoja na kuwa sheria moja inafahamika Sheria ya Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni ambayo imeshapitishwa na Baraza lako tukufu.
v. Kazi ya ununuzi wa vifaa vya kurikodia sauti na picha kwa ajili ya Studio ya Muziki na Filamu imekamilika na studio hiyo iko tayari kutumika.
vi. Kamisheni imeendelea kufanya malipo kwa wafanyakazi wake watano (5) waliopo masomoni katika ngazi ya Diploma, Cheti na Stashahada. Pia imewapatia stahiki za likizo, muda wa ziada na posho la kukaimu wafanyakazi wake kwa ajili ya kuongeza ari ya kazi.
vii. Katika kuweka mazingira bora ya kazi Kamisheni imenunua vitendea kazi mbali mbali.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kamisheni iliidhinishiwa jumla ya shilingi 864,412,000/= kwa kazi za kawaida hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 659,639,148 sawa na asilimia 76 kwa kazi za kawaida. Na katika rasilimali hizo Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imetekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 42 na 43.

**IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE**

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Idara hii ni kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza historia ya Zanzibar kwa kutumia Makumbusho, na maeneo ya kihistoria. Pia kuelimisha jamii juu ya umuhimu na faida za matumizi ya Makumbusho na

Mambo ya Kale. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ilipanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 43 na 44.

i. Kuwa na Makumbusho yenye ubora wa kimataifa kwa kuyaendeleza, kuyafanyia matengenezo na kuyawekea uzio ili kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni na historia nchini.
ii. Kuwa na maeneo ya kihistoria yalio endelevu kwa kuandaa viongozi wa Shehia katika kila Wilaya, kuanzisha programu zitakazowajengea wananchi mwamko juu ya umuhimu wa kuhifadhi na kulinda maeneo ya kihistoria kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.
iii. Kuwa na mazingira bora ya kazi yatakayowezesha Idara kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuipatia vifaa muhimu vya kutendea kazi na kuwajenga wafanyakazi kielimu na kitaaluma.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Katika kuyaweka majengo ya makumbusho katika hali ya kuvutia Idara imeyafanyia usafi majengo ya Mnazi mmoja na Makumbusho ya Kasri ya Mfalme Forodhani pamoja na ununuzi wa vifaa vya zamani katika jitihada za kutunza na kuendeleza uhifadhi wa historia.
ii. Katika kufanya utafiti wa maeneo ya kihistoria kwa ajili ya maendeleo ya Utalii taarifa za eneo la Kasri ya Chukwani zimekusanywa. Pia Idara imeendelea na utafiti wa pango la Kuumbi kwa kushirikiana na wanafunzi wa Chuo cha Winscon cha Marekani.
iii. Katika kuanzisha programu zitakazowajengea wananchi muamko wa kulinda na kuhifadhi maeneo ya kihistoria Idara imeandaa vipindi 18 vilivyorikodiwa na kurushwa hewani kupitia *ZENJ FM*, *ZBC* Redio, Chuchu *FM* na Redio Jamii ya Tumbatu juu ya Historia ya Beit-El-Amaan na Kisima cha Wivu kilichoko Pujini Pemba pamoja na athari za uvamizi wa maeneo ya kihistoria na hasara zake katika kulinda na kuhifadhi urithi wa Historia na Utamaduni wa nchi yetu.
iv. Ukusanyaji wa picha za maeneo ya Kihistoria ya Mangapwani, Chuini, Kijichi, Msikiti wa Kizimkazi na Tumbatu umekamilika na kufanyiwa tafsiri kwenye mabango ya matangazo katika lugha nne tofauti ambazo ni Kiswahili, Kitaliano, Kifaransa na Kiingereza ili kuleta tija kwa wanyeji na wageni wanaotembelea katika maeneo hayo.
v. Idara imeandaa ziara ya kuwatembeza waandishi wa habari katika maeneo ya kihistoria kwa lengo la kushajiisha jamii juu ya utalii wa ndani, kujenga dhamira ya kuhimiza utalii kwa wote kwa jamii ya Zanzibar

pamoja na usambazaji wa vipeperushi vya maeneo ya kihistoria katika sehemu za Bandarini, Ngome Kongwe, na Kamisheni ya Utalii.

vi. Idara imeendelea kuwalipia ada ya masomo wafanyakazi wake watano (5), waliokuwepo vyuoni, Stashahada ya Manunuzi na Ugavi (2), Utunzaji wa Kumbukumbu (1), Uhifadhi wa Urithi wa Utamaduni (2) katika vyuo tofauti. Aidha, Idara imefanya sehemu ya malipo ya wafanyakazi wake wawili (2) waliohudhuria mafunzo ya muda mfupi nchini Kenya, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji katika shughuli zao za kila siku.

vii. Katika kuandaa mikutano pamoja kufuatilia shughuli za kazi ndani na nje ya nchi, Idara imemgharamia mtendaji wake safari ya kikazi nchini Oman kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa Kiutamaduni baina ya nchi mbili.

viii. Idara katika kuweka mazingira bora ya Ofisi imefanya malipo ya ununuzi wa vitendea kazi kama vile, Kompyuta 1 na Printer 1 na mafuta ya dizeli, petroli, umeme, intanet. Aidha, Idara imewapatia stahiki za likizo wafanyakazi, muda wa ziada na malipo kwa walinzi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 603,973,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 150,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 392,206,301/= sawa na asilimia 65 kwa kazi za kawaida na shilingi 41,754,270 sawa na asilimia 28 kwa kazi za maendeleo. Pia ilipangiwa kukusanya shilingi 210,000,000/= na kufanikiwa kukusanya shilingi 66,103,359/= sawa na asilimia 31 hadi kufikia Aprili, 2015. Na upatikanaji huo wa rasilimali Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imefanikiwa kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 44 hadi 46.

## BARAZA LA KISWAHILI LA ZANZIBAR

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Kiswahili la Zanzibar ni kukuza, kushajiisha na kufuatilia matumizi na maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza hili lilipanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 47.

i. Kuendeleza na kukuza matumizi ya Kiswahili fasaha kitaifa na kimataifa.

ii. Kuwa na mazingira mazuri ya kazi kwa kuipatia ofisi vitendea kazi na kuwapatia wafanyakazi fursa za masomo.

## UTEKELEZAJI HALISI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza la Kiswahili limetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Katika kutoa taaluma juu ya matumizi sahihi na fasaha ya Kiswahili kupitia Vyombo vya Habari pamoja na kukitangaza Kiswahili kitaifa na kimataifa, Baraza limeandaa vipindi 18 vya “Kiswahili lugha yetu” vilivyorushwa kupitia *ZBC TV*, *ZBC* Redio, *Hits FM* na Redio *Coconut FM* vinavyosaidia kukuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili.
ii. Baraza limefanya kikao na wajumbe walioleta taarifa za kukusanya msamiati wa viumbe vya baharini na ule wenye mnasaba na mazingira ya baharini kwa lengo la kuandaa Kamusi la Majina ya Viumbe vya Baharini. Pia Baraza limefanya kikao kimoja cha wajumbe wa BAKIZA na malipo ya kitabu cha Kiswahili kwa wageni.
iii. Kuadhimisha Siku ya Kiswahili kwa kufanya mashindano ya vitendawili na hadithi kwa kuwashirikisha wanafunzi wa elimu ya msingi na kufanya kongamano katika kuadhimisha siku hiyo
iv. Kushiriki katika kikao cha Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki kilichofanyika Arusha na kikao cha Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki mjini Dar es Salaam.
v. Kuimarisha Ofisi kwa kuipatia vitendea kazi kama vifaa vya kuandikia, umeme, mafuta pamoja na matengenezo ya gari ili kurahisisha utendaji wa kazi za kila siku.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Baraza la Kiswahili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 32,800,000/= kwa matumizi ya kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 limefanikiwa kupata shilingi 30,000,000 sawa na asilimia 91. Baraza lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 40,000,000/= na kufanikiwa kupata shilingi 1,229,000/= sawa na asilimia 3. Na Baraza la Kiswahili limetekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 47 na 48.

**BARAZA LA SANAA ZANZIBAR**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza la Sanaa lilipanga kutekeleza malengo makuu mawili kama yanavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 48.

i. Kuwa na maendeleo ya sanaa na wasanii kwa kuwafanya wananchi kushiriki na kutekeleza shughuli za sanaa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

ii. Kuimarisha mazingira ya kazi yatakayowezesha Baraza kufanya kazi zake kwa ubora na ufanisi zaidi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza la Sanaa limefanikiwa kutekeleza malengo yake kama yafuatavyo:-

i. Katika kuwashajiisha wasanii, kuziendeleza kazi zao ili kuyatumia masoko yaliopo na kujiongezea mapato, Baraza liliwakutanisha wasanii wa vikundi 3 vya sanaa za kazi za mikono katika wilaya 4 za Zanzibar zikiwemo Wilaya Kusini – Jambiani, Kaskazini A - Mkwajuni, Wilaya ya Kaskazini B – Bumbwini na Wilaya ya Kati – Kidimni kujadili maendeleo ya kazi zao.
ii. Baraza lilifanya kikao na Wajumbe wa Baraza hilo kwa lengo la kuanzisha Sheria mpya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni, Sheria ambayo ishakamilika na tayari inafanya kazi kwa sasa. Aidha, katika kukuza uhusiano na mashirikiano baina ya BASAZA na BASATA, Baraza limeshiriki katika mashindano ya ushairi wa Ibrahim Hussein yaliyofanyika Dar es Salaam.
iii. Katika kuimarisha Ofisi na vitendea kazi Baraza limelipia huduma za umeme, maji, mafuta ya petroli na dizeli, vifaa vya kuandikia na vifaa vya usafi. Aidha, Baraza limeendelea kugharamia masomo kwa mfanyakazi mmoja (1) anayesoma Stashahada ya Ukatibu Muhtasi pamoja na kulipa stahiki za likizo na posho la kukaimu kwa wafanyakazi wake.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Baraza la Sanaa liliidhinishiwa jumla ya shilingi 15,800,000/= kwa Matumizi mengineyo na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 14,000,000/= sawa na asilimia 89. Baraza lilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 10,000,000/= na kufanikiwa kupata shilingi 4,970,000/= sawa na asilimia 50. Na kwa upatikanaji huo wa fedha Baraza la Sanaa limefanikiwa kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 49.

**BODI YA SENSA YA FILAMU NA SANAA ZA MAONESHO**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Bodi hii imepanga kutekeleza malengo makuu mawili kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 50.

i. Kuwa na kazi za sanaa zilizo bora zenye kuzingatia Mila, Silka na Utamaduni wa Mzanzibari.

ii. Kuwa na mazingira bora ya kutendea kazi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuipatia Ofisi vitendea kazi.

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho limefanikiwa kutekeleza malengo yake kama yafuatavyo:-

i. Katika kukagua filamu na sanaa zinazooneshwa hadharani ili kuhakikisha zinaendana na Maadili ya Kizanzibari, jumla ya filamu 254 zimekaguliwa kati ya hizo filamu 180 kutoka *ZIFF* ambapo kwa ujumla wake filamu 14 kati ya hizo zimekataliwa, 12 zimefanyiwa marekebisho na 183 zimekubaliwa kuoneshwa hadharani. Aidha, Bodi imefanya ukaguzi wa kazi za maigizo 15 kati ya hizo tano (5) zimekubaliwa na mbili (2) zimekataliwa kuoneshwa kutokana na kutoendana na maadili ya Mzanzibari.
ii. Baraza katika kutoa taaluma jinsi ya utayarishaji wa kazi zinazoendana na Milka, Silka na Utamaduni wa Kizanzibari, Bodi imefanya vikao viwili (2) na Jumuiya ya Wapiga Picha pamoja na kuandaa Semina kwa wasanii thalathini (30) wa filamu na maigizo kwa lengo la kuwajengea uelewa katika kazi zao.
iii. Katika kuweka mazingira bora ya Ofisi, Bodi imeghramia upatikanaji wa vitendea kazi kama vile, maji, umeme, huduma za mawasiliano na mafuta ya dizeli na petroli. Aidha, Bodi ilimlipia mafunzo mfanyakazi mmoja (1) katika fani ya Katibu Muhtasi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho liliidhinishiwa jumla ya shilingi 15,500,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 14,500,000/= sawa na asilimia 94. Na rasilimali hizo zimesababisha Bodi ya Sensa, Filamu, Sanaa na Maonesho kufanikiwa kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 50 na 51.

**BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO**

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza hili limepanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 52.

i. Kuwa na mazingira bora ya shughuli za maendeleo ya michezo

ii. Kuweka mazingira mazuri ya kazi

**UTEKELEZAJI HALISI**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Katika kushajiisha na kuhamasisha mashindano ya vijana na watoto chini ya umri wa miaka 19, Baraza limeitayarisha timu ya Taifa ya vijana ya Zanzibar kwa ajili ya kushiriki mashindano ya *Challenge* ya Mpira wa Mikono (*ZAHA*) nchini Uganda na mashindano ya Ligi Kuu ya Zanzibar.
ii. Baraza limefanikisha kuanda mashindano ya michezo katika ligi tofauti ambazo ni ligi ya mpira wa pete, ligi ya mpira wa wavu, mbio za baskeli, mpira wa meza, mpira wa vinyoya na mchezo wa judo. Aidha, Baraza limeratibu Bonanza la mazoezi ya viungo kwa ajili ya kushajiisha wananchi kufanya mazoezi ili kudumisha na kuimarisha afya zao.
iii. Katika kusaidia shughuli za maendeleo ya michezo kwa watu wenye ulemavu, Baraza limewawezesha viongozi watatu wa chama cha viziwi (CHAMIVIZA) kushiriki kikao Dar - es - Salaam kujadili ushiriki wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa yatakayofanyika nchini *Ivory Coast*. Aidha, wachezaji wenye ulemavu wa viungo wamesaidiwa kushiriki mashindano ya kutafuta viwango vya kimataifa yaliyofanyika Dar – es – Salaam
iv. Kufanya mapitio ya katiba za vyama 4 vya michezo. Baraza limegharamia mkutano mkuu wa chama cha mpira wa miguu (*ZFA*) kwa ajili ya kupitisha katiba yao, pia Baraza limegharamia mkutano mkuu wa washirika wa michezo kwa ajili ya kupata wajumbe wapya wa *BTMZ.*
v. Katika kuwaongezea ujuzi na maarifa watendaji wake, Baraza limewagharamia wafanyakazi wake wawili (2) katika ngazi ya Diploma (*ICT and Account*) katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii na ngazi ya Diploma ya Ukatibu Muhtasi.
vi. Aidha, Baraza limenunua vifaa vya ofisi, mafuta pamoja na kuipatia ofisi huduma ya intanet na simu kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa kila siku.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Baraza liliidhinishiwa jumla ya shilingi 70,000,000/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Aprili, 2015 imefanikiwa kupata shilingi 69,319,448/= sawa na asilimia 99. Kwa upatikanaji huo wa fedha Baraza la Taifa la Michezo limefanikiwa kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 52 na 53.

**KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (*PROGRAM BASED BUDGET* - *PBB*) KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

Mhe. Spika, katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 Serikali inaendelea kufanya mageuzi ya bajeti ikiwa ni sehemu ya mageuzi ya utawala na udhibiti wa fedha za umma. Mageuzi hayo ni kutoka mfumo wa bajeti wa sasa unaotumia vifungu (*line item*) kwenda katika mfumo unaotumia programu (*PBB*). Kama ilivyoelezwa katika matoleo mbali mbali ya Serikali, mageuzi ya bajeti inayozingatia matokeo itapelekea ufanisi katika kutatua changamoto nyingi zinazoikabili serikali kwa sasa ambapo, mfumo huo unategemewa kuleta uwiano mzuri wa Mipango ya Taifa katika bajeti pamoja na kuweka uwazi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa jamii.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imepanga kutekeleza programu kuu tano (5) nazo ni:-

1. Programu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji.
2. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo.
3. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii
4. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii.
5. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Spika, wizara itatumia jumla ya shilingi 13,052,200,000/= kwa ajili ya kutekeleza programu hizo tano.

**Programu ya 1: Maendeleo ya Habari na Utangazaji.**

Mhe. Spika, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa na jamii iliyoimarika katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia habari. Aidha, matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni wananchi kupata na kutumia habari zenye kiwango bora. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 3,841,853,000/= na imepangiwa kusimamia programu ndogo mbili:-

- Upatikanaji na Usambazaji wa Habari.
- Usimamizi wa Vyombo vya Habari na Utangazaji.

Mhe. Spika, katika programu ndogo ya upatikanaji na usambazaji wa habari inatekelezwa na taasisi na idara tofauti nazo ni, Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*), Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti, Chuo cha Uandishi wa Habari na Kampuni ya Uunganishaji Maudhui (*ZMUX*). Jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha jamii, kuratibu

uchapishaji wa magazeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kutoa mafunzo ya taaluma ya uandishi wa habari na mawasiliano. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni urushaji wa vipindi kupitia TV/Redio, utoaji wa taarifa picha, makala, filamu na sinema, utoaji wa magazeti, utoaji wa mafunzo ya habari na mawasiliano na usambazaji wa maudhui ya utangazaji.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 3,601,853,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya Shilingi 1,178,000,000/=.

Mhe. Spika, programu ndogo ya pili ni usimamizi wa vyombo vya habari na utangazaji ambayo inatekelezwa na taasisi na idara zifuatazo: Idara ya Habari Maelezo na Tume ya Utangazaji Zanzibar na jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kusimamia vyombo vya utangazaji vya serikali na vya binafsi vinavyoanzishwa nchini ili kwenda sambamba na Sheria ya Habari na Utangazaji. Huduma ambayo inayotarajiwa kutolewa ni udhibiti na usimamizi wa shughuli za habari na utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2015/2016, naliomba Baraza lakotukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 240,000,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya shilingi 65,000,000/=

**Programu ya 2: Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo**

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa Utamaduni wa Zanzibar unawaendeleza wasanii kiuchumi na kupunguza umasikini pamoja na kuwa na rasilimali watu yenye ujuzi na ustadi wa kukuza utalii nchini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga afya na ajira kwa jamii. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa soko la kazi za sanaa, uhifadhi wa utamaduni, kukuza utalii kupitia rasilimali watu yenye ujuzi na ustadi na kutoa ajira kwa jamii kupitia michezo. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 2,955,069,000/= na itakuwa na programu ndogo mbili.

- Uimarishaji wa Utamaduni na Maeneo ya Kihistoria.
- Uendelezaji wa Rasilimali watu katika Utalii na Ukuzaji wa Michezo.

Mhe. Spika, programu ndogo ya uimarishaji wa utamaduni na maeneo ya kihistoria inatekelezwa na taasisi na idara zifuatazo: Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni, Baraza la Kiswahili, na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, jukumu la msingi katika programu hii ndogo ni kusimamia, kuratibu, kuimarisha, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za

utamaduni Zanzibar. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, kurikodi kazi za sanaa kupitia studio ya filamu na muziki, uratibu wa kazi za sanaa na wasanii, ukaguzi wa filamu na sanaa za maonesho, utoaji wa elimu kuhusu matumizi fasaha ya Kiswahili, uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya kihistoria, uelimishaji na ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na urithi wa utamaduni.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,585,349,000/= kwa kazi za kawaida na makusanyo ya shilingi 290,812,000/=.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya uendelezaji wa utalii na ukuzaji wa michezo inatekelezwa na Taasisi na Idara zifuatazo, Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo na Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ), jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kutoa taaluma ya Utalii itakayowezesha kuijenga rasilimali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika na kukubalika katika viwango vya kimataifa pamoja na kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa nchini. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni utoaji wa mafunzo ya Utalii, ukarimu na ujasiriamali, uratibu na uendelezaji wa shughuli za michezo, uendelezaji wa miundombinu ya michezo na usimamizi wa shughuli za vyama vya michezo kupitia Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ).

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kufanya kazi zake katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 889,720,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 480, 000,000/= kwa mradi wa maendeleo na makusanyo ya shilingi 454,000,000/=.

**Programu ya 3: Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii**

Mhe. Spika, programu hii inayotekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili kuleta tija kwa maslahi ya taifa.

Mhe. Spika, lengo kuu la programu hii ni kuongeza tija ya sekta ya Utalii kwa kuongeza ajira kwa jamii, idadi ya watalii na thamani yao. Aidha, matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuifanya Zanzibar kuwa kituo bora cha Utalii chenye kukidhi mahitaji ya jamii na watalii. Huduma inayotarajiwa kutolewa ni kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 304,500,000/= kwa kazi za kawaida, na makusanyo ya shilingi 1,656,951,000/=.

**Programu ya 4: Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii.**

Mhe. Spika, Programu hii inayotekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Mipango na Sera, yenye jukumu la kuratibu na uendelezaji wa utalii pamoja na kuwajenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi wafanyakazi wa Kamisheni.
Mhe. Spika, lengo kuu la programu hii ni kuwa na mazingira na rasilimali watu bora katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa será na mipango ya utalii. Aidha, matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuwepo kwa utalii endelevu na wenye kuhimili ushindani. Huduma ambazo zinazotarajiwa kutolewa ni uratibu na uendelezaji wa utalii na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi

Mhe. Spika, ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 921, 400,000/= kwa kazi za kawaida.

**Programu ya 5: Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.**

Mhe. Spika, programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Aidha, matokeo ya muda mrefu wa programu hii ni kuwepo kwa usimamizi bora wa mipango na uendashaji wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 5,029,378,000/= na itasimamia programu ndogo tatu.

- Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
- Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.
- Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, programu ndogo ya utawala na uendeshaji katika Sekta za Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo itatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo ina jukumu la kusimamia shughuli zote za utawala, utumishi, maendeleo, wajibu na maslahi ya wafanyakazi wa wizara.

Mhe. Spika, lengo kuu la programu ndogo hii ni usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu wa wizara. Huduma ambazo zinazotarajiwa kutolewa ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi na utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,370,153,000/= kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, programu ndogo ya kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya wizara ambayo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kuratibu, kufuatialia  na kutathmini mipango, Sera, tafiti na miradi ya maendeleo kwa wizara.

Mhe. Spika, lengo kuu la programu ndogo hii ni kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti za wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera na tafiti, kuratibu, kuandaa na kuwasilisha bajeti na kuratibu mipango na miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 120,305,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 2,500,000,000/= Kwa utekelezaji wa programu ya Maabara ya Utalii.

Mhe. Spika, programu ndogo ya kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango ya Ofisi Kuu-Pemba, ambayo inatekelezwa na  Ofisi Kuu Pemba, ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za wizara Pemba. Programu ndogo hii ni kiunganishi katika kuhakikisha majukumu, malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, lengo kuu la programu ndogo hii ni kusimamia na kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu-Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa será, tafiti na mipango mikuu Wizara-Pemba, kuratibu miradi ya maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

Mhe. Spika, ili programu hii ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2015/2016 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,038, 920,000/= kwa kazi za kawaida.

**SHUKRANI**

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Shukurani maalumu ziwaendee Mhe. Naibu Waziri Bihindi Hamad Khamis, Katibu Mkuu Dk. Ali Saleh Mwinyikai, Manaibu Katibu Wakuu Nd. Issa Mlingoti na Dk. Juma Yakuti, Makatibu Watendaji wa Kamisheni ya Utalii na Tume ya Utangazaji, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi, Wakuu wengine wa Taasisi za Wizara na wasaidizi wao wote kwa kufanya kazi kwa juhudi, maarifa, uadilifu na umakini mkubwa. Kwa kweli wamekuwa wakinisaidia sana kutekeleza majukumu yangu. Pia nawashukuru Wenyeviti wa Mabaraza na Bodi mbali mbali kwa kusimamia vyema taasisi zetu na kunishauri kwa hekima na busara.

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru wafanyakazi, wamiliki wa vyombo vya habari na waandishi wa habari, wanamichezo, wasanii, washirika wa utalii na wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa michango yao katika kufanikisha shughuli za wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuishukuru Wizara ya Fedha pamoja Tume ya Mipango kwa ushirikiano mkubwa waliotupa kwa mahitaji ya fedha na ushauri.
Mhe. Spika, naomba uniruhusu nizishukuru nchi mbali mbali na Mashirika kadhaa ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Serikali ya Misri, Japan, Serikali ya Ujerumani, Serikali ya Oman, *UNESCO* na Shirika la Utangazaji la Ujerumani (*DW*) tuliyoshirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu ya wizara yetu.

Mhe. Spika, mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini mkubwa. Aidha, naomba kuishukuru tena Kamati ya Mifugo, Habari, Uwezeshaji na Utalii kwa namna ambavyo muda wote imekuwa ikinisaidia katika kuisimamia na kuiongoza wizara hii.

Mhe. Spika, naliomba sasa Baraza lako Tukufu kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya shilingi 13,052,200,000/=. Fedha hizo ni pamoja na miradi iliyoibuliwa kwenye Maabara ya Utalii (*Tourism Laboratory*). Kati ya hizo shilingi 10,072, 200,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 480,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Pia naomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,500,000,000/= kwa utekelezaji wa Programu ya Utalii**.**

Aidha, naliomba Baraza lako liidhinishe makusanyo ya mapato ya shilingi 2,050,763,000/= kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia makusanyo ya shilingi 2,589,000,000/= ambazo hukusanywa na taasisi

zilizoruhusiwa kutumia makusanyo hayo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za taasisi hizo**.**

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili, watushauri, watuelekeze na hatimaye watupitishie Bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sasa naomba kutoa hoja.

## VIAMBATANISHO

**KIAMBATANISHO NAMBA 1A FEDHA ZILIZOINGIZWA JULAI 2014 HADI APRILI 2015 KWA MATUMIZI YA KAWAIDA.**

| | IDARA | MAELEZO | FEDHA ZILIZOTENGWA 2014/2015 | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI APRIL 2015 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 416,141,000 | 355,143,650 | 85% |
| | | Matumizi Mengineyo | 928,172,000 | 859,000,000 | 93% |
| | **JUMLA** | | **1,344,313,000** | **1,214,143,650** | 90% |
| 2 | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - | - | |
| | | Matumizi Mengineyo | 82,949,000 | 42,798,064 | 52% |
| | **JUMLA** | | **82,949,000** | **42,798,064** | 52% |
| 3 | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 737,382,000 | 605,469,300 | 82% |
| | | Matumizi Mengineyo | 700,464,000 | 339,758,842 | 49% |
| | **JUMLA** | | **1,437,846,000** | **945,228,142** | 66% |
| 4 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 1,239,290,000 | 1,026,763,352 | 83% |
| | | Matumizi Mengineyo | 315,000,000 | 165,000,000 | 52% |
| | **JUMLA** | | **1,554,290,000** | **1,191,763,352** | 77% |
| 5 | Idara ya Habari Maelezo | Mishahara | 235,975,000 | 166,986,300 | 71% |
| | | Matumizi Mengineyo | 85,332,000 | 28,672,229 | 34% |
| | **JUMLA** | | **321,307,000** | **195,658,529** | 61% |
| 6 | Shirika la Magazeti | Mishahara | 344,053,000 | 224,788,900 | 65% |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | ya Serikali | Matumizi Mengineyo | 243,673,000 | 243,673,000 | 100% |
| | **JUMLA** | | **587,726,000** | **468,461,900** | 80% |
| 7 | Chuo cha Uandishi wa Habari | Mishahara | 202,320,000 | 199,763,251 | 99% |
| | | Matumizi Mengineyo | 35,490,000 | 29,375,000 | 83% |
| | **JUMLA** | | **237,810,000** | **229,138,251** | 96% |
| 8 | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 146,499,000 | 131,649,399 | 90% |
| | | Matumizi Mengineo | 50,000,000 | 44,700,000 | 89% |
| | **JUMLA** | | **196,499,000** | **176,349,399** | 90% |
| 9 | Chuo cha Maendeleo ya Utalii | Mishahara | 370,029,000 | 259,809,001 | 70% |
| | | Matumizi Mengineyo | 44,000,000 | 29,320,000 | 67% |
| | **JUMLA** | | **414,029,000** | **289,129,001** | 70% |
| 10 | Kamisheni ya Utamaduni na Michezo | Mishahara | 641,811,000 | 508,353,600 | 79% |
| | | Matumizi Mengineyo | 205,101,000 | 148,685,548 | 72% |
| | **JUMLA** | | **846,912,000** | **657,039,148** | 78% |
| 11 | Bodi ya Sensa | Mishahara | - | - | |
| | | Matumizi Mengineyo | 15,500,000 | 14,500,000 | 94% |
| | **JUMLA** | | **15,500,000** | **14,500,000** | 94% |
| 12 | Idara ya Makumbusho | Mishahara | 430,791,000 | 353,778,300 | 82% |
| | | Matumizi Mengineyo | 154,282,000 | 37,255,371 | 24% |
| | **JUMLA** | | **585,073,000** | **391,033,671** | 67% |
| 13 | Baraza la Kiswahili | Mishahara | - | - | |
| | | Matumizi Mengineyo | 32,800,000 | 30,000,000 | 91% |
| | **JUMLA** | | **32,800,000** | **30,000,000** | 91% |
| 14 | Baraza la Sanaa | Mishahara | - | - | |
| | | Matumizi Mengineyo | 15,800,000 | 14,000,000 | 89% |
| | **JUMLA** | | **15,800,000** | **14,000,000** | 89% |
| 16 | Baraza la Michezo | Mishahara | - | - | |
| | | Matumizi Mengineyo | 70,000,000 | 69,319,448 | 99% |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **JUMLA** | | **70,000,000** | **69,319,448** | 99% |
| 17 | Shirika la Utangazaji Pemba | Mishahara | 144,246,000 | 122,206,200 | 85% |
| | | Matumizi Mengineyo | 41,000,000 | 34,740,000 | 85% |
| | **JUMLA** | | **185,246,000** | **156,946,200** | 85% |
| 18 | Idara ya Habari Maelezo Pemba | Mishahara | - | - | |
| | | Matumizi Mengineyo | 17,500,000 | 2,700,000 | 15% |
| | **JUMLA** | | **17,500,000** | **2,700,000** | 15% |
| 19 | Idara ya Makumbusho Pemba | Mishahara | - | - | |
| | | matumizi Mengineo | 18,900,000 | 2,700,000 | 14% |
| | **JUMLA** | | **18,900,000** | **2,700,000** | 14% |
| 20 | Kamisheni ya Utamaduni Pemba | Mishahara | - | - | |
| | | Matumizi | 17,500,000 | 2,600,000 | 15% |
| | **JUMLA** | | **17,500,000** | **2,600,000** | 15% |
| 21 | Kamisheni ya Utalii | Mishahara | 554,399,000 | 442,765,500 | 80% |
| | | Matumizi Mengineyo | 834,801,000 | 493,067,363 | 59% |
| | **JUMLA** | | **1,389,200,000** | **935,832,863** | 67% |
| | **JUMLA KUU** | | **9,371,200,000** | **7,029,341,618** | 75% |

## KIAMBATANISHO NO. 1B FEDHA ZILIZOINGIZWA JULAI 2014 HADI APRILI 2015 KWA KAZI ZA MAENDELEO

| | MIRADI YA MAENDELEO | BAJETI | MATUMIZI HADI APRIL 2015 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uhifadhi wa Maeneo ya kihistoria na Mambo ya Kale. | 150,000,000 | 41,754,270 | 28% |
| 2 | Mradi wa Maabara ya Utalii (*Tourism Lab*) | 5,595,375,000 | 476,745,730 | 9% |
| 3 | Ujenzi wa vituo kutoa taarifa za Usalama za Utalii | 250,000,000 | 80,000,000 | 32% |
| | **JIMLA KUU** | **5,995,375,000** | **598,500,000** | 10% |

### KIAMBATANISHO NO. I C FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2014 HADI APRILI 2015.

| S/N | TAASISI | BAJETI YA REVENUE | MAPATO YALIYOKUSANYWA HADI APRIL 2015 | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | IDARA YA MAKUMBUSHO | 210,000,000 | 66,103,359 | 31% |
| 2 | KAMISHENI YA UTAMADUNI | 50,000,000 | 6,199,000 | 12% |
| 3 | TUME YA UTANGAZAJI | 52,000,000 | 30,248,894 | 58% |
| 4 | IDARA YA HABARI MAELEZO | 19,000,000 | 7,255,500 | 38% |
| 5 | KAMISHENI YA UTALII | 1,340,000,000 | 1,427,291,516 | 107% |
| | **GRAND TOTAL** | **1,671,000,000** | **1,537,098,269** | **92%** |

**KIAMBATANISHO NO. 1 D FEDHA ZILIZOKUSANYWA NA TAASISI AMBAZO ZIMEPEWA UWEZO WA KUTUMIA MAKUSANYO YAKE KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2014 HADI APRILI 2015.**

| S/NO. | TAASISI | FEDHA ZILIZO PANGWA KUKU SANYWA | FEDHA ZILIZO KUSANYWA | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Chuo cha Uandishi wa Habari | 126,250,000 | 93,451,300 | 74% |
| 2 | Chuo cha Maendeleo ya Utalii | 360,000,000 | 297,348,014 | 83% |
| 3 | Hoteli ya Bwawani | 995,000,000 | 237,086,045 | 24% |
| 4 | Shirika la Magazeti ya Serikali | 500,000,000 | 268,864,325 | 54% |
| 5 | Shirika la Utangazaji (*ZBC*) | 300,000,000 | 277,415,538 | 92% |
| 6 | Kampuni ya Uunganishaji Maudhui (*ZMUX*) | 140,000,000 | 72,272,000 | 52% |
| | **Jumla** | **2,421,250,000** | **1,246,437,222** | **51%** |

**KIAMBATANISHO NAMBA 1 E FEDHA ZINAZOOMBWA JULAI 2015 HADI JUNI 2016.**

| | IDARA | MAELEZO | FEDHA ZILIZOTE NGWA 2015/2016 |
|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 433,900,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 605,020,000 |
| | **JUMLA** | | **1,038,920,000** |
| 2 | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineyo | 120,305,000 |
| | **JUMLA** | | **120,305,000** |
| 3 | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 756,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 614,153,000 |
| | **JUMLA** | | **1,370,153,000** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 1,245,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 390,000,000 |
| | **JUMLA** | | **1,635,000,000** |
| 5 | Idara ya Habari Maelezo | Mishahara | 210,900,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 114,358,000 |
| | **JUMLA** | | **325,258,000** |
| 6 | Shirika la Magazeti ya Serikali | Mishahara | 311,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 249,610,000 |
| | **JUMLA** | | **560,610,000** |
| 7 | Chuo cha Uandishi wa Habari | Mishahara | 270,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 52,490,000 |
| | **JUMLA** | | **322,490,000** |
| 8 | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 165,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 55,000,000 |
| | **JUMLA** | | **220,000,000** |
| 9 | Chuo cha Maendeleo ya Utalii | Mishahara | 320,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 49,000,000 |
| | **JUMLA** | | **369,000,000** |
| 10 | Kamisheni ya Utamaduni na Michezo | Mishahara | 589,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 460,601,000 |
| | **JUMLA** | | **1,049,601,000** |
| 11 | BASFU | Mishahara | 56,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 90,000,000 |
| | **JUMLA** | | **146,000,000** |
| 12 | Idara ya Makumbusho | Mishahara | 431,900,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 234,282,000 |
| | **JUMLA** | | **666,182,000** |
| 13 | Baraza la Kiswahili | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineyo | 40,800,000 |
| | **JUMLA** | | **40,800,000** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 14 | Kampuni ya Uunganishaji Maudhui | Mishahara | 120,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 427,000,000 |
| | **JUMLA** | | **547,000,000** |
| 16 | Baraza la Michezo | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineyo | 90,000,000 |
| | **JUMLA** | | **90,000,000** |
| 17 | Shirika la Utangazaji Pemba | Mishahara | 160,000,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 41,000,000 |
| | **JUMLA** | | **201,000,000** |
| 18 | Idara ya Habari Maelezo Pemba | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineyo | 30,495,000 |
| | **JUMLA** | | **30,495,000** |
| 19 | Idara ya Makumbusho Pemba | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineyo | 53,367,000 |
| | **JUMLA** | | **53,367,000** |
| 20 | Kamisheni ya Utamaduni Pemba | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineyo | 60,119,000 |
| | **JUMLA** | | **60,119,000** |
| 21 | Kamisheni ya Utalii | Mishahara | 594,300,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 631,600,000 |
| | **JUMLA** | | **1,225,900,000** |
| | **JUMLA KUU** | | **10,072,200,000** |

## KIAMBATANISHO NAMBA 2: WAFANYAKAZI WA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO AMBAO WAMEKWENDA MASOMONI KWA MWAKA 2014/2015

| | Jina Kamili | Jinsi | Taasisi | Fani | Kiwango | Muda | Chuo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mwan'dawa Ibrahim Othman | Mke | Uendeshaji na Utumishi | Utawala wa Umma | Shahada 2 | Miaka 1 | Tsinghua University |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Abdillah Haji Manzi | Mke | Uendeshaji na Utumishi | Ugavi na Ununuzi | Shahada 1 | Miaka 3 | Zanzibar University |
| 3. | Wahida Ali Khatibu | Mke | Uendeshaji na Utumishi | Human Resource | Stashahada | Miaka 2 | ICPS, Zanzibar |
| 4. | Moh'd Haji Makame | Mume | Uendeshaji na Utumishi | Utunzaji wa Kumbukum | Cheti | Mwaka 1 | ICPS, Zanzibar |
| 5. | Ali Abdallah Salum | Mume | Mipango Sera na Utafiti | Network and Security | Shahada 2 | Miaka 2 | University of Bagamoy |
| 6. | Zaituni Mwalim Suleiman | Mke | Habari Maelezo | Teknolojia ya Habari na Uhasibu | Stashahada | Miaka 2 | ICPS, Zanzibar |
| 7. | Nassor Ameir Nassor | Mume | Hoteli ya Bwawani | Law | Shahada | Miaka 3 | Bagamoyo University |
| 8. | Asha Khamis Burhani | Mke | Hoteli ya Bwawani | Hospitality and Hotel Mgt | Stashahada | Miaka 2 | ZIToD |
| 9. | Is-hak Hassan Is-hak | Mume | Hoteli ya Bwawani | Hospitality and Hotel Mgt | Stashahada | Miaka 2 | ZIToD |
| 10 | Khadija Khamis Abeid | Mke | Hoteli ya Bwawani | House Keeping | Cheti | Mwaka 1 | ZIToD |
| 11 | Rahma Hamza Koa | Mke | Hoteli ya Bwawani | Food Preparation & Pastry | Cheti | Mwaka 1 | ZIToD |
| 13 | Mwaka Khamis Haji | Mke | Hoteli ya Bwawani | Food Preparation & Pastry | Cheti | Mwaka 1 | ZIToD |
| 14 | Yahya Khamis | Mume | Hoteli ya Bwawani | Food & Bevarage | Cheti | Mwaka 1 | ZIToD |
| 15 | Salum Said Mkombo | Mume | Hoteli ya Bwawani | Front Office Operation | Cheti | Mwaka 1 | ZIToD |
| 16 | Tatu Rajab Omar | Mke | Chuo cha M/Utalii | Mapishi | Stashahada | Miaka 2 | National College of Tourism |
| 17 | Hassan Hussein Abdalla | Mme | Chuo cha M/Utalii | Uongozi wa Hoteli na Utalii | Stashahada | Miaka 2 | ZIToD |
| 18 | Issa Shaaban Moh'd | Mme | Chuo cha M/Utalii | Utafiti na Sera za Umma | Shahada ya pili | Miaka 2 | Mzumbe |
| 19 | Maganga Msafiri Fungameza | Mme | Chuo cha M/Utalii | Logistics Management | Shahada ya Pili | Miaka 2 | Chuo cha Uhasibu Arusha |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 20 | Fatma Msanif Ali | Mke | WHUUM/ Pemba | HRM | Stashahada | Miaka 2 | Dar College of Business |
| 21 | Issa Juma Issa | Mume | WHUUM/ Pemba | HRM | Stashahada | Miaka 2 | Zanzibar College of Business |
| 22 | Salha A. Abdalla | Mke | WHUUM/ Pemba | Procurement and Supply | Stashahada | Miaka 2 | Zanzibar College of Business |
| 23 | Khadija Ali Juma | Mke | WHUUM/ Pemba | Human R.Management | Stashahada | Miaka 2 | Dar College of Busines |
| 24 | Khamis Ali Juma | Mme | WHUUM/ Pemba | Tourism Management | Shahada ya 1 | Miaka 3 | SUZA |
| 25 | Hamzia Khamis Khalfan | Mke | WHUUM/ Pemba | Human R.Management | Stashahada | Miaka 2 | Dar College of Busines |
| 26 | Mwajuma Hija Kipenda | Mke | WHUUM/ Pemba | Human R.Management | Stashahada | Miaka 2 | Dar College of Busines |
| 27 | Zaituni Mwalim Suleiman | Mke | Idara ya Habari Maelezo | Record Management | Stashahada | Miaka 2 | ICPS |
| 28 | Hassan Ameri Vuai | Mme | Kamisheni ya Utalii | Uongozi wa Biashara | Shahada 2 | Miaka 2 | Tunguu |
| 29 | Aviwa Issa Makame | Mke | Kamisheni ya Utalii | Sheria | Shahada 2 | Miaka 2 | Tunguu |
| 30 | Ali Jaku Ali | Mme | Kamisheni ya Utalii | Uongozi wa Utalii | Shahada 2 | Miaka 2 | Tunguu |
| 31 | Khalfan Mohammed Ali | Me | Kamisheni ya Utalii | Uongozi wa Utalii | Shahada 1 | Miaka 3 | Sokoine Mororgoro |
| 32 | Mwanaidi Moh´d Ali | Mke | Kamisheni ya Utalii | Uongozi | Shahada 1 | Miaka 3 | Chuo Kikuu |
| 33 | Sharifa Mzee Rajab | Mke | Kamisheni ya Utalii | Uhasibu | Stashahada | Miaka 2 | Chuo cha KIU |
| 34 | Hamad Amin Ali | Mme | Kamisheni ya Utalii | Uongozi | Shahada1 | Miaka 3 | Chuo cha KIU |
| 35 | Rifai | Mme | Kamisheni ya Utalii | Utalii | Shahada 1 | Miaka 3 | Sokoine Morogoro |
| 36 | Hassan Hannas | Mume | Kamisheni ya Utalii | Utalii | Shahada 1 | Miaka 3 | Sokoine Morogoro |
| 37 | Asha Haji Khamis | Mke | Kamisheni ya Utalii | Utalii | Stashahada | Miaka 2 | Chuo cha Azania |
| 38 | Khadija Haji Mussa | Mke | Kamisheni ya Utalii. | IT | Stashahada | Miaka 2 | ICPS |
| 39 | Mvita [illegible] | Mke | Kamisheni ya [illegible] | IT | Stashahada | Miaka 2 | ICPS |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 40 | Kei Moh'd Abdalla | Mke | Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Tourism Management &Marketing | Shahada ya 1 | Miaka 3 | SUZA |
| 41 | Ibrahim Ali Sharif | Mme | Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Tourism Management &Marketin | Shahada ya 1 | Miaka 3 | SUZA |
| 42 | Zuhura Ali Juma | Mke | Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Tourism Management &Marketin | Shahada ya 1 | Miaka 3 | SUZA |
| 43 | Faida Ramadhan Senga | Mke | Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Tourism Management &Marketin | Shahada ya 1 | Miaka 3 | SUZA |
| 44 | Halima Juma Omar | Mke | Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Project Planning &Management | Shahada ya 2 | Miaka 2 | Kabale Uganda |
| 45 | Amour Salim Said | Mme | Kamisheni ya U/Michezo BAKIZA | Fasihi ya Kiswahili | Shahada 2 | Miaka 2 | Chuo kikuu cha Dodoma |
| 46 | Mwanaidi Fundi Ameir | Mke | Kamisheni ya U/Michezo BAKIZA | Record Management | Stashahada | Miaka 2 | IPA |
| 47 | Hawa Ibrahim Saburi | Mke | Kamisheni ya U/Michezo BAKIZA | ICT with Account | Stashahada | Miaka 2 | ZIToD |
| 48 | Jamhuri Ameir Simai | Mme | Shirika la Magazeti ya Serikali | Udereva | Stashahada | Mwaka 1 | Nationa Institute Transport |
| 49 | Mwanaiman Rashid Ismail | Mke | Shirika la Magazeti ya Serikali | Bessiness Information Technology | Stashahada | Miaka 2 | IPA |
| 50 | Hamida Daudi Khalid | Mke | Chuo cha Uandishi wa Habari | Cultural Management and Tourism | Stashahada | Miaka 2 | SUZA |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 51 | Rukia Abdulsalam | Mke | Chuo cha Uandishi wa Habari | Uhasibu | Shahada 2 | Miaka 2 | Mzumbe University |
| 52 | Nangi Abel Mwampaja | Mke | Chuo cha Uandishi wa Habari | Uandishi wa Habari | Shahada 1 | Miaka 3 | Uganda Pentecost al University |
| 53 | Haji Khatibu Haji | Mum e | ZBC | Rasimali Watu | Shahada 1 | Miaka 3 | KIU University |
| 54 | Fatma Masururu Saadat | Mke | ZBC | Teknolojia ya Habari | Shahada 1 | Miaka 3 | Open University Dsm |
| 55 | Ashura Ali Omar | Mke | ZBC | Uongozi wa Biashara | Shahada 1 | Miaka 3 | Open University Zanzibar |
| 56 | Haji Khatibu | Mum | ZBC | Rasimali | Shahada 1 | Miaka 3 | KIU |
| 57 | Fatma Masururu Saadat | Mke | ZBC | Teknolojia ya Habari | Shahada 1 | Miaka 3 | Open University DSM |
| 58 | Adam Suleiman Makame | | ZBC | Teknolojia ya Habari | Shahada 1 | Miaka 3 | SUZA |
| 59 | Fatma Abdalla | Mke | ZBC | Computer | Stashahada | Miaka 2 | SUZA |
| 60 | Mwanaidi | Mke | ZBC | Computer | Stashahada | Miaka 2 | SUZA |
| 61 | Hamida Daudi Khalid | Mke | Chuo cha Uandishi wa Habari | Cultural Manageme nt and Tourism | Stashahada | Miaka 2 | SUZA |
| 62 | Rukia Abdulsalam | Mke | Chuo cha Uandishi wa Habari | Uhasibu | Shahada 2 | Miaka 2 | Mzumbe University |
| 63 | Nangi Abel Mwampaja | Mke | Chuo cha Uandishi wa Habari | Uandishi wa Habari | Shahada 1 | Miaka 3 | Uganda Pentecost al University |

**KIAMBATANISHO NAMBA 3: KAZI ZA SANAA ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA 2014-2015**

| S/NO | **AINA YA KAZI ZILIZO KAGULIWA** | **ZILIZO KUBALIWA** | **ZILIZO KATALIWA** | **ZILIZO REKEB ISHWA** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Filamu kutoka nje | 297 | 3 | - | 300 |
| 2. | Filamu za ndani | 49 | 4 | 22 | 75 |
| 3. | Mashairi | 9 | 1 | 2 | 12 |
| 4. | Rasimu za michezo ya maigizo (*Script*) | 8 | - | 2 | 8 |
| 5. | Ngojera | 8 | 1 | 2 | 9 |
| | **JUMLA KUU** | **371** | **9** | **28** | **404** |

**KIAMBATANISHO NAMBA 4: MASHINDANO MBALI MBALI AMBAYO TIMU ZA ZANZIBAR ZILISHIRIKI.**

| **S/ N O.** | **CHAMA** | **MASHINDANO** | **PAHALA** | **MAELEZO** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Chama cha Netiboli | Mashindano ya klabu bingwa ya Afrika Mashariki ya mchezo wa Netiboli | Zanzibar, Machi, 2015 | Timu ya Polisi ilipata ushindi wa kwanza, JKU mshindi wa pili na KVZ mshindi wa tatu kwa upande wa wanaume. |
| | | Mashindano ya ligi kuu ya Zanzibar | Zanzibar, Novemba, 2014 | Vilabu mbali mbali vilishiriki |
| 2. | Chama cha Mchezo wa Kuogelea | Mashindano ya klabu bingwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Dar-es-salaam, Machi, 2015 | Timu ya KMKM ilipata medali 2 za shaba, na 2 za Fedha |
| | | Mashindano ya uteuzi wa timu ya Taifa ya kuogelea ya Tanzania | Dar es salaam, Machi, 2015 | Timu ya Taifa yenye sura ya Muungano imeundwa |
| | | Master Swimming Competition | Dar-es-salaam, Aprili, 2015 | Timu ya KMKM ilipata medali 7 za dhahabu, medali 2 za shaba, na 4 za Fedha |
| 3. | Chama cha Mpira wa Wavu | Mashindano ya Tanzania ya Mpira wa Wavu wa Ufukweni (Beach Volleyball) | Dar-es-salaam, Januari, 2015 | Mshindi wa kwanza na mshindi wa tatu. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mashindano ya Mpira wa Wavu wa Ufukweni ya Afrika Mashariki na kati (Beach Volleyball) | Dar-es-salaam, Febuari, 2015 | Timu ya Zanzibar ilitolewa nusu fainali |
| | | Kombe la Mapinduzi | Zanzibar, Januari, 2015 | Timu ya Umiseta ilipata mshindi wa kwanza |
| | | Mashindano ya ligi kuu ya Zanzibar | Pemba, Novemba, 2015 | Chuoni walipata mshindi wa kwanza kwa wanaume na Wete stars kwa wanawake |
| 4. | *Special Olympic of Zanzibar (SOZ)* | Mashindano ya kitaifa ya Riadha na Mpira wa Miguu | Kibaha,April, 2014 | Mshindi wa kwanza kwa upande wa mpira wa miguu na Kwa upande wa Riadha walipata medali 9 za dhahabu na 5 za silva |
| 5. | Chama cha Mpira wa Vikapu | Mashindano ya Karume Cup | Zanzibar Novemba, 2015 | Vilabu mbali mbali vilishiriki |
| | | Mashindano ya Vijana chini ya umri wa miaka 20, 15 na 12 | Zanzibar, Machi, 2015 | Vilabu mbali mbali vya vijana vilishiriki |
| 6. | Chama cha JUDO | Mashindano ya Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki | Moshi, Febuari, 2015 | Zanzibar ilipata mshindi wa pili kwa kupata Medali 2 za dhahabu, 1 Silva na 3 shaba. |
| | | Mashindano ya 13 ya "Zanzibar Budokan JUDO CUP" | Zanzibar, Disemba, 2014 | Vilabu 9 vilishiriki |
| 7. | Chama cha Riadha | Mashindano ya Klabu Bingwa ya Zanzibar | Zanzibar,July, 2014 | KMKM walipata mshindi wa kwanza |
| | | Mashindano ya Wilaya zote za Zanzibar | Zanzibar, Disemba, 2014 | Wilaya ya Mjini ilipata mshindi wa kwanza |
| | | Mashindano ya Klabu Bingwa ya Tanzania (Mikoa) | Dar-es-salaam, 2014 | Mkoa wa Mjini Magharib ilipata Ubingwa |
| | | Mashindano ya Afrika | Moroco, 2014 | Zanzibar haikufanya vizuri |
| 8. | *Zanzibar Weight lifting Association* | Mashindano ya Common Wealth | GlasGlow, July-Aug, 2014 | Zanzibar imeingia katika kumi bora |
| 9. | Chama cha Mpira wa Miguu | Kombe la Shirikisho | Machi | Timu ya polisi katika mzunguko wa kwanza |
| | | Mashindano ya Klabu Bingwa ya Afrika | Zanzibar, Februari, 2015 | KMKM walitoa katika mzunguko wa kwanza |
| 10. | Chama | Mashindano ya | Uganda, 2014 | Timu ya wanaume ilipata ushindi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | cha Mpira wa Mikono | Kombe la Challengi | | wanne na wanawake ushindi wa 5 |
| 11. | *Zanzibar Association for Disable* | Mashindano ya kutafuta viwango | Dar es salaam, Julai, 2014 | Timu ya Taifa yenye sura ya Muungano imeundwa |
| 12. | Chama cha Mchezo wa Viziwi | Mashindano ya Klabu Bingwa ya Zanzibar | Zanzibar, Oktoba, 2014 | |
| 13. | Chama cha Baskeli | Mashindano ya Taifa ya Baskeli | Zanzibar, Novemba, 2014 | Vilabu mbali mbali vilishiriki |
| 14. | Chama cha Mchezo wa Vinyoya | Mashindano ya Klabu Bingwa ya Zanzibar | Pemba, Novemba, 2014 | Vilabu mbali mbali vilishiriki |
| 15. | *Zanzibar Table Tennis Association* | Mashindano ya Klabu Bingwa ya Zanzibar | Zanzibar, Novemba, 2014 | |
| 16. | Chama cha Mchezo wa Karata | Mashindano maalum ya mchezo wa karata | Zanzibar, Machi, 2015 | Yamefanyika Unguja na Pemba. Washindi wa 4 kutoka Unguja na wa 4 kutoka Pemba wamepatikana |
| | Chama cha Mchezo wa Bao | Mashindano maalum ya mchezo wa Bao | Zanzibar, Machi, 2015 | Yamefanyika Unguja na Pemba. Washindi wa 4 kutoka Unguja na wa 4 kutoka Pemba wamepatikana |

## KIAMBATANISHO NAMBA 5: MAFUNZO MBALI MBALI KWA VYAMA VYA MICHEZO

| S.NO. | CHAMA | MAFUNZO | PAHALA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | *Zanzibar Weight lifting Association* | Mafunzo ya Ualimu na Uamuzi | Nigeria, Julai,2014 | Viongozi 2 walishiriki |
| | | Mafunzo ya Uwalimu na Uamuzi | Uturuki, Agosti, 2014 | Kiongozi 1 alishiriki |
| **2.** | Chama cha Mchezo wa Kuogelea | Mafunzo ya Ukocha wa vijana (Youth Program ) | Qatar, 2015 | Mwalimu 1 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | katika ngazi ya cheti | | |
| **3.** | Chama cha Mpira wa Vikapu | Mafunzo ya awali ya uamuzi | Pemba, Machi, 2015 | Waamuzi 20 walishiriki |
| **4.** | Chama cha JUDO | International Judo coaching course | Japan, Nov-Desemba, 2014 | Mwalimu 1 alishiriki |
| **5.** | Chama cha Mpira wa Miguu | Mafunzo ya msingi ya tatu ya Makocha wa vijana (Junior na Senior) | Oktoba, 2014 | Washiriki 60 kutoka Zanzibar |

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Spika:** Tunakushukuru sana Mhe. Waziri umeweza kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yako kwa muda wa dakika 50, tunakushukuru sana. Muda uliobaki ni mchache mno haumuwezeshi Mwenyekiti kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati.

Waheshimiwa Wajumbe sasa nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa mashirikiano makubwa, lakini kuna hojaji imetolewa, yaani *questionnire*, kuhusiana na *assessment* ya mradi wetu wa *LSP*. Tunatakiwa tuijaze na tuwakabidhi watendaji ili wairejeshe kwa watendaji wakuu wanaohusika na mradi wetu huo.

Waheshimiwa Wajumbe basi baada ya hayo machache sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

*(Saa 12:56 Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

*Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) Alikalia Kiti.*

**Mhe. Mwenyekiti:** Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Karibu Mwenyekiti!

**Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: (Mwenyekiti wa Kamati wa Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari):** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kwa mara nyengine tena kukutana hapa katika Mkutano huu wa Bajeti ambao huenda ikawa ni wa mwisho katika Baraza hili la Nane la Wawakilishi.

Aidha, namshukuru tena Muumba kwa kuijaalia nchi yetu kuendelea kuwa katika hali ya amani, utulivu, usalama na mashirikiano, mambo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Pili napenda kuendeleza shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha mchango wangu kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Mifugo, Utalii,Uwezeshaji na Habari na pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bumbwini, kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kujitahidi kutekeleza malengo na majukumu yao kwa bidii kubwa katika kipindi cha mwaka 2014/2015, pia kwa mashirikiano yao mazuri waliyotupa wakati Kamati ilipokua ikitekeleza kazi zake za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 96 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ilipata fursa ya kulifikiria kwa kulifanyia uchambuzi wa kina fungu la makadirio ya bajeti ya Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo nachukua nafasi hii kukuarifu kuwa kazi hiyo tuliifanya na leo hii tupo hapa kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu taarifa ya kazi tuliyoifanya kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 93 (9) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Utangulizi huo napenda sasa nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kamati ya Mifugo, Utalii,Uwezeshaji na Habari kuhusu makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kama ifuatavyo:-

**SEKTA YA UTALII**

Mhe. Mwenyekiti, hakuna asiyeelewa kwamba Utalii ni Sekta kiongozi inayochangia pato la Taifa hasa baada ya kupungua kwa soko la Karafuu Duniani. Tafiti zinaonesha kuwa Sekta hii imekuwa ikichangia zaidi ya asilimia 25 ya pato

la Taifa na asilimia 80 fedha za kigeni. Kwa mantiki hiyo basi, Serikali haina budi kuhakikisha kwamba inaweka kasma ya kutosha katika kuuendeleza utalii hapa nchini, ikiwemo bajeti ya kuutangaza utalii. Kamati yangu inaamini kwamba utalii unaweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa endapo Serikali itazidi kuutangaza ndani na nnje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono Programu ya Utangazaji na uhamasishaji wa Utalii, ambayo imetengewa shilingi 304,500,000 kwa lengo la kuongeza tija katika sekta hii ambapo matokea yake yanalenga kuifanya Zanzibar kuwa kituo bora cha Utalii. Kamati inaliomba Baraza kuidhinisha fedha zote zilizoombwa kwa ajili ya programu hii, ili iweze kutekeleza kazi zake kama ilivyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka unaomalizika yaani 2014/2015 Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo iliidhinishiwa Jumla ya shilingi 5,595,375,000 kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya maabara ya Utalii. Kamati yangu kwa unyonge inaliarifu Baraza lako Tukufu kwamba hadi kufikia Aprili 2015 Wizara imeingiziwa shilingi 476,745,730 sawa na asilimia 8.5 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

Kwa bahati mbaya Programu hii inaripotiwa kucherewa kuanza kama ilivyopangwa kwa madai ya kwamba baadhi ya Taasisi zinazohusika na maabara hiyo kucherewa kuwasilisha shughuli walizopanga kutekeleza. Aidha, kuchelewa kuanza kwa Programu hii pia kunatokana na baadhi ya tasisi kuwasilisha bajeti ambazo hazikuwa halisia. Kamati inaiomba serikali kupitia wizara hii kujipanga vizuri ili kuhakikisha kwamba mipango kama hii inafanyiwa utafiti wa kina ili wakati wa utekelezaji wake, matatizo kama haya yaweze kuepukika.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine litalotaka kufanyiwa kazi na wizara hii ni kuimarisha Utalii wa ndani kwani nchi yetu imebahatika kuwa na maeneo mengi ambayo yakiendelezwa na kuimarisha yataongeza vivutio vya utalii tulivyo nanvyo kama vile magofu, mapango na chumba cha chini kwa chini kule Makangale. Utafiti unaonyesha kua nchi nyingi duniani zimekukua zikifaidika na mapato yanayotokana na Utalii wa ndani .

Mhe. Mwenyekiti, Hotuba ya Mhe. Waziri, inaonesha kwamba katika utekelezaji wa wizara kwa mwaka 2014/2015 Kamisheni ya Utalii imefanikiwa kufanya utafiti wa vituo vipya vya Utalii kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii wanaiingia nchini, hapa Kamati inashauri Utafiti huo ufanyiwe kazi kwa haraka huku mbinu nyengine zizidi kufikiriwa katika suala zima la kuongeza idadi ya watalii na mapato yanayotokana na sekta hii. Aidha, wananchi nao wahamasishwe kuthamini

utalii wetu na kutembelea maeneo ya kitalii na kuondokana na ile dhana iliyojengeka kwamba mtalii lazima yule anayetoka nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kuimarisha na kukiendeleza chuo chetu cha Maendeleo ya Utalii, ili kisaidie kuwaandaa vijana wetu na hatimae waweze kuikabili vyema sekta ya utalii hapa nchini. Kamati yangu hairidhiki kabisa na fedha zinazotengwa kwa ajili ya uendeshwaji wa chuo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu sahihi za watalii wanaingia nchini bado ni tatizo linaloripotiwa na Kamisheni ya Utalii, hivyo tunaiomba Wizara ishirikiane na Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu na Wizara ya Fedha ili waandae taratibu maalum za upatikanaji wa takwimu sahihi za wageni wanaoingia nchini.

Aidha, pamoja na kuipongeza Serikali kwa juhudi kubwa za kuimarisha huduma za kijamii katika maeneo mbali mbali na kwa kweli imefanikiwa sana katika suala hili, hata hivyo tunaisisitiza Serikali kuzidi kuimarisha miundombinu hasa barabara , umeme na maji katika sehemu za kitalii ili kuondosha usumbufu hasa barabara zinazounganisha barabara kuu na hoteli za Kitalii.

Vile vile, Kamati inaipongeza Wizara Kupitia Kamisheni ya Utalii kwa kusambambaza elimu ya Utalii mijini na vijijini, Kamisheni imeripoti kwamba ilifika Skuli ya Umbuji kwa ajili hiyo, hili ni suala zuri , lakini Kamati inaitaka Kamisheni hiyo kuendelea kutoa elimu hiyo katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba huku ikizishirikisha kikamilifu kamati za Utalii za Shehia na Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba sekta ya Utalii inawanufaisha wananchi wengi, serikali ilianzisha dhana ya "Utalii kwa wote" wenye lengo la kuwashirikisha zaidi wananchi katika harakati za utalii ili kuweza kujiongezea kipato. Pamoja na mafanikio hayo, kumekuwa na changamoto mbali mbali wanazokutana nazo wananchi katika uhudumiaji wa sekta ya utalii hasa wale wanaojihusisha na usambazaji wa bidhaa katika nyumba za kulala wageni, mikahawa na nyenginezo. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwepo kwa baadhi ya wawekezaji wasiokuwa waaminifu kwa wananchi wanaotowa huduma katika sehemu hizo.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine ni ukosefu wa mikataba rasmi baina yao na wenye mahoteli, ukosefu wa mawasiliano ya moja kwa moja kati yao na uongozi wa hoteli husika, na ukosefu wa jumuiya imara inayosimamia shughuli zao. Katika kuliondosha tatizo hili Kamati yangu inaishauri Wizara kuwasajili kihalali watowa huduma hao, ili wafanyekazi zao kwa wepesi zaidi. Aidha tunawashauri watoa huduma hao wakati wa utekelezaji wa kazi zao watumie

mikataba badala ya kutegemea risiti tu au kuaminiana kwa maneno kitu ambacho hupelekea kupoteza haki zao. Aidha tunawataka kuwashirikisha kamisheni ya Utalii wakati wa uingiaji wa makubaliano ya kibiashara na wawekezaji.

**SEKTA YA HABARI**

Mhe. Mwenyekiti, Kama tulivyowahi kusema katika Ripoti zetu za nyuma, Kamati inahisi kwamba Serikali ilikurupuka kuazisha Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC)* ambalo kwa sasa wananchi wanahisi litaitia hasara serikali. Tukiangalia Ripoti mbali mbali za Wizara, tunaona kwamba fedha za Uendeshaji wa Shirika hili ni nyingi mno ukilinganisha na makusanyo ya Mapato yanayozalishwa. Aidha, upatikanaji wa fedha za uendeshaji nao ni wa kusuwa sua. Tunaiomba serikali ijitathmini upya juu ya uanzishwaji wa Shirika hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa lengo la serikali ni kuilea (*ZBC)* hatimaye ijiendeshe na ijitegemee, suala la ukusanyaji wa mapato nalo ni muhimu. Bado taasisi nyingi za serikali hazilipii matangazo yao, suala hili linarejesha nyuma ukusanyi wa mapato na hivyo kushindwa kujiendesha kama Shirika, tunaziomba taasisi hizo zilipie matangazo yao ili lengo la kuanzishwa kwa Shirika hilo liweze kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna taarafa kwamba Afisi ya Baraza la Wawakilishi imeshafanya maandalizi ya kulipia matangazo ya Mikutano ya Baraza la Wawakilishi kuanzia Mkutano ujao. Hii ni habari njema na ya faraja, Kamati yangu inalipongeza Baraza la Wawakilishi kwa uamuzi huo na kuziomba taasisi nyengine kuwa na mikakati kama hiyo ya kulipia matangazo yao.

Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inashari kwamba kabla ya malipo hayo kuingizwa moja kwa moja katika akauti za *ZBC*, kuwe na mpango maalum wa kutenga fedha hizo na kuwalipa hapa hapa wafanyakazi wao wanaokuja hapa Barazani kwa ajili ya kurikodi Mikutano yetu ili kuondosha ufumbufu unaoweza kutokea huko Shirikani.

Mhe. Mwenyekiti, wakati tunasubiri utekelezaji wa mpango huo mpya , Kamati yangu, kwa uchungu inalazimika kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba hadi tarehe 10 mwezi huu wa sita, wafanyakazi hawa *ZBC* hawajalipwa posho zao za kazi kubwa na nzito wanayoifanya ya kurikodi na kurusha vikao vya Baraza hili tokea Mkutano wa 17 wa Baraza hili na Nane. Kwa kweli suala hili ni la kusikitisha sana na kwa kweli hatuwatendei haki wafanyakazi hawa.

Mhe. Mwenyekiti, iwapo wafanyakazi hawa wamelipya posho hizo basi ni kwa ajili ya kutunyamazisha sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili tuweze kuwapitishia Bajeti hii, lakini si kwa ajili ya kuwajali wafanyakazi hawa.

**Shirika la Magazeti ya Serikali**

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Magazeti lina changamoto kubwa ya kutokuwa na mtambo wake wa kuchapisha magazeti na kupelekea magazeti kuchapishwa Tanzania Bara, hali ambayo huongeza gharama kubwa kwa Shirika hilo. Kwa muda mrefu sasa kamati yangu na wajumbe wa Baraza lako wamekuwa wakielezea umuhimu wa kuwa na Mtambo huu ili kuokoa fedha nyingi zinazotumika kwa kuchapisha magezeti huko Tanzania Bara. lakini mpaka sasa bado hatujajua suala hili limefikia wapi? Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuiingiza Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Shirika pamoja na ununuzi wa Mtambo wa kuchapishia magazeti ya rangi kuingizwa katika Bajeti kuu ya serikali.

**Chuo Cha Uandishi wa Habari**

Mhe.Mwenyekiti, pamoja na kwamba Chuo cha Uandishi wa Habari hivi sasa kiko katika harakati za ujenzi wa Ofisi zake katika eneo la Kilimani, chuo hicho kinakabiliwa na Changamoto kadhaa ikiwemo uhaba wa vifaa unaotokana na kasma ndogo inayotengewa chuo hicho. Changamoto hii ya kibajeti inaweza kupungua baada ya Chuo hicho kukamilisha ujenzi wa Ofisi zake kwa wakati, na hatimae kitaweza kuchukuwa wanafunzi wengi na pia kutanua wigo wake kwa kuongeza kozi mbali mbali na hivyo kuwaongezea mapato zaidi. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mipango ya kukamilisha ujenzi huo inatekelezwa kama ilivyokusudia kwa kukipatia fedha za kutosha chuo hicho ili ujenzi huo umalizike kwa wakati uliopangwa.

**Kampuni ya Uunganishaji Maudhui Zanzibar *Multiplex* (*ZMUX*)**

Mhe. Mwenyekiti, Suala la Kampuni ya *Zanzibar Multiplex ZMUX* bado halizungumzwi vizuri ndani ya jamii. Kuna wasiwasi kwamba lengo la kuanzishwa kwa Kampuni hii halijafikiwa, ikizingatiwa kwamba *ZMUX* imeanzishwa kama Kampuni ambayo ipo ndani ya Wizara ya Habari, lakini bado haijakuwa na vyanzo vya kukusanya mapato na kujiendesha yenyewe hivyo kuibebesha mzigo mkubwa Serikali. Ingawa Wizara iliunda Kamati kwa ajili ya kutafiti kuendelea kuwepo kwa *ZMUX* au la, lakini hadi muda huu hatujapata matokeo ya utafiti huo. Kamati inahisi kwamba ipo haja kwa Kampuni hii kuiondoa Serikalini na kuifanya ifanye kazi zake chini ya mwamvuli wa *ZBC*.

Mhe. Mwenyekiti, Kitabu cha Mheshimiwa Waziri kinaonesha kwamba katika mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara imepanga kutekeleza programu 5 na programu ndogo 10. Kwa Kuwa utekelezaji wa Programu hizi unafuata mfumo mpya wa Kibajeti, *PBB* tunaamini kwamba Wizara itakuwa na ufanisi mkubwa katika kutatua changamoto nyingi zinazoikabili wizara kwa uwazi na ufanisi zaidi

katika utoaji wa huduma kwa kuwa Bajeti hiyo imezingatia matokeo na kuongeza ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, Programu za Wizara hii ni pamoja na

1. Maendeleo ya habari na utangazaji,
2. Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo, yaani utangazaji na uhamasishaji wa utalii na kuratibu na kusimamia maendeleo ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba kufanikiwa kwa programu hizi ambazo zimeombewa jumla ya shilingi za Kitanzania milioni kumi na tatu, hamsini na mbili milioni na laki mbili. Sekta za habari, utalii na utamaduni zitawasaidia wananchi katika kuimarisha maendeleo yao ya kijamii na kiuchumi. Hivyo, Kamati inaliomba Baraza lako Tukufu kwa kauli moja kuidhinisha fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya programu hizo ili Wizara iweze kutekeleze vyema programu hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijakamilisha hotuba yangu ninapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano yao makubwa walionesha wakati wote ambapo Kamati yetu imefanya kazi ya kupitia bajeti ya Wizara hii pamoja na kazi za ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuihoji Serikali na kutoa maoni yao kwa lengo la kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji kwa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwatambua Wajumbe hao wa Kamati kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Abdalla Mohammed Ali | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe.Asha Bakari Makame | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mussa Ali Hassan | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Kazija Khamis Kona | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Asaa Othman Hamad | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali | - | Mjumbe |

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa naomba niwashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Himid Haji Choko na Salum Khamis Rashid kwa kuratibu vyema kazi za Kamati hii wakati Kamati ikipitia bajeti hii na kazi zote za Kamati kwa kipindi cha uhai wa Kamati. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda sasa kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu na pia ninapenda kukushukuru kwa mara nyengine tena wewe binafsi kwa kuniruhusu kutoa maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kutamka kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini ninaiunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. (*Makofi*)

Aidha, ninawaomba Wajumbe wote wachangie na kuunga mkono makadirio ya bajeti ya Wizara hii kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu na malengo ya Wizara waliyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati. Sasa ni nafasi ya Mhe. Saleh Nassor Juma na baadae Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote ninapenda nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na hatimae kutupa uwezo na afya njema ya kuweza kuondoka katika maeneo yetu kule tunakoishi hadi hapa, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, ninadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kuchangia hoja iliopo mbele yetu. Kwa mnasaba huo ninasema ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nianze katika hoja iliyoopo mbele yetu kwa maana hii ya Hotuba ya Mhe. Waziri, Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Hotuba ya Mhe. Waziri kwanza nimpongeze sana kwa kuweza kututayarishia hotuba hii na kuisoma kwa utulivu mkubwa, kiasi ambacho hata ambaye hasikii vizuri basi ameisikia na kuifahamu. Ninasema Mhe. Waziri ahsante sana. Ama kweli dhahabu ni dhahabu hata uitie kwenye tope basi haipotezi thamani yake. Kwa hivyo Mhe.Waziri ahsante sana kabisa kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika sekta ya habari. Sekta hii kama tulivyoelezwa katika hiki kitabu ina taasisi tano. Taasisi zenyewe ni pamoja na Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti la Serikali, Tume ya Utangazaji pamoja na Shirika la Utangazaji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwanza niende moja kwa moja katika Shirika hili la Utangazaji. Jukumu kubwa la Shirika hili kwanza ni kuhabarisha; yaani kutupa habari na pili kutuburudisha. Kwa kweli Shirika hili linatoa burudani nzuri sana, mambo ya taraabu, mambo haya ya Bongo fleva, mambo ya taraabu asilia yale, yote tunapata kupitia hili Shirika. Kwa hivyo ni shirika muhimu sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Shirika hili la *ZBC* ni mdomo wa Serikali, kwa upande mwengine tunasema ni kiunganishi baina ya Serikali na raia wake. Kwa mnasaba huo, shirika watumishi wake wanatakiwa wawe makini sana katika kufanya kazi zao na wawezeshwe.

Kuna habari ambazo zinatokea katika nchi na zinatolewa na Serikali, zinatakiwa kutoka Makao Makuu ya Serikali mpaka vijijini zifike kwa wakati. Inasikitisha sana kwamba hawa watu wana mazingira magumu sana katika kufanya kazi zao, kiasi ambacho hivi sasa inasikitisha mno kuona kwamba *ZBC-TV*; televisheni ya mwanzo ya rangi katika ukanda huu wa Afrika, imeanzishwa vizuri tangu zamani hapa enzi za A.A. Karume. Wakati huo *TV* ndugu zetu wa damu hawana kabisa kabisa, sisi tukawa na TV ya rangi hapa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, wakati tunaanzisha *TV* hii ilikuwa ina umakini mkubwa sana katika kufanya kazi. Mimi wakati *TV* hii inaanzishwa tulikuwa tunajenga meli ya Zanzibar kule Japan, meli ipo dakhili ya Pemba pale, Vitongoji karibu maili kumi kutoka pale Chake Chake mjini. Lakini nilikuwa ninaweza kuona meli inachongwa Japan. Kutokana na jinsi ya wafanyakazi na Serikali ilivyokuwa inajali hii taasisi kwa enzi zile.

Kuanzia juzi juzi, sasa hivi inasikitisha kwamba chombo chetu hiki hakipo makini, hakiwezeshwi. Juzi juzi tulikuwa tunaambiwa tunatengenezewa meli nchi ya Korea, anakuja Waziri hapa anatwambia tunaweka mkuku. Huu ni mwaka wa tatu, meli inawekwa mkuku hatuoni, wakati zamani tangu mchoro unachorwa ule wa meli tunaona. Sisi kupitia chombo chetu kwa siku zile inaitwa *TVZ*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana pamoja na kwamba mitambo ya siku zile ilikuwa ya *analogue*. Lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyokuwa ikiongozwa na Mzee Karume siku zile walimudu kuihudumia mitambo ile kila *step* ya meli ile ikawa tunaona. Hapa Waziri wa Fedha tunamuomba jamani basi tuonesheni angalau kidogo, akatwambia mutaona, mutaona hadi leo hii. Kwa hivyo inaonesha dhahiri kwamba hawawezeshwi hawa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefanya tafiti katika nchi nyingi za Afrika na hata hizi za Ulaya hizi, bajeti ya "*Wizaratul Akhbary*" inakuwa karibu asilimia 30 au 25

hivi, lakini sisi sidhani kama tunaifikisha angalau bajeti asilimia 10 bajeti ya Wizara muhimu kama hii. Hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, unaambiwa nilitembelea nchi moja sitaki niitaje, katika chombo cha habari wana-*dictate* taarifa, yaani ikitokea tu taarifa hata iwe *mile* mia moja kutoka kwenye chombo cha *mile* mia mbili, tatu au kilomita ngapi, zinakuwa *dictated*, pale ni kupeleka *helicopter* muandishi anakwenda anatoa, habari mpasuko zinapatikana kwa wakati, lakini katika chombo hiki chetu sisi habari mpasuko tunashindwa. Chombo cha Serikali kinashindwa mpaka na *ZENJ FM,* ni aibu! (*Makofi*)

Mimi ninaona huu ni wakati wa sayansi na teknolojia, hiki chombo bajeti ipanuliwe, wawezeshwe hawa. Hawa vijana wanafanya kazi ya ziada. Wewe mchana wa kutwa kazi yao ni kutumurika tu, sijui hata wana nini, yaani wananung'unika hawapati mafao.

Kila mtu anaona hivi Baraza linavyoendelea kutokana na kazi za hawa vijana maskini. Lakini juzi juzi walikuwa wanasikitisha, sijui mara hii mambo yao yamewekwa sawa au vipi, lakini inasikitisha sana kwa mfano, hebu tupewe uzoefu wa kule Pemba.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wa *ZBC* pale Pemba, lile posho la Mhe. Rais la mwaka 2013, sijui ilikuwa ni shilingi ishirini na tano elfu, kwa taarifa tulizozipata walipewa miezi kumi tu, baadae mpaka sasa hivi wamekatishiwa wananung'unika wanateketea kwa njaa, elfu ishirini kwa mfanyakazi wa Serikali ni nyingi sana.

Hebu fuatilieni taarifa za wafanyakazi wa *ZBC* kule Pemba wanavyopata shida, ni tatizo. Kuna wafanyakazi ambao wamemaliza mafunzo *FTC, diploma level, first degree* wapo pale, wamesharekebishiwa mishahara hivi juzi lakini *areas* zao karibuni za mwaka mzima au miaka miwili hawajalipwa, huu ni uhaini, hawapati moyo.

Mimi ninadhani katika hili Mhe. Mwenyekiti, tuwe makini sana. Huu ni mdomo wa Serikali na *middle media* ya *information* baina ya Serikali na sisi raia, tujitahidi sana kuwawezesha, bajeti yao ipanuliwe, wawezeshwe kupata mishahara kidogo inayolingana na kazi zao. Saa ishirini wapo katika vioo hawa, wanakwenda katika mikutano ya hadhara hawa ya vyama tofauti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hawa vijana na karibu ndiyo kampeni za siasa zinaanza hizo. Kuna muandishi aliuwawa Iringa kule mwaka juzi, kuna muandishi mmoja aliuliwa katika mkutano wa hadhara. Hawa wanapewa *risk allowance*

wanaposhiriki katika kazi zile, vyama vyengine hatujui vitakuwa na ustaarabu kiasi gani na wao wanakwenda kuchukua taarifa hawa.

Mimi ninadhani hawa vijana pamoja na kwamba wakati mwengine wanakuwa *bias*, taarifa nyengine wanazitoa hivi ndivyo, sivyo vya vyama vyengine, eeh! wasiwe *bias* bwana sisi tunatetea humu na taarifa na zetu tukifanya mikutano vile vile muitoe vizuri, musituoneshe kichwani tu, mutuoneshe na ile *audience* yote ile iliopo.

Mhe.Waziri chombo chako cha *ZBC* kipo *bias* kinakuonesha kwenye kichwa tu kwenye mikutano ya hadhara, na umati uliopo pale. Hii pesa wanayopokea hawa mujue kama ni pesa ya walipa kodi, nikiwemo mimi ninaye-*conduct public rally* pale Udusini na Umangani.

Mhe. Waziri, ujitahidi sana katika hili kurekebisha hiki chombo ili kifanye kazi kwa mujibu wa sheria. Hawa vijana wakija katika mikutano ya hadhara muangalie vizuri, vyama vyengine vina fujo wanaweza wakaja wakapata hasara, vifaa vyao vikaja vikaharibiwa, angalau muwape *risk allowance* na kampeni ndiyo zinaanza karibuni. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye hii hii *ZBC*. Ni tatizo gani hasa kwamba *ZBC TV* bado kule Pemba haisikilikani vizuri, hata redio, lakini bora hata redio inasikilikana, inanguruma sana cheee! *ZBC* radio ina macharaza mengi, mbona ukenda kwenye hawa *Al-Istiqama radio* ambazo ni redio za juzi tu sauti safi kabisa, ukenda kwenye *ZENJ FM* sauti safi kabisa. *Hit radio* ni sauti safi kabisa. Sisi tumeanza miaka yote hiyo ni cheee! Nini tatizo? Hebu twambie. Eeeh! juzi kumeanzishwa redio Swahiba hapa, wewe unataka uisikilize tu, nenda kwenye chombo chetu hiki cha Serikali ni cheee! Husikii vizuri macharaza chungu nzima.

Ikiwa tatizo ni pesa sema tu kwa Mhe. Mohammedraza tukamkope, maana yeye mwenyewe kasema akopwe, tuwaletee kidogo tukishamuona Mhe. Mohammedraza, vyombo vya milioni ishirini au mia moja hivi, tunaweza tukampa hapa Mhe. Waziri ikiwa Serikali hamna pesa. Yeye mwenyewe si ameshasema akopwe, basi tumkopeni almuradi chombo chetu kisikilikane. *(Makofi/Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika Idara ya Makumbusho ya Kale. Hii ni idara muhimu sana. Kwa kweli siyo kwamba inahami na kulinda utamaduni, lakini hata katika masuala ya kuingizia mapato katika nchi kupitia sekta ya utalii. Kwa hivyo inahitaji kutunzwa sana hii. Inasikitisha sana kwamba hivi sasa historia ya Zanzibar inapotea kidogo kidogo kwa sababu ya kutokuwa makini kwenye hii Idara yetu, kwa kuangalia mambo ya Makumbusho haya. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo ninaamini yakitangazwa vizuri, na yakihifadhiwa, basi watalii watakuja sana katika nchi hii. Mimi hivi karibuni nilitembelea Iran kule, nikaulizwa habari ya Msikiti wa Mkamandume kule Iran. Lakini magofu hayakuhifadhiwa. Magofu yapo yamelemewa na kifusi na mchanga. Pale yale magofu, chini kuna *underground floor* ambayo Mzee Mkamandume alikuwa na mke wake wa kijini kule anakaa naye, lakini yamefunikwa na mchanga.

Kuna kile kisima cha Wivu, lakini wanasema wanakishughulikia, hakijashughulikiwa chochote!

Ule Msikiti wenyewe wa Mkamandume pale hauonekani hata zile kuta hivi sasa. Sasa kama tungehifadhi hili eneo, kwa sababu Wairan kwa kuwa ni mtu wa kwao wanataka waje sana kufanya utalii, lakini wakija watavunjika moyo sana. Kumbe kuna vivutio vingi hatuvihifadhi.

Nilikuwepo juzi sehemu moja pale Lubumbashi wakaniuliza habari ya Mvumopanda, huu Mvumo uko Kisiwa Panza, lakini hautangazwi katika sekta ya utalii. Nilikuja nikawaeleza hawa jamaa kuhusu Mvumopanda, wakaniambia ule mti utakufa. Mwanangu ingekuwa ni kiumbe kinahifadhiwa, hata ukifa itakuwa tumejenga lile eneo. Tukishautangaza mbona historia ya Chifu Mkwawa bado ipo na fuvu lake nimekwenda mimi mwenyewe kuliona pale. Yeye mwenyewe kafa lakini tunakwenda kutalii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikwenda Kalenga hivi karibuni tu; nilikwenda nikaona fuvu na silaha za Chifu Mkwawa zimehifadhiwa katika majengo.

Sasa Mbuyupanda kama utakufa hata yale makuti yake Mvumopanda tunaweza tukayafanya ikawa watalii wanakuja kuangalia ule Mvumo, hatuko makini. Ule Mvumo wanautaka Waarabu waje wauangalie Wa-*Persian*, hata Waafrika wa Lubumbashi ambao kazi yao ni miziki tu, wao wanataka kuja kuuona ule Mvumo pale.

Halafu tuangalie ule Msikiti mkongwe pale Vitongoji. Kuna Msikiti huo mkongwe sana pale Mkomani na wanatoka Waarabu wanakuja kuuona pale, lakini haujahifadhiwa. Kama tungeuhifadhi tukaweka *entrance gate* tukakusanya mafao, basi tungepata mafao. Kuna *traditions* wanafanya pale watu kutoka nchi mbali mbali za Huba huku, kuja kuweka nadhiri. Sasa ingekuwa tunakusanya mapato, lakini serikali haiko *serious* katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni alikuja *PhD candidate* mmoja kutoka Amerika, akaja hapa kutaka kujua historia. Halafu kule Amerika yeye anafanya *African History,* ame-*specialize Zanzibar Revolution*. Kaja hapa akataka historia ya Field

Marshal John Okello. Akahangaishwa hangaishwa sana, sijui wanaogopa nini watu kutoa historia ya John Okello katika nchi hii. Mpaka tukampeleka kwa wazee waliofanya naye kazi John Okello kule Pemba, kina Mzee Maisara kule Mkoani na bwana mmoja anaitwa Abdalla bin Juma kule Vitongoji, walikuwa wakichimba mawe pamoja, akapata historia kwa watu *locals*.

Sasa kama zile pesa zingekuja serikalini, yule alitoa vipesa kidogo, lakini kama angekuja serikalini kukawa na picha yake John Okello na akawa mtu anasoma pale anatoa maelezo serikali inakusanya mapato, si ingepata serikali. Leo tunajua watu wadogo wadogo kama sisi kutoa historia za Field Marshal John Okello jamani, hili ni tatizo. Labda kama alifanya makosa kwenye Mapinduzi, lakini historia ipo inabaki inaganda.

Halafu kuna lile gofu la nyumba ya mapumziko pale, Diko la Genzi pale Vitongoji. Ilikuwa Mfalme akiwa amekuwa- *frustrated* anakuja zake Pemba moja kwa moja katika Diko la Ngezi kule Vitongoji, kule kuna Gofu lake *fresh* kule Makaani Vitongoji pale. Kuna nyumba alikuwa akipumzika yeye na familia yake, walikuwa na maboti yao walikuwa wakiteremka pwani pale kupata upepo. Lile Gofu halijafufuliwa, watu wanataka kujua vipi. Serikali ingenadi mambo kama haya tungepata fedha nyingi. Tunaomba katika hili Mhe. Waziri uende ukayaone hayo maeneo tuliyokutajia; utaona Msikiti wa Mkomani mkongwe kabisa, utaona Gofu la Diko la Ngezi. Twende mimi na wewe Mkamandume pamoja na Abdalla Juma ambaye ni kwao kule, tukakuoneshe jinsi ya lile Gofu mlilolidharau la Mkamandume kule Pujini. Haya ni mambo ya kiutalii sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niingie moja kwa moja katika Baraza la Sanaa. Hapa ndio kwenye mambo, sio tu baraza hili linakuza vipaji na kusimamia sanaa tu pekee, lakini hata kuenzi mila, silka za Wazanzibari, lina wajibu huo. Hili Baraza la Sanaa lazima linatakiwa liwe makini sana.

Mhe. Mwenyekiti, nini sanaa. Sanaa ni kiyoo ambacho jamii hukitumia. Hiyo sanaa na hatimae kujirekebisha, ndio maana ya sanaa hiyo. Sasa tuziangalie sanaa zetu ni kiyoo kweli?

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni watoto wangu walifungua *TV* pale nyumbani, nikaona hizi ngoma za vijana za siku hizi, na kwa bahati chombo kilichokuwa kikionesha sanaa ile ni hiki hiki chetu siye *ZBC*. Mimi ndio nilikuwa nataka kupumzika hivi, watoto wangu wananiwekea chakula na ile *TV* imefunguliwa nilikwenda mbio chumbani nikajifanya kama naumwa. Haiangaliki, wanacheza humu wanajikamata kwenye maeneo yao ya siri, wakati mwengine vile viguo wale wanawake ndio tatizo Mhe. Mwenyekiti. Wanaume wana nguo refu, lakini

wanawake wana viguo vifupi. Mimi nashangaa badala ya wanawake kuvaa nguo refu basi hao wanawake ndio wanaovaa viguo vifupi, tena nakuambia haziangaliki.

Sasa hicho ndio kiyoo, kwamba wewe uangalie wanakwenda nusu uchi, sijui tatizo liko wapi katika nchi hii. Mimi naomba *ZBC* isioneshe michezo kama ile inatutia haya, inatutayarishia magoma kama yale *ZBC*, naomba Mhe. Waziri mu-*edit* ngoma zinapigwa vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wakati wa miaka ya 1960 katika nchi hii ilikuwa taarabu zipo na ngoma zipo, lakini ukienda kwenye taarabu, mwimbaji humuoni katika miaka 1960, kajifunika baibui lake wewe unasikia sauti tu. Ilikuwa roho zinatuburudika, unasikia sauti tu nyororo ya mama yetu Sitti bint Saad wala hakuna vijembe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisikiliza nyimbo moja katika hizi sanaa nilicheka sana, hamu-*edit* haya mambo. Kuna nyimbo iliimbwa na mama mmoja wa Kizanzibari inaitwa daktari, ilimradi ile nyimbo kama ukiyasikiliza maudhui ni tatizo. Kwa sisi tuliokuwa hatusikilizi miziki tunasikiliza nyimbo haifai mambo mengine kusemwa mbele ya watu, hatari kubwa.

Mambo kama haya mtatusaidia vipi yasiendelee Mhe. Waziri na nyinyi mpo serikali. Watu tangu zamani wanapigana vijembe katika mambo ya kuimba, lakini sasa kipindi hiki wamezidi. Anamuambia sijui komo tupu, miguu yote ya kushoto, hivi hivi unamuumbua mwenzako wazi wazi. Wangeiga sanaa za zamani na hawa watu wako wa sanaa waambie waige sanaa za zamani. Wakati mama Sitti bint Saad yuko hapa kwa shughuli zake za kuburudisha, watu wa mjini walimsema sema.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nimnukuu kidogo. Kuna mama anaitwa Mwasada bint Ali, katika kumpiga vijembe mama Sitti alimwambia, naomba nimnukuu kidogo;

> "Sitti bint Saad umekuwa mtu lini, umetoka kwenu shamba na kaniki mbili chini, kama si sauti ungekula nini."

Bi Sitti wala yeye hakutukana, kama wanavyotukana hawa wasanii wa sasa. Mama Sitti alisema, naomba ninukuu vile vile. *(Makofi)*

> "Uzuri wa mtu sio sura, jamii wala utukufu sio jubakubeli, hasara ya mtu kukosa akili".

Alijibu hakutukana na tuliburudika sisi. Lakini haya mambo ya matusi mnatupeleka wapi nyinyi mnaoshughulika na mambo haya watu wa serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naona uliniwashia taa, naomba nimalizie na mambo ya Baraza la Michezo ambalo linasimamia soka. Hapo sasa ndio kwenye vita. Kuna aina tatu za soka. Kwanza nataka nikuambie zaidi ya asilimia 100 ya Wazanzibari wanapenda soka kabisa. Inasikitisha kwamba wizara inayoshughulika na mambo ya soka hampo makini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hapa katika miaka ya 1980 Mzee Jumbe alihangaika kutuletea kocha anayeitwa Kamwelea, aliliendeleza soka hapa tukashinda Kombe la Afrika ya Mashariki na hao hao wachezaji wa *local* tuliokuwa nao; akina Kidevu, Karume Mussa akina Thomas Kohoe, ni sababu gani sasa hatufanyi vizuri, inasikitisha. Kocha yule Tambwelea alitubadilisha na tukamuozesha mke hapa kama zawadi, mtoto mzuri wa kiarabu.

Leo nyinyi mnatufanya nini, kila kukicha sisi tunafungwa, kila kukicha tukienda kushindana tunafungwa tu, mpaka Burundi wanatufunga, wapi sijui wanatufunga, ilimradi hivi vijinchi vyengine ambavyo hata havistahiki kutufunga, vinatufunga.

Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, hebu tujitahidini na sisi kidogo mtunawishe uso Wazanzibari, soka tunalipenda sana hebu anzisheni ule utaratibu kama walioanzisha ndugu zetu wa damu. Ndugu zetu wa damu wao wameanzisha *Airtel Rising Star* wakaibua vipaji. Bwana yule sijui nani aliyekuwa na kituo kile cha kuinua vipaji pale Dar es Salaam vyuo vingi vipo sasa, nyinyi hamna kazi yetu kusema maneno sio kufanya vitendo, hebu tufanyeni matendo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna soka hili la ufukweni hivi juzi kulikuwa kuna kombe la dunia, Zanzibar hawajui lolote na fukwe tulizonazo ni chungu nzima, kazi yetu ni kuwapa watalii wakijenga mahoteli tu. Lakini kuna soka la ufukweni siku hizi, ukenda Abudhabi lipo, Dubai lipo, Oman lipo, kwa nini sisi fukwe zote hizi hatufanyi soka la ufukweni. Juzi kulikuwa na soka la dunia la soka la ufukweni Zanzibar, hatukushiriki kwa sababu hatuna fukwe za kuchezea mpira, tumeshawapa watalii wanazijengea mahoteli. Tatizo ni njaa, tukiendekeza njaa itatuumiza na itatuweka pabaya.

Mhe. Mwenyekiti, hebu tuangalie jambo jengine. Kuna soka la akinamama siku hizi limeshamiri ulimwengu mzima, wala msijekufikiria labda ni wazungu tu hapana, mpaka nchi za Arabuni. Mimi nilikwenda kuangalia mechi, pale Rashidia wanacheza mechi akinamama, wamekula *tracksuit* zao wenyewe wanacheza mechi za wanawake.

Je, hapa tuna timu ngapi za akina mama na tumeshashiriki mashindano mangapi ya soka la wanawake. Tatizo hii ni *globalization* tusijifanye kama tuko vichochoroni.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tujitahidini sana nilikuwa nafikiria suala la kwamba tuajiri kocha kutoka nje ya nchi ili tuinuwe hili soka. Lakini kama tutakuwa makini na kuwafundisha hawa hawa kina Suleiman Jabiri, basi wanaweza kulifanya soka hili kuwa zuri.

Kwa nini *Paul Western Gwivah* mwaka 1974 ni *local* kocha na wachezaji tuliokuwa nao hapa ni kina wale wale kina Adam Sabu, Abdalla Kibadeni, Shaban Baraza, Othman Mambosasa wale wale ndio *local players* waliiwezesha Simba kuingia nusu final ya Kombe la Afrika. Ni yule yule *Paul Western Gwivah* Mnyamwezi wa Tabora. Kwa nini Suleiman tusimuwezeshe, Mzanzibari wa hapa hapa tukampeleka kufanya mafunzo akaja akaiwezesha hii timu yetu, angalau tukanawa uso katika ulimwengu wa soka.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nadhani nitaunga mkono hoja hii baada ya kupata maelezo ya kina jinsi ya mtakavyoliboresha lile Gofu la Mkamandume, jinsi mtakavyouboresha ule Mvumopanda kule Kisiwapanza kwa Maalim Haji Faki, jinsi mtakavyoboresha suala zima la Msikiti wa Mkomani pale. Baada ya maelezo hayo, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nilikuwa nataka nikuulize swali dogo sana. Swali hilo mimi naamini Waheshimiwa Wajumbe wanaweza wakaniunga mkono. Hivi nikuulize mawaziri wa upande wa kule wamekwenda likizo. Hili ndio swali langu dogo, naona siwaoni kule. Aah! yuko mmoja waziri mtarajiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na kuchangia na kile kipindi ambacho kinaitwa maelezo baada ya habari. Kipindi hiki ni kizuri sana kwa kutoa habari hasa za wakubwa ikiwa zimewakuta, basi kipindi hiki huwa zinawatolea, tena badala ya siku moja huwa wanatoa mpaka siku mbili, nina kumbukumbu.

Katika kipindi fulani, nilitokezewa na tatizo kama niliumwa na tumbo siku hiyo, bahati mbaya na wewe ndio ulikuwa shahidi na ulikuwa wewe Mwenyekiti kama hivi ulivyokua. Nilikuwa naumwa na tumbo la kuharisha. Kwa bahati mbaya basi tena ikawa balaa dunia nzima, kipindi kile kinaeleza tu habari. Mwenyekiti kaingia mitini, Mwenyekiti hivi, Mwenyekiti hivi. Lakini kuna mambo yalipasa alikuwa ayatolee maelezo kila leo kwa kuweza kuwasaidia wenzao au ilikuwa inachagua la ndani hataki kulisema, anapenda sana kulitoa la nje. Namuomba sana kama yupo ananisikiliza basi leo nataka nimwambie.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hawa wanaotuhudumia humu ndani kwa kweli ni watu ambao wanapata tabu sana na kama posho waliambiwa wachukuwe 50,000 wanapata 25,000 na ile wanakopwa. Ilikuwa habari iseme kuwasemea hawa, iwatolee taarifa kwa kuwaelekeza jinsi gani hawa wanavyopata tabu.

Mhe. Mwenyekiti, haisemi hiyo mimi nashangaa sana habari maelezo inachagua, inataka wakubwa tu. Lakini wale waliokuwa wadogo ambao wanastahiki kutolewa maelezo wanapata tabu maskini ya Mungu, kwa sababu wapo wanapata tabu kutwa nzima wanasimama. Wakati mimi niko mzima na sisubutu kusimama dakika nzima, seuze wao maskini ya Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana, sasa namuomba awaelezee hawa Habari Maelezo wenyewe ndio hawa kwa sababu yeye ndio muona zaidi kuliko sisi. Unajua kuna jambo ukilisema wewe unalisema vizuri sana kuliko kukusemea mtu mbali. Sisi tunawasemea, lakini halishiki, akilisema yeye litashika.

Kwa hivyo, namuomba sana mtayarishaji wa kipindi hiki ajiangalie na yeye ndani, mapungufu anayo mengi sana. Kwa sababu hii *ZBC* ni televisheni ya zamani sana, wakati huo tukisema 'uhuru ni wetu'. Lakini wapi sasa hivi. Ningemalizia lakini kidogo sauti imeganda.

Mhe. Mwenyekiti, wakati ule ilikuwa jengo zuri, sehemu ya kurikodia nzuri. Nenda leo wenzetu wameshatupita na sisi katika *East Africa* nzima televisheni ile ndio ilikuwa ya mwanzo. Hayati mwenyewe aliitengeneza ile kwa nguvu zote na *TV* zake zilikuja za *model;* za fomeka sijui kama wengine walikuwa washazaliwa, lakini leo tumerudi nyuma wenzetu wametuzidi. Sasa ningeomba sana hiki kipindi kisichagua mwahali mwa kusema, kiwasemee na wenzake.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wanajituma katika hali halisi ilivyo, lakini ukija katika vile vyombo vya kisasa hamna. Siku moja mie nilicheka, *TV* hii inatakiwa ikapokee Rais, *TV* hii inatakiwa itoe maelezo watu waone jinsi gani Baraza linavyoendeshwa, sasa kinyang'anyiro. Sijui kwa sababu gani kuwa siku zote hatuna *modern system,* kila siku tuna mambo yale yale. Ukweli hatupigi hatua, hii inasikitisha sana. Inavyotakiwa sasa hivi tuwe mbali kabisa, si utani tuwe mbali sana. Lakini tunarudi nyuma kila siku, tatizo hili linanisumbua sana.

Mhe. Mwenyekiti, ukija kwenye *private sectors* hapa miye ndio ninapolia machozi *private studio* zao ni nzuri sana, zipo mahiri utataka wewe ulale, ukialikwa wewe mwalikwa uliyekwenda pale, unaambiwa dakika zimeisha bado unajidai kujizungurusha uongo. Maana yake maana yake, kutokana na ile hali halisi si kam *government.*

Mheshimiwa nijiulize bajeti inakuwa ndogo inawezekana labda bajeti inaweza kuwa ndogo, kwa sababu utiliwaji unavyotakiwa kwa asilimia *hundred,* unakuwa unapata *fifty percent,* hiyo inawezekana.

Kwa kuwa sasa hivi tunaelekea huko kwenye hii PBB mimi nafikiria labda Mhe. Waziri atakayerejea tena hapa atakuwa makini sana katika kuendesha programu hii ambayo itakuwa mahiri sana. Hawa ndugu zetu wa Mawiyo, inasaidia sana Mawiyo; inafichua watu kweli lakini ukweli bado hatujawa *serious* nao, inasikitisha sana. Kuna kipindi fulani tulikosa hata Mawiyo kuyasikiliza.

Mheshimiwa, kama hatuna watu hawa wa Mawiyo sijui kama *radio* yake itaweza ku- *work* vizuri. Zamani wenzetu Bara walikuwa wana majira, kwa hivyo mimi naomba sana tuendane na *system.* Sasa hivi twende na wakati. Mimi nakuaminia kabisa juzi umerudi Ulaya umeshaona mambo mengi wenzetu wanavyokwenda.

Kwa sababu kwenda Ulaya kuchukuliwa na Rais kwenda kuangalia ya kule ukaja ukaturisisha, mimi nakuambia naamini hiyo sasa muda uliobakia mchache, huu utatengeneza mambo mazuri katika redio, naamini hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kitabu kidogo hivi kina hii *emergence* kuimarisha huduma katika kitengo cha matibabu ya dharura *emergence* Juni; hii kwa kweli tunaanzisha vitu vizuri lakini je, nijiulize tunazo zana na hii *emergence* inakuwa uwanja wa ndege au bandarini, lakini tumejiandaa vizuri kwa sababu *emergence* ni nzuri sana.

Kwanza kwa wenzetu inatakiwa *emergence* iende na *ambulance*, ukishafanya *treatment* pale ukiona hali imekuwa ngumu inatakiwa um-*control* je, hilo tunalo. Hiki kitabu kidogo ukurasa wa 10 kitabu chako ninacho hiki. Tuwe na dawa kamili za hii *emergence,* kwa sababu sasa watu wanakwenda na wakati. Wenzetu huko nchi za nje wanavyo vitu kama hivi vimejaa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba sana vitu hivi uanze, mimi sijui kama kipo na kama kipo sijui kikoje, kinalingana na ile *emergence* yenyewe au basi *emergence* tu mdomo. Maana yake unaweza kutengeneza *emergence* umeweka meza moja pale na kitanda ovyo ovyo basi ndio *emergence.* Tunataka *full equipments oxygen* iwepo pale, *doctor* awepo pale. Nimeona nieleze mapema isijekuwa *emergence* ile ya kwenda hospitali Mnazi Mmoja, kuna baadhi ya vitu vyengine hamna. Sasa mimi nakuomba jitahidi sana katika suala hili la *emergence* kwa sababu binaadamu wale wanapokuwa wanashuka kwenye ndege watu wanaweza kupata presha hafla, moja ukamuona kaanguka inawezekana kapata kizunguzungu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kusema jambo moja najitahidi sana kujaribu kuishauri Serikali hususan Wizara, sisi wengine mtakuja kututaka tukupeni fikra,

mtakuja kutukosa. Kwa sababu tunajitahidi sana ili kutoa fikra ziendane na ile hoja yenyewe.

Leo mimi nina ushauri mwengine na mnapokaa na Rais mwambieni msione tabu Waheshimiwa, Rais ni binaadamu, Rais si mambo yote anayaona, inatakiwa nyinyi Mawaziri muwe *friend* na Marais, muwe munamuomba kila baada ya muda mwende mukakae na Rais kutokana na Sheria hizi na hizo nyengine zinakuwa zinapitwa na wakati, ili kwa kwenda kumlobi Rais. Rais ni mtu msikivu, hana tabu na mcheshi. Msingojee mpaka akwiteni Rais, ataita wangapi kapige hodi tu Mhe. Rais, si unataka nije nikuone. Mkifanya hivyo basi mutamsaidia sana Rais wetu, tena mutamuweka pahali pazuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, natoa wazo langu jambo hili linanisumbua sana kwenye akili yangu. Nazeeka sana kwa suala hili kwa sababu ni jambo la umuhimu na likajengeka kwa sera nzuri kwa mujibu wa sheria, Mheshimiwa ana utalii lakini utalii wake una mipaka ambayo kwa mujibu wa sheria hawezi akaingia.

Sasa hapa ndio kosa lenyewe linakuja hilo wazo lenyewe. Ukimwendea Rais ukimwambia Mhe. Rais mimi nina utalii lakini sheria hainipi ku-*control* utalii kutokana na sheria siipati iko katika Wizara nyengine.

Mheshimiwa, mngeipata Idara ya Kamisheni ya kazi ukaiweka hapa, ungefanya kazi nzuri sana, lakini kwa kuwa ile haipo hapa unakuwa na utalii ambao uliokuwa hauna mashiko.

Kwa sababu gani nikasema waheshimiwa nikijiuliza mahoteli yale *controller* nani na ndio utalii ule, hebu tuangalie sheria hizo nenda katizame kama ipo. Mimi nikisema leo nitakuwa nakuonea bura hapa, utakuwa huna vya kunambia, nakuonea huruma sana kwa sababu mahotelini watu wanadhalilishwa, unangojea wewe mpaka sheria akutolee mtu. Wewe umenyamaza kimya tu pale na wakati wewe unatakiwa urekebishe yale masuala, lakini sheria huna, labda kama unayo sheria hiyo niombe utusaidie sana kwa sababu kuna mambo mengi.

Mhe. Mwenyekiti, Mungu amlaze mahala pema Ndugu yangu Ali Hanen Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri huko, ampunguzie adhabu ya kaburi, alikuwa alikuwa akitusaidia sana *hundred percent,* alitusaidia kutukutanisha wana kijiji na mwenye hoteli na kutengeneza mikataba ambayo inaweza ikawasaidia wana kijiji wakatumia haki yao ya ardhi, alifanya kazi vizuri tu.

Kwa hivyo, mimi ningeomba kutokana na hili sasa hivi tunaona iko *silence* kabisa kwa sababu zile sheria alizokuwa akizisimamia marehemu sasa sidhani kama kuna mtu mwengine anasimamia, kwa sababu kuna matatizo kule Kiwengwa,

mahotelini, wawekezaji na wananchi kulikuwa na ugavi wa *percentage* ya kuingia kazini ya wafanyakazi, kwenda kufanya kazi mule ndani ya hoteli kutokana na kuridhia zile ardhi zao na kuridhia kufungwa njia.

Sasa Mheshimiwa unajua zile njia zilikuwa zinafanya *short cut*, lakini wamekubali wananchi wazunguruke kwa juu kabisa, ili wende katika eneo jengine mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, wale walitengeneza sheria nzuri lakini leo haziwasaidii kitu, ndio maana mie nikawa najiuliza sasa ndio maana nikakwambia tuangalie hizi sheria kuwa je, wewe unazo sheria, kama unazo sheria kwa nini hazifanyi kazi katika Wizara yako, sidhani kama unazo.

Mheshimiwa sasa hivi wanapata tabu wananchi wanakubaliana *African diner* wakati ule walikuwa wakiingia watu chungu nzima sasa hivi *African diner* wanaingia watu kumi tu, inasaidia nini? Kwa kweli inasikitisha sana.

Kwa hivyo, kama yupo mwanasheria wako naomba sana sheria kama inampa ashuke chini akawaone wale wananchi kule vijijini, ili waweze kufika na kuona mambo mengi sana ndani ya mkataba walikubaliana mle, mna mambo ya kusaidia timu, mna mambo ya kusaidia maji, lakini leo utacheka wananchi wanakatiwa maji na muwekezaji, maji yamo kwenye ardhi yao. Hili ni jambo ambalo linasikitisha sana, hawana maji wananchi. Kuna maana gani kuwekwa hoteli.

Sasa mimi nashangaa sana hawa watu wanapokuja wana maneno matamu, wamewalobi wananchi vizuri, wananchi wamejaa tele hatimae wamewachia mbali, walisema tutawasogezea umeme, walisema tutawasogezea maji, tutawapa maji matamu kama asali na kila kitu hawajapewa hao Mheshimiwa Waziri.

Jamaa wamewalobi vizuri mpaka kinamama wameinama hivi shingo upande, leo kinamama Kiwengwa wanashindwa kutia kalikiti, kutwa wako kwenye kubeba madoo tu. Haistahiki, mimi naomba sana tuweze kubadilisha utaratibu, ndio maana nikakuuliza, kama unayo sheria rafiki yangu uje unijibu na kunijibu kwako nione utekelezaji wake ukoje, katika hatua inayokwenda nao.

Kwa kuwa tunapenda sana kusema lakini ufuatiliaji unakuwa mdogo sana ni kitu ambacho nasikitishwa sana, mimi nafikiria watakaokuja mwakani hapa undeni sheria, Sheria hiyo isiwe tumalizie sisi ndani ya Baraza la Wawakilishi, wakimaliza ndani ya Baraza tuwe na *Manpower* ya kuweza kwenda kufuatilia yale mambo bila ya kusulubishwa chochote, bila ya kuwekewa kiwango, hiyo nafikiri itasaidia sana.

Sheria tuibadilishe hiyo kwa sababu sisi humu nyie ndio mnakuwa watiifu, wakimya kabisa, mnaridhia hewalla bwana mnamjibu mtu kwa utaratibu maana yake mna-*enjoy* mnavyotujibu kwa utaratibu, unangoja umalize hapo ikipita ndio ukifika siku ya pili hufanyi tena lile jambo, hapo mimi mnanichekesha.

Mimi nafikiria sheria lazima iangaliwe upya Katiba inapokuja ikafanye mageuzi ya mambo na hivi vituko vyengine vya lazima vilazimike, asingojee kupitisha bajeti tu akubaliwe moja kwa moja akimaliza afuatilie awe na sheria ya kuweza kufuatilia mpaka akijue mwisho.

Kwa sababu wengine Mhe. Mwenyekiti, ukiwafuatilia wanakushangaa sana ooh, Mheshimiwa Muwakilishi ananifuatilia, allah wee vipi! Kwa sababu hakuna sheria tunakwenda kimabavu tu wengine, lakini kungekuwa na sheria unamwambia kifungu namba fulani kinasema hivi na hivi, mimi nafikiri leo mwanasheria kenda likizo sijui angekuwepo ningemwambia ajaribu kututafutia sheria, ili aweze kutusaidia au wanitafute mie wasione vibaya kunitafuta mie nikawasaidia sheria, kwa sababu sheria mimi nashangaa watu wengine sheria lazima usome kama Mhe. Wanu, si lazima sheria usome unayo mwenyewe akilini tu. Unaziandaa zile sheria ambazo unatumia katika nchi nyengine, unaangalia *reference* ya nchi nyengine wenzetu wanaendeshaje mabunge. Unaweza ukatoa mfano ukawa mzuri watu wakashangaa kabisa hapa, umepata wapi sheria zile kumbe mwenyewe umezitizama zinavyofanya kazi, zitamsaidia nani.

Kwa sababu kuna sheria nyengine si mabano, utunge sheria ambazo zitawasaidia jamii. Mimi ningefurahi sana kitu hicho, ili uweze kusadia katika harakati za kuendesha.

Mhe. Mwenyekiti, unyanyasaji umezidi katika mahoteli, tumeshasema sana kwenye idara ya kazi lakini ufuatiliaji bado ungali hafifu, wanafukuzwa watu wetu, ma-*P.O* wa Kenya Mheshimiwa sio Watanzania ni jambo ambalo linasikitisha sana Mheshimiwa wangu, ni ma- P.O ambao Wakenya wapo kibao kwenye Mahoteli hatuwataki. Kwa nini jamani wakubwa mnatung'ang'ania wanawaleta wenzao Watanzania tunakosa nafasi, tunalia na njaa tunalia na ukame, haki yetu wenyewe, ardhi yetu wenyewe, inasikitisha sana.

Mheshimiwa, *Wallahi* nataka kulia inasikitisha sana watu wanakuja kuchuma watu wa nje, vijana tunao wamesomeshwa utalii wanaweza kukaa U-*P.O* wanaweza sana, tunao Watanzania wapo wengi tu chuo kile kina maana gani cha utalii.

Mheshimiwa, inasikitisha tunasema hatuwataki ma-*P.O* wageni tena, halafu mafisadi maana yake ufisadi wenyewe wana fitina, neno si neno umefukuzwa

wanaleta mtu wao ndani. Nendeni kwenye mahoteli kama ninasema uwongo mie wamejaa tele, tunawachekelea tu sijui *migration* wanafanya kazi gani pale.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sasa tumebakia jamani hatari hatari, chonde chonde tusiwaamshe hawa ndugu zetu waliolala, vijana watakuja kutupiga mikwaju inasikitisha sana. Utakuta mtu kwa mfano kuna hoteli ya Melia imo ndani ya jimbo langu ana kesi chungu nzima za kuwadhalilisha watu kumbe yule mama sie ni Mganda, ati anasema kwao Pemba mimi nilishangaa, ukimuelekeza kiswahili anashindwa ata kile Kipemba hakipati tumemgundua kwamba sie yule.

Naomba sana, anasema ati jamaa zake kina Marehemu Dkt. Omar ninashangaa sana kumbe sie anatumia ubini tu anadhalilisha vijana wetu, hatari hatari haisemeki, jamani kilio mtu neno si neno anamfukuza wapo watoto wanawake wakafanye kazi wapi, hata bustani nobe bustani. Inasikitisha sana iko siku mie nitaandamana, nitawachukua vijana twendezetu, kweli inasikitisha tushasema sana hapa. Tushasema sana Mhe. Waziri, tufikirieni, tuoneni huruma tunawatetea wananchi kwa uchungu kabisa kwa sababu hawapati, ile fursa iliyotolewa na Serikali hawaipati.

Hoteli za kule Nungwi wote hawana maana pesa mbili, wanawadhalilisha tena bosi, mabosi wenyewe wanaingia nchini bila ya vibali wanakuja wanachukua rizki zetu bila ya vibali, Serikali tumelala.

Mheshimiwa, wanaingia bila ya utaratibu, wako kibao ukija kaskazini, kusini wapo kibao ninaomba Kamandoo wewe hebu wewe kaa *meeting*, sasa jikusanye Mheshimiwa ziite hizi *department* zote zinazohusika kesho kama hatujapitisha bajeti yako mimi naitia mfukoni, hii bajeti yako na unajua nikikupigia fatiha watu wote watakuunga vizuri hao. Kaa na zile sekta zinazohusika, kaa na uhamiaji, waite *labour* kaeni *team work* kwani kuna tatizo gani. Kaeni nao *ZRB*, watieni pingu hawa. *Wallahi* inasikitisha sana tena wanafika pahali wanasema ah! viongozi wote wamewakamata mkononi, wamewafunga. Wanamatusi, Mzungu huyo anasema au sijui Mkenya ameitia mfukoni Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar? Ah! Inasikitisha sana, anasema huku anaringa, na kiasi ni kweli. Lakini na sisi viongozi tuna tamaa pengine tunakwenda kulishiwa, tunakwenda kupewa pesa kule. Jamani inasikitisha sana, anatutusi kwa kutwambia Serikali yote ya Mapinduzi ya Zanzibar imo ndani ya mfuko. *Oh, my God! Inna lillahi waina ilayhi raj-uun*, Ah! Mtu anafikia *level* hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu hawana fursa, wakikohowa basi kosa, wao hawafukuzwi. Kuna mtu kapigana ndani ya hoteli akafukuzwa, wakati yeye ndiye aliyepigwa na mwenzake. Mwenzake kaendelea kazi. Tunakwenda wapi? Kwa kweli hatujawatendea haki ndugu zetu. Mimi naomba kutoa ushauri au nasaha.

Unajua, ngojeni nikupeni mfano hai, wenzetu walivyokuwa wanajali sheria. Nilivyokuwa Australia mwezi mmoja, huyo niliyekwenda naye, tajiri mwenyewe alikuwa ana *restaurant* pale. Kuna jamaa alikuwa *chief cooker,* alifoji cheti kumbe yeye hajafikia kuwa *chief*.

Mhe. Mwenyekiti, sheria ilivyokuwa kali, jamaa yule kakamatwa halafu na ile *restaurant* ya yule jamaa, kaambiwa aifunge masaa 24, aondoke. Yule jamaa ni mtu wa Spain. Tizama wenzetu walivyokuwa wana sheria. Leo nenda Mahoteli, haki ngapi tunazikosa, *Wallahi* tunazikosa haki nyingi sana hatuna ufatiliaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikuulize swali moja. Sisi tuliunda *committee* ya ulinzi ya Polisi juu ya mambo ya ulinzi wa utalii. Ile sijui ikoje? ina *play* vizuri au basi tu kwa sababu walikuwemo maafisa mbali mbali, mfano walikuwemo KMKM, Magereza, hiki kitengo kikoje na hizi haki zinatendeka vizuri. *Influence* zile wanapewa vizuri, inatusaidia sana katika ulinzi ile. Kwa sababu walikuwa haweshi kuvamiwa vamiwa. Hebu ukija unambie vizuri na ikoje na umeimarisha vipi. Maana nasikia watu wanafukuzana tu ovyo ovyo. Naomba sana ile na kama haipo tuweze kuirejesha. Tuirejeshe kwamba wengine wanakuwa hawana uwezo wa kukodi *security*. Lakini wengine wanao uwezo wa kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende katika michezo. Michezo hakuna mtu asiyejua kwamba ina raha zake. Zanzibar tumekuwa kama kichwa cha mwendawazimu kila siku tunafungwa tu. Tujiulize kwa nini tunashindwa. Timu ile ya Taifa ya Zanzibar, sijui kama inafika angalau watu 50 na kamati ya ufundi sijui nayo kama inafika watu 50.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikwambie tatizo linaanzia na ule uwongozi wenyewe, kwanza niseme ukweli ulivyo. Uongozi wenyewe ndiyo unaoanza kutoa jambo la hatarishi. Kama nyinyi viongozi hamjawa mahiri, hamjawa na hamu ya kuendesha kile kitu, si dhani kama jambo litaenda, nakataaa kabisa tusidanganyane.

Mimi siingii kwenye Wizara kwanza, ule uwongozi wenyewe kwanza. Uwe na hamu wa lile jambo. Mfano, tizama sasa hivi riadha inavyokufurahisha. Wale viongozi wenyewe wana hamu ya kuirudisha ile hadhi yao lakini sema hakuna fedha, hamtutilii fedha, hamtusaidii wenye vilabu, inasikitisha. Hebu tusaidieni muone watakuleteeni medali kila siku za dhahabu hawa wana riadha.

Sio mchezo, lakini hatujawa *serious* na mambo ya michezo katika Zanzibar, tuseme ukweli, hatujawa *serious* katika michezo yote; *netball*, riadha, *volleyball*, *football*, kila kitu, mambo ya uogeleaji, mambo ya *table tennis,* sijui kama ipo.

Mheshimiwa, usione shida waiteni wale waanzilishi wa huko nyuma. Hebu jaribu kuwaita, kaa nao waambie, waiteni, zungumza na Katibu mwambie awaite na tuweze kujua kosa letu ni nini, watusaidie. Sisi katika timu yetu katika uwongozi wetu tumewakusanya wale wakimbiaji wa zamani, kina Yakuti, Yussuf Nassor, na wengineo wote, tunao pale wanatusaidia. Lakini sisi wenyewe tu sugu. Sasa na nyinyi Mhe. Waziri waite watu wa *football*, halafu wachezaji wa zamani wale, kina Shabani, kina Abdalla, wapo bado, hebu waambiye jamani sababu gani inayosababisha kutokufanikiwa? Tupeni maarifa, nyinyi mkae kimya, muwasikilize nini watakavyokwambieni. Halafu muyachukue yale wanayokwambieni.

Tunasikia watu wanaopelekwa Mahakamani, tunasikia watu wanaambiwa wajiuzulu, hawajiuzulu. Michezo vurugu vurugu tu, kwa kweli inasikitisha sana. Naomba sana tujenge heshima yetu ya Zanzibar katika michezo yote. Uwezo tunao, tena sisi ni wazuri sana Zanzibar, *Wallahi*. Lakini hatuwatumii kwa sababu hatujawa tayari. Mfano mdogo tuone kwamba tunanyanyaswa riyadha tu kuomba chumba cha ofisi mnawapiga danedane, leo kesho, njooni huku, leo fanyeni hivi. Jamani mimi nauliza hawa riyadha watoto wa nani? Hebu niambiwe, ili niwapeleke kwa baba yao. Hawa ni watoto wenu lakini hamjawathamini. Ule uwanja umekuwa ndio japo kuwa una idara maalum, lakini msifike kuwanyanyasa kiasi hicho. Nchi za wenzetu vyombo vile vinakuwa karibu na uwanja.

Nimekwenda mimi kutembea uwanja wa *Badalona* nimekuta *basketball* ipo karibu, nimekuta kila kitu kipo karibu ndiyo hayo yanayong'arisha uwanja. Leo hapa mnawasumbua, imekuwa kama watoto mayatima. Riyadha ipo yatima kutokana na hali halisi ilivyo. Juzi tu hapa wamekwenda Bara wamepiga vibaya sana, wameleta medali hapa. Si tuwone raha ile. Sasa mambo kama haya bwana tunakuwa tunawafanyia kwa makusudi hawa watu, ili kuweza kuwadhalilisha. Naomba sana hili.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie makumbusho. Kwenye makumbusho ukurasa wa 43, mimi naona hatujawa *serious* katika kuweka kumbukumbu zetu. Unajuwa kuna watu wanaweka kumbukumbu, mimi huwa nashangaa. Huwa natoa mfano sana hapa wa Mzee Ali Mzee. Mimi nilifikiria ana kumbukumbu za magazeti, ana kumbukumbu za mabarua. Lakini ana kumbukumbu ambazo wewe Mhe. Waziri akikuonesha hizo picha wakati mdogo mimi mwenyewe nimeshangaa alizipata vipi.

Tizama mtu binafsi tu anaweka kumbukumbu za historia, anajifahamu zamani kulikuwa na nini na picha hii nimepiga kwa wakati gani na kulikuwa na maafa gani mpaka tukapiga picha hii. Waheshimiwa wapo hawa tunaona tabu gani kuwafata. Kuna sehemu ambazo pengine Mzee Ali anazijua za historia ambazo pengine kuna

jengo lina historia nyinyi mnataka kujua, waiteni hawa tusione shida. Kwani tunaona tabu gani, si kumwita kwani si binaadamu na yeye anajuwa. Kuna watu wengine elimu imo ndani ya ubongo kama mimi nilivyo elimu yangu imo ndani ya ubongo. Maana yake mimi naona mambo, lakini mimi nikikwambieni hamtaki kuyafanyia kazi ,kumbe yapo ndani ya mstari.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana nimshukuru huyu mama Dkt. naye ni jasiri lakini sasa ujasiri wake unazimia kutokana na vianzio. Wenzetu katika kuunadi Mji Mkongwe (*Stone* town), wenzetu wanataka kuujenga kwa matofali sijui sasa hivi tutauitaje *stone* tofali, au vipi. Tutachekesha au *town tofali* au vipi? Tutachekesha lakini *Stone town* ndio asilia.

Tulione lile jengo la wenzetu limejengewa kwa kitu gani. Utaona ile saruji tu imekolea, wanakuwa wanafanya mambo ya asilia, kama mnavyofanya ile jahazi. Lakini wanakuwa wanaweka ile miundombinu ya kuleta zile ngoma za asilia za vijijini, wanakuwa wanazifanyia *party* katika ile sehemu ambayo wanaiweka maalum. Wana siku maalum wanakuwa zile ngoma za asili zinapigwa. Basi nisikilizie watalii wanavyojaa hapo. Wakijua mambo kama yale yapo, tutafanikiwa katika utalii, tuvitafute hivi viko kama mfano kule Mwembe Majogoo kuna sindimba ile ya asili hasa ya kibati, tuwaite na vinyago vyao. Yale mangongoti, tuwaweke katika laini mle, uwone.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Naam, nimalizie hapa na niunge mkono kwa shingo upande kwa kuwa ndio bosi wangu usije ukaninyima pesa za fungu la riadha, maana yake mashindano tunaanza karibuni. Naunga mkono kwa asilimia mia. Nakuona mnyonge Mheshimiwa, umeshaweka shingo upande. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Mwenyekiti, asante sana na mimi kupata nafasi ya kuuliza machache sana juu ya Wizara hii tunayoijadili hivi sasa. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Nimpongeze Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa namna alivyowasilisha taarifa yake hii kwa umakini na kwa muda mfupi kiasi.
Pia nimpongeze na kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati na yeye kwa mchango wake na uwasilishaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii kama ilivyojieleza ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwa hivyo hii wizara inahusika na vidokezo vinne navyo ni:

- Mambo ya habari;
- Mambo ya utamaduni;
- Mambo ya utalii; na
- Mambo ya michezo.

Nianze na hii Sekta ya Habari; habari kwa hapa kwetu imegawika sehemu tatu; tunapata habari kutokana na redio, televisheni na magazeti.

Redio Zanzibar ni kongwe mno kabla nyote hamjazaliwa. Kutokana na ukongwe wake ingekuwa redio hii iwe na taarifa nzuri ambazo zipo *up to date* kutufikishia sisi wasikilizaji.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Waziri kuwa wameanzisha redio FM nyingi kama walivyozitaja kuwa saba na televisheni nne. Lakini je, redio hizi na televisheni hizi ukilinganisha na zile zetu ambazo ni kongwe, hata TV ni kongwe kuliko hizi ambazo zimeanzishwa.

a) Ni zipi zenye ufanisi zaidi katika matangazo yao?
b) Ni zipi ambazo zinatoa habari kwa haraka kwa wananchi kuliko ile ya kwetu, ya serikali au hizi za binafsi?

Kwa sababu hii redio ndio msemaji Mkuu wa Serikali. Kuna watu wasikie habari katika redio nyengine zote bado watakuwa wana wasi wasi kama hawajaisikia hii ya serikali. Kuna watu wasikie tangazo la TV nyengine yoyote ile lakini bado watashindwa kuamini kama hawajasikia ile ya serikali. Kwa hivyo, matangazo ya serikali yanahitajika yawe ya haraka na yenye ufanisi na yenye ukweli wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, ili kufikia hatua hiyo;

- Je, hii redio yetu na *TV* yetu wafanyakazi wake wanawezeshwa kufanya kazi zao vizuri?
- Je, wamepata mafunzo ya kutosha juu ya kazi wanazozifanya?
- Je, wameelimishwa uzuri namna ya kutafuta habari na kuzitoa?

Kwa hivyo, ili wafanye kazi zao lazima wawe na elimu ya kazi yao wanayoifanya. Wawezeshwe vizuri kukabiliana na matatizo mbali mbali ya kazi zao na ili waweze kutoa huduma nzuri kwa jamii. Lakini si dhani kuwa haya yapo. Kwa sababu mfano mzuri na mdogo ni hawa vijana ambao wanahudumia humu ndani, miaka mitano yote. Kila anayesimama anawasemea hawa juu ya posho lao la kukaa humu na serikali hata haina habari. Lakini sidhani hata kidogo kuwa posho hilo

wamepatiwa. Sidhani kwa sababu nimemsikiliza vizuri Mwenyekiti wa kamati alivyokuwa akiwasilisha ripoti yake ya Kamati.

Hivi jamani kuna ugumu gani wa kuwapatia posho vijana hawa ambao wanafanya kazi kubwa, ngumu na nzito. Wafanya kazi wenu wenyewe, msiwe wakaidi kiasi hicho. Kuna msemo wa kiswahili unaosema "Mcheza kwao hutunzwa". Watunzeni hawa wanafanya kazi nzuri kwani;

- Kama sio wao watu wasingelisikia kazi inayofanywa hapa Barazani.
- Kama sio wao watu wesingeona kwamba sasa hivi Barazani hamna watu.
- Kama sio wao aliyekuwa hana *TV* asingesikia kwamba sasa hivi kuna mtu anazungumza, lakini redio ipo wazi watu wanatusikia, televisheni zipo wazi lakini bado tumekuwa wagumu, wakaidi wa kuwahudumia na kuwapatia posho ya kazi hii kwa sababu hii ni kazi ya ziada sio kazi ya kawaida.

Kwa hivyo, ningeomba wizara kwa hali yoyote ile vijana hawa wapewe posho zao na sio Sh. 5,000/= muwape posho hasa kwa sababu wanafanya kazi kubwa na nzuri, bila ya wao sisi tusingesikilikana na watu huko nje.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vipindi kadhaa ambavyo vinatayarishwa vya habari, taarifa za wizara mbali mbali na nyengine ambazo zinatoa matangazo kama za maonesho. Ningeomba kwa taarifa zote ambazo pengine za kimichezo zinazooneshwa, zifanyiwe uhakiki kabla ya kutolewa na kutangazwa, ili isije ikakiuka utamaduni, silka zetu za Wazanzibari. Kuanzia redio yetu, *TV* yetu, za watu binafsi na hizi *Radio FM* ingawaje hizi *Radio FM* nyingi zinatoa zaidi taaluma za kidini na nyengine ni mambo ya kawaida.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeiomba wizara hii iitazame hii sekta ya habari kwa jicho la huruma ili wafanyakazi wake wawe na moyo zaidi, uzalendo wao uwe mkubwa zaidi, kwa kweli ni wazalendo kufanya kazi katika mazingara magumu na ikawa wanafanya bila kuchoka. Hawa hawajatutuma hata siku moja kwamba tusemeeni, wala hawajatunon'goneza.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja nilikuwa natembea pale mjini nikamuona kijana mmoja anatoka pale *TV* mimi simjui lakini yeye ananijua, akanisalimia akanambia hunijui mimi mtu wa *TV*, ehe naam, unatoka kazini, ndio, unakaa wapi, mbali kidogo, gari ya kwenda nyumbani unayo, aa napanda daladala kwa wakati huo na ni mwaka huu si mwaka jana, vijana wengine wanatoka usiku gari ya kuwarejesha majumbani hakuna na ni wanawake, ni hatari kidogo.

Lazima tuwafanyie utaratibu wa kuwarudisha makazini hasa wale ambao wanaingia usiku au wanatoka usiku kurudi majumbani, sio wakakae barabarani kungojea daladala kama anaenda Jan'gombe anasubiri ya Jan'gombe, kama anakwenda Bububu anangojea ya Bububu. Wizara itayarishe au Idara inayohusika iwatayarishie usafiri hawa watu.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye sehemu ya utamaduni, kuna utamaduni wa mambo ya kale ya athari zilizobakia katika maisha ya zamani; wakati wa utumwa na vyenginevyo. Kuna majengo ya asili ya zamani, wizara hii au idara inayohusika bado haijafanya vyema katika kuvitafuta vitu hivi.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, pale Mgagadu palikuwa na bwana mmoja alikuwa ana watumwa na kwa kipindi kirefu ile minyororo ambayo ilikuwa wale watu wakifungwa, ilikuwa ipo. Maeneo kama yale yalikuwa yanastahiki kutunzwa, ili ile historia isipotee. Kule kwetu sehemu fulani Mtule kulikuwa na msikiti mkongwe, msikiti haupo tena lakini mpaka leo kisima kipo, maji yamo lakini hakitumiki. Mambo kama yale ilikuwa yahifadhiwe, iwe kama ni mambo ya historia yaonekane, lakini pole pole yanaanza kupotea.

Kwa hivyo, baadae itakuwa vipi, watu wa zamani waliishi, majengo yake yalikuwaje yatapotea kwa hivyo tamaduni hizi zisipotee Wizara hii iwe na jukumu la makusudi la kujaribu kuvitafuta vituo mbali mbali ambavyo vya kiutamaduni wa zamani watu walivyokuwa wakiishi.

Mheshimiwa, kwa upande wa utamaduni wa ngoma, ngoma za asili takriban zote zimepotea ingawa sihimizi kuwa ngoma zifufuke aa, lakini tunaimarisha ngoma za kisasa na zile za kiasili zinapotea. Kulikuwa na ngoma ya msondo inapotea, umundi na pungwa mambo kama haya ya kiutamaduni wa kiasili katika mambo ya ngoma. Katika nyimbo zilizokuwepo zamani kwa sababu nyimbo zote huwa zinalenga kitu fulani, lakini nyimbo zetu za kileo vimeweka vitu bayana.

Nyimbo zote Mhe. Mwenyekiti, zina siri fulani ndani yake, pale waswahili waliposema vin'garavyo vyote si dhahabu vyengine shaba navyo hughilibu, pale haijakusudiwa dhahabu kuna kitu ambacho kimefichwa lakini waimbaji wa leo hawafichi wanasema moja kwa moja. Kwa hivyo huu utunzi wenu wa kileo ni utunzi ambapo unakwenda na maadili kwa zamani huwezi ukajua mpaka uwe ni msomi au uwe ni mhakiki wa lugha, ndio ujue alaa huu wimbo umekusudiwa hivi. Wa leo hautaki tochi uko moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, turudisheni utamaduni wa kiasili katika mambo yote ili hadhi na haiba yetu irudi kama ilivyokuwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika utalii; hii nitasemea katika mfumo nitakao mimi tu. Keshokutwa ni Ramadhani nchi hii wenyewe tunasema utalii ndio njia yetu kuu ya uchumi zamani ilikuwa karafuu, mbata au nazi, pilipili hoho; leo imekuwa utalii mnavyosema wenyewe ndio unaongoza inafatiwa na karafuu, sina hakika kuwa ni kweli lakini iko hivyo.

Huu utalii unaimarishwa zaidi na wageni; wageni wanaokuja wanakuja kwa tamaduni zao, silka zao na mavazi yao. Keshokutwa Mhe. Mwenyekiti, tunafunga tunakwenda sokoni na sina hakika kuwa huu ni msimu wa utalii au vipi. Hawa wageni kulingana na kuwa tunaheshimu haki za binaadamu watakuwa hawafungi, wanakula, wanaovuta wanavuta, wanatembea na nguo zao wanavyotembea nazo, lakini sisi tumefunga na jicho halina pazia.

Huu utalii wetu kwa mwezi huu Mhe. Mwenyekiti, utabatilisha Ramadhani za walio wengi. Kwa sababu kufunga si kukata kula na kunywa tu, kuna mengine. Je, katika mwezi huu Serikali ina mipango gani ya kudhibiti hii hali, ili angalau kwa mwezi wa Ramadhani iwe hatuoni watu kula ovyo, hatuoni kutembea bila ya nguo za stara na kadhalika. Lakini tena na sisi kwa upande mwengine tunahitaji mengi kwa Mwenyezi Mungu, sijui tuna utaratibu gani wa kuweza kudhibiti angalau huu mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, wengine walikuwa hawajazaliwa, ilikuwa Mzee Karume alikuwa akimkutia anakula, anatembea sivyo mwezi wa Ramadhani ilikuwa anamuweka mpaka Ramadhani nyengine. Kwa hivyo, kila mtu ilikuwa anakuja Zanzibar akiwa anafuata silka za Wazanzibari zilivyo. Zamani ilikuwa hizi ndege ndogo ndogo haziko, ilikuwa kuna ndege kubwa hizi ambazo zina watu wanaitwa *air hostess* na aghlabu wale wanakwenda *half naked*, lakini wakija Zanzibar ama hatoki kwenye ndege na akitoka japo kanga anavaa kama shuka lakini lazima afuate mila, silka, desturi za kizanzibari. Leo kwa kuheshimu haki za kibinaadamu kwa kila mtu ana uhuru, haya yote hayako tena.

Kwa hivyo, ili kuweza kuuenzi utamaduni wa Zanzibar na silka zake lazima kuna mambo yachukuliwe hatua za kisheria, kama hakuna tuwekeni sheria, lakini hii nchi isiwe kuwa kila mtu anafanya anavyotaka tu, kila mtu anatembea anavyotaka tu. Hatimae vijana wetu haya yote wanaiga na tunashindwa kwa wazazi hata Serikali kuona kuwa huu mwendo ambao vijana wetu wanakwenda si mzuri.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ina jukumu kubwa sana kwa sababu mambo ya utamaduni yamo katika wizara hii na utamaduni si ngoma na maonesho tu pamoja na mavazi, tabia, kuheshimu dini za watu, kuheshimu mambo mbali mbali, mtu kuja akala mchana dini yetu hajaiheshimu. Mtu akija akatembea hana nguo vyema, dini hajaiheshimu na sisi tunatoa macho tu kwa sababu tunapata pesa.

Ningeomba kwa hivyo, *at least* kwa huu muda wa siku chache zijazo kuanzia keshokutwa kuna baadhi ya mambo yachukuliwe hatua, ili funga zetu ziende vizuri na salama isiwe ni watu ambao tumejizuia kula na kunywa lakini ikawa kumbe hatukufunga.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kuhifadhi kumbukumbu, hili ni jambo muhimu sana, Mhe. Mshimba, hapa kamtaja Mhe. Ali Mzee, kuwa na kumbukumbu, kahifadhi mambo mengi na ni kweli. Mimi nikikwambia kuwa nilisoma *form I* mwaka 1967 wewe hujazaliwa mabuku yangu ya *form I* mpaka leo yapo wala hayajaliwa na mchwa. Lakini mwanangu ambaye yuko *form V* leo buku la *form IV* hana. Nina picha niliyopiga nikiwa Paunia Mtambile miaka kadhaa nyuma tokea Paunia, wewe ulikuwa hujazaliwa. Sasa mtu *simple* kama mimi kwa kumbukumbu zangu binafsi ninazo lakini ukenda Serikalini mara nyengine unatafuta kumbukumbu zako zinashindikana kuonekana, huu ni msiba mzito kwa Serikali. Kama watu binafsi wanaweza kutunza kumbukumbu zao, lakini Serikali kama Serikali ikawa kumbukumbu zinashindikana kupatikana kikamilifu. Kwa hivyo, ili tuende vizuri lazima tuwe na mfumo wa kutunza kumbukumbu zetu, tuwaelimishe wafanyakazi wetu namna ya kutunza kumbukumbu, ili ziweze kutumika leo, kesho na baadae. Vyenginevyo kila siku itakuwa tuna kumbukumbu ya leo na kesho tu, ya juzi na jana itakuwa imepotea.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani dakika 5 ulizonambia zimamalizika, nakwambia ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza na mimi nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* ambaye ametujaalia uhai, tukaweza kukutana hapa jioni hii katika kutekeleza majukumu yetu.

Pia, nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe Mwenyekiti, kunipatia na mimi fursa hii nikaweza kusema machache katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo katika bajeti yake hii ya mwaka 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe fursa hii kumshukuru Waziri na Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kazi kubwa na ngumu ambayo wanaifanya katika wizara hii. Kwani wizara hii ndio kioo chetu cha jamii ambacho tunategemea kujifunza mengi kupitia wizara hii, kwa hivyo na wizara bado ina changamoto nyingi zinazoonekana kuna ukosefu wa vifaa basi ndio maana nawapa pole kwa kazi hiyo ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika ukurasa wa tatu ambapo kuna sekta ya habari. Sekta hii ni muhimu sana ndio inayowapelekea wananchi wetu kujua habari mbali mbali katika nchi yao na nje ya nchi yao. Lakini ndani ya sekta hii tuna wafanyakazi muhimu ambao tunao katika Baraza letu hili wanafanya kazi moja kubwa kabisa na wenzangu waliotangulia wamesema na mimi nachukua fursa hii kuelezea vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu waliomo humu ambao wanashughulika na kazi hizi za habari wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi ngumu lakini pia katika mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya wafanyakazi hawa nadhani ripoti hizi ambazo zinakusudiwa kutoka kuwafikia jamii, ili waone basi wawakilishi wao jinsi gani unawawakilisha katika Baraza hili, lakini niseme bado wafanyakazi hawa wanakabiliwa na changamoto kubwa ambayo inaonekana Mhe. Waziri, hili lazima tulizingatie kwa kukosa maposho wafanyakazi hawa na jinsi ya utaratibu wa kazi yao ilivyo, si jambo zuri.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi hawa wanahitaji lishe bora kutokana na kazi yao, ili wawe na stamina nzuri ya kusimama pale kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, tunapowanyima maposho wafanyakazi hawa wakakosa na wao kujikimu katika mahitaji yao mbali mbali tuone hatuwatendei haki wafanyakazi hawa kama inavyopaswa kwa wafanyakazi au kwa mwanaadamu mwengine yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, nayasema haya na labda ninukuu Katiba inasemaje kuona wafanyakazi hawa na wao wana haki kama walivyo wafanyakazi wengine.

Mhe. Mwenyekiti, ibara ya 21(4) kinaeleza:

> "Kila mtu, bila ya kuwepo ubaguzi wa aina yoyote, anayo haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake na watu wote wafanyao kazi kulingana na uwezo wao watapata malipo kulingana na kiasi ya sifa za kazi wanayoifanya".

Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa nimetangulia kueleza wanafanya kazi kubwa, si busara sisi kuwanyima haki yao ya msingi ambayo ingeweza na wao wakajikimu katika maisha yao. Hawa ni watu wanyonge tuwafikirie, pengine kutokuwalipa sisi wanakopa huko mitaani ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kila siku, ni lazima tungewafikiria katika hali ya kuwapatia haki yao ya msingi kama wanavyopatiwa wengine.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na sekta hii ya habari kama ilivyojieleza katika kutekeleza majukumu yake ya mwaka 2015/2016 inaeleza, sekta hii kuwapatia wananchi huduma bora za habari na kwa wakati, kwa njia ya magazeti, redio na televisheni.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli habari hizo tunazihitaji tuzipate kwa wakati hasa ukizingatia hivi sasa mambo ya utandawazi yalivyo, si vyema jambo likawa limetoka hapa nchini kwetu ikawa sisi tunapata kiporo kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, bado katika sekta hii niseme kuna changamoto kubwa ya kupata habari kwa wakati, na pia bado mimi nieleze hapa habari au vipindi ambavyo tunavipata bado ni vipindi vinavyojirejea kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, si busara kipindi kujirejea hicho kwa hicho kinachosha na kinafanya kututia uvuvi wa kuangalia televisheni yetu, na sisi ni wadau wakubwa wa kuona chombo chetu hiki ndicho ambacho tunakitegemea kwa kupata habari za ndani ya nchi yetu kwa wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, habari zinajirejea rejea sana, kipindi utakisikiliza tangu wiki tatu zilizopita, utakuta bado kinarejea hicho kwa hicho. Mimi naomba kama ikiwa bado hatujapata kipindi chengine cha kuweka pale, basi bora turejeshe hata kipindi chengine, ili kile tukiondoshe pale kwanza angalau tubadilishe mandhari ya kuweza kuleta usikilizaji mzuri kwa wale wasikilizaji au wanaoangalia vipindi vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, hii changamoto tujitahidi ili iweze kutuondokea, kuhakikisha *TV* yetu na sisi inakwenda na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika sekta ya utalii. Kwanza napenda nitoe pongezi za dhati kabisa katika sekta hii kwa kuona kamisheni imefanikiwa katika kukamilisha jengo lile la ghorofa na ukuta ambao unaleta haiba nzuri. Hili ni jambo zuri na ni jambo la kupigiwa mfano. Pia ni hali moja wapo ya kudhibiti yale majengo yetu, jambo hili tunalipigia kelele kila siku kwamba kulijenga jengo halafu ukaliwekea ukuta. Ni jambo ambalo litaepusha migogoro siku za baadae, kwa sababu eneo lako lote utakuwa umelidhibiti na utakuwa huna ugomvi na mtu yeyote.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika sekta hii bado ile dhana ambayo imekusudiwa utalii kwa wote, bado haijaweza kupatikana. Bado katika sekta hii ambapo tunategemea ajira zetu kutokana na mahoteli yetu yaliyopo. Hivyo bado hatujazingatia kuwapa kipaumbele vijana wetu katika kuwaajiri na bado ajira zinaendelea kutoka kwa wageni zaidi kuliko wale vijana wetu wazalendo.

Mhe. Mwenyekiti, zamani kulikuwa na malalamiko na yalikuwa yanakubalika, tulikuwa hatujasoma kabisa mambo ya sekta ya utalii. Lakini kwa sasa changamoto hii tumeweza kukabiliana nayo na vijana wetu wamesoma kwa sasa na wanaweza kukabili katika kuendesha ajira katika sehemu ya utalii, kwa sababu sasa elimu tayari wanazo. Lakini, wenzangu wametangulia kusema na mimi napenda nirejee kusema hilo.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto kubwa zinawakuta vijana wetu katika mahoteli, bado niiombe serikali kufanya utafiti wa kina ili waone wafanyakazi ni nini wanatendewa katika mahoteli yetu ambayo yanafanya kuwarejesha nyuma wafanyakazi wetu.

Kwanza wanapatiwa kazi kubwa lakini kipato ni kidogo. Kwa hiyo, ningeomba sana katika sekta hii tungeangalia na tungewaangalia sana vijana, ili wakaweza na wao kupata ajira tukapunguza sisi serikali, changamoto ile ya ajira ambayo inatukabili kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, niende na mchango wangu katika ukurasa wa tano ambapo kuna sekta ya utamaduni.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tuna utamaduni wetu; utamaduni ambao unakubalika na unajenga heshima kubwa katika nchi yetu na pia kuitangaza nchi yetu katika nchi nyengine kupitia utamaduni wetu huu. Utamaduni huu unapendwa na wenzetu wa nchi za nje, ni jambo la kujisifia sana. Lakini bado hatujaenzi utamaduni wetu ipasavyo na tunahadaika na kufata tamaduni za nchi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, kufuata tamaduni za nchi nyengine maana yake tunaiacha nchi yetu kama haina utamaduni, kuiga tamaduni ambazo sisi hatupaswi kuwa nazo kwa hiyo tunapoteza ile sifa, umaarufu na heshima kubwa ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, utamaduni wetu sisi unaonesha hata mtu ukikutana nae tu basi anapata moyo wa kukuamini kutokana na vile ulivyo, kwa sababu anahisi ni mtu makini umetulia anakuona una busara, vile anapokuona tu ulivyo anafanya kujenga imani kubwa kutokana na utamaduni wetu. Vile vile utamaduni huu tungeujenga na kuuenzi vizuri, basi pia ingewajenga wajasiriamali kuweza kuwa na soko zuri la bidhaa katika utalii wetu na hali ambayo ingeweza kuwaongezea wao kipato.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tuna mambo mengi katika utamaduni wetu wa Kizanzibari kama tulivyoona niseme nichukue mfano mmoja tu wa karafuu ambayo tunayo.

Mhe. Mwenyekiti, karafuu zao hili kwa kuliingiza katika utamaduni wetu linaweza kutupatia sifa moja kubwa, kwa sababu karafuu ina sarifiwa katika mambo mbali

mbali. Leo kunatengenezwa sabuni ambazo zinatokana na karafuu kwa hiyo tungeweza kutengeneza hizi na kuzipatia soko na tena zina manufaa makubwa. Tungeweza kuzitengeneza na kuwapatia wajasiriamali masoko na tukaeleza faida zake ambazo zinapatikana kwa kutumia sabuni hii, basi wajasiriamali wangeweza kukuza kipato kupitia utalii wetu uliopo nchini.

Mhe. Mwenyekiti, lakini karafuu pia huwa inatengenezwa madongo na kuna *massage* ya karafuu yanayopatikana kwa hakika ingeweza kutumika basi lazima ingekubalika, kwa sababu karafuu inaondosha taka katika mwili wa mwanadamu, lakini karafuu pia inanyoosha mishipa na kumfanya mtu kuwa *fresh.* Kwa hiyo, mwili wake unakaa sawa na pia karafuu inaondosha uchovu katika mwili.

Kwa hiyo, karafuu hii tungeweza kuitumia vizuri tukaieleza katika kutangaza utalii wetu wenzetu wangezidi kuvutika kwa sababu tuna vitu vizuri, lakini bado hatujavinadi vizuri katika utalii.

Mhe. Mwenyekiti, nirudi nyuma kidogo niliacha *point* yangu moja katika utamaduni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, utamaduni ambao tunao nilitaka niueleze pia tungeweza kufata utamaduni. Jamii yetu pia mimi naishauri kwamba turudi katika utamaduni wetu wa zamani. Kwa sababu utamaduni wetu wa zamani ulionesha pia kupunguza hizi talaka za kiholela ambazo zinaonekana hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, utamaduni uliokuwepo uliweza kutoa elimu hii ya utamaduni wetu tangu mtoto anapoposwa mpaka kufika kuolewa, alikuwa anaweza kupatiwa elimu kubwa ambayo ilikuwa inamjenga jinsi ya kwenda kuanza maisha anapofika kwake.

Mhe. Mwenyekiti, kurejesha utamaduni huu ambao ungeweza kutujenga na jamii yetu ingeweza kujengeka vizuri, naishauri sana jamii kurejea katika utamaduni wetu na tuachane na mila hizi na desturi za kuigaiga ambazo zisingetujengea sifa nzuri katika nchi yetu, kwa sababu kuiga siku zote uige jambo lilokuwa zuri lakini jambo ambalo linakutoa katika mila na silka zako, basi jambo hilo sio zuri kuliiga.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu katika Baraza la Sanaa. Kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza sana wasanii wetu kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kuielimisha jamii yetu. Lakini pia niseme Baraza hili lina kazi kubwa ya kuchunga sanaa yetu na kuiona bado sanaa tunayoitoa inaendana na mila, silka na desturi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari bado zipo sanaa ambazo zinazotolewa badala ya kuelimisha, mimi naona zinaweza zikaongeza matatizo. Kwa hiyo, ndio maana naliomba hili Baraza la Sanaa liweze kuchunga na kuchuja, ili sanaa itakayotoka pale iwe ni bora ambayo itaweza kuisaidia jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, siku hizi mimi nasikia kuna mchezo mmoja unatolewa, mimi kwa upande wangu sijui wenzangu ningeomba serikali iupitie na ichunguze vizuri, uko mchezo unatolewa ambao unahusiana na mambo ya udhalilishaji. Mimi nikitizama ile mantiki nzima inaonesha kama inachochea lile jambo na badala yake sisi tunategemea lipungue. Naomba sana huu mchezo mimi sijauzingatia lakini unaelezea katika mambo haya ya udhalilishaji wa kijinsia. Kwa hiyo, naomba ule mchezo ungeangaliwa vizuri, maana yake dhana nzima hapa tunataka tuiokoe jamii kutokana na mambo machafu na tuielekeze katika mambo mazuri. Kwa hiyo, naomba sana hili serikali iliangalie katika kukifatilia hiki kipindi, ili wajue kama sanaa inayopatikana basi inaelimisha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini bado katika sanaa nataka nirudi katika ile sheria yetu ya mavazi ambayo tumekuwa tukikukera hapa muda mwingi. Sheria hii kwamba tunaihitaji ili basi wasanii wetu hawa na wao wangeweza kubanwa na sheria hii na wangeweza kuvaa mavazi ambayo yanaendana na mila na utamaduni wetu, wakaweza kuonesha sanaa zao katika hali nzuri kabisa jambo ambalo lingejenga heshima na sanaa hiyo isingemchukia mtu yeyote, bali angefurahia na wala isingemfanya labda mzazi mmoja kuondoka akakimbia akawaacha watoto wakiangalia. Kwa hiyo, mimi nasisitiza bado mavazi yaendelee kupatikana mavazi yaendelee kupatikana mavazi ambayo yatakuwa yastara, mazuri ambayo yataweza kujenga mila na utamaduni wetu kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kulielezwa katika ripoti ya Mwenyekiti kama kuna taasisi za serikali hazilipi fedha katika Wizara hii ya Habari jambo ambalo linaikwaza wizara katika kujipapatua katika shughuli zake nyengine. Mhe. Mwenyekiti, mimi nieleze hizi taasisi ili wao wafanikiwe na yao basi lazima waelewe kama kuna na wengine na wao wanataka wafanikishe yale ya kwao. Kwa hiyo, wao tunapowatolea matangazo yao maana yake huwa tunawafanikishia yao, kwa hiyo na wao ni lazima warejeshe fedha ili wizara hii nayo iweze kutekeleza yale ya kwake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu ulikuwa huo mdogo lakini nilisema nichangie japo kidogo katika wizara hii ili kuhakikisha bajeti hii na naomba nitamke kwamba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kwa wakati huu wa jioni kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Mhe. Said Ali Mbarouk.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya yote niseme nampongeza Mhe. Said Ali Mbarouk pamoja na watendaji wake wote ambao wametuandalia bajeti hii na kuweza kuichangia kwa wakati huu wa jioni.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na sehemu ya utalii. Kwa kuwa utalii umekuwa kupitia sekta hii ya utalii, lakini bado serikali haijawa makini kwa wananchi wetu kuwaendeleza na kudhalilika siku hadi siku kutokana na baadhi ya mambo yanayofanywa katika fukwe.

Mhe. Mwenyekiti, mambo haya yakiwemo uharibifu wa mazingira kwa mfano niseme mazingira sasa hivi ni kitu ambacho cha hatari sana. Kwa mfano, katika fukwe zetu hizi kimoja kinachokuwa ni tatizo na katika mazingira ni kujengwa kwa mahoteli kiholela au kienyeji na hapa inatokana na kufanyiwa tathmini ya mazingira jambo ambalo linaathiri hata viumbe vya baharini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano niseme kasa, kasa sasa hivi wanakosa sehemu ya kutagia na mwa kutotolea watoto wao kutokana na mazingira kuharibiwa na kutokana na ujenzi wa kiholela ambao unajengwa sasa hivi, na kasa ni miongoni mwa vivutio ambalavyo tunategemea sana kwa watalii. Mhe. Waziri, naomba jambo hili ulielewe sana kwa sasa hivi, kwa wakati tulionao huu tutakosa hata viumbe katika bahari yetu.

Pia, nije katika sekta ya utamaduni; nianze na sanaa moja ya kitu muhimu katika jamii ni sanaa, lakini chakusikitisha sana sanaa nyingi zinazochezwa hivi sasa zinakosa mafunzo yaliyokuwa mazuri. Tukiangalia hasa watoto wetu sasa hivi wengi wanapocheza sanaa zao huwa wanajikamata katika sehemu zao ambazo hazitajiki, hushusha suruali zile, wakapandisha, hili ni tatizo kubwa sana na hutokana na kuwafundisha wengine ambao watoto wanaranda mitaani, utamkuta mtu kapandisha suruali hiyo; hili ni tatizo kubwa sana.

Kwa hiyo, sanaa zetu zina matatizo na watoto wetu ambao wanaonesha sanaa pia wanawafundisha watoto wa mitaani kuchuchua suruali. Suruali inakamatwa sehemu ya siri, anatembea tena anadunda. Hiki ni kitu kibaya sana, naomba ukielewe.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikija katika sehemu ya sekta ya michezo; kwanza nampongeza Mhe. Waziri, sana kwa hatua kubwa atakazozichukua kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa kufanya matengenezo ya viwanja vyetu hivi vya mipira.

Kiwanja cha Amani, Gombani na Kiwanja cha Mao-Tse-Tung na hivi sasa tayari tunakiona Kiwanja cha Mao-Tse-Tung kinaanza kutengenezwa.

Mhe. Mwenyekiti, niseme nimpongeze Mhe. Waziri, kwa hili moja kati ya vivutio kwa wananchi ni kuangalia michezo hususan mchezo huu wa mpira wa miguu na kufanya mazoezi na kuondosha maradhi mengi yanayotukabili hivi sasa. Nampongeza Mhe. Waziri kwa kufanya juhudi hiyo ya mwaka 2015/2016 kujenga viwanja hivyo ambavyo hata na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa wale watakaorudi, naamini watakwenda katika viwanja kufanya mazoezi.

Mhe. Mwenyekiti, pia niseme ziko timu zetu hizi za wilaya; timu hizi ndizo zinazozaa timu kubwa za taifa. Timu hizi niseme kwamba zinashindwa kujiendeleza kutokana na kushindwa kusaidiwa, Mhe. Waziri naomba timu hizi azifuatilie sana na kuweza kuzipatia misaada ili ziweze kujiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, timu nyingi hivi sasa zinavunjika moyo, ukija katika michezo yao ya wilaya na hutokea sana migogoro na migogoro hii kutokana na kutokuwawezesha. Naomba Mhe. Waziri hili alielewe na timu zetu hizi nazo zipewe kipaumbele ili ziweze kujiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchezo huu wa mpira wa *football* moja kati ya michezo inayopendwa sana ni mpira huu wa *football.*

Kwanza ziko aina mbili za michezo na katika mchezo huu moja ni mpira huu ambao huchezwa na wanawake na wanaume, naomba mpira huu upewe kipaumbele hususan ukiangalia hawa wanawake na wanaume mwanamke kucheza mpira wa *football* si jambo dogo na ni jambo ambalo linakuwa la *fanny* kumuona mwanamke anacheza mpira wa *football* na ikawa bado serikali hawajawaangalia angalau kuwapatia timu zile vifaa vya kuweza kuchezea.

Pia, katika aina mbili hizi bado tuko nyuma kutokana na sababu zifuatazo; kwanza niseme sijui kwamba bajeti haikujikita katika mchezo huu wa mpira wa miguu, lakini vile vile kuna ukosefu wa makocha. Makocha wetu bado hawana elimu na taaluma, nimuombe Mhe. Waziri hili alione ili kutuletea makocha ili waweze kufundisha michezo hii kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, pia, katika sekta hii ya utamaduni niseme sekta hii ni sekta ya kupewa kipaumbele zaidi, lakini tukiangalia sasa haipewi kutokana na kwamba tunakwenda na wakati. Hapo nyuma utamaduni ulikuwa ni mzuri sana hata ukiendelea vijijini kulikuwa na ngoma zetu za asili, kulikuwa na michezo ya ng'ombe, kulikuwa na michezo ya msondo, ngoma za gonga, lakini sasa hivi michezo hii yote haipo na ngoma zetu hizi hatujui kwa nini na ukiangalia kwa hivi

sasa ingekuwa kivutio kikubwa kwa nchi yetu. Ningeomba michezo hii ikaimarishwa ili kuweza kurejewa katika mitaa na kuweza kuoneshwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika sehemu ya soka la wanawake; ni kivutio kikubwa na sio hapa Zanzibar tu, lakini hata sehemu za Uarabuni, mchezo huu wanawake unapendwa sana. Namuomba Mhe. Waziri mchezo huu uchukuliwe hatua za makusudi ili uweze kuimarishwa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika tamaduni bado nasema tamaduni bado ni kivutio ambacho kinatuvutia wananchi na utamaduni hivi sasa tumeuacha. Tukiangalia utamaduni wetu hivi sasa tumeuacha toka enzi na enzi na sasa hivi tunakwenda na mambo ambayo hayafai kabisa. Kwa sababu tukiangalia watoto wetu sasa hivi bado hawana utamaduni wa Kizanzibari.

Zamani utamaduni wetu ilikuwa mtoto anakuwa na heshima kubwa sana anapokuwa anafunzwa na watoto hawa ilikuwa tayari wanafunzwa ndani wanawekwa muda wa wiki au wiki mbili yuko ndani anafundishwa tu, lakini sasa hivi mtoto yule hata ile heshima ya mafunzo hana.

Mtoto anapoolewa kufika kwake anakuwa kumpa mafunzo ni tabu kwa sababu hakupata mafumzo ya kiasili, lakini enzi zetu ilikuwa mtoto anafundishwa kwa muda wa wiki moja au mbili na hatimae anatoka nje mtoto yule anakuwa na heshima, lakini hivi sasa niseme kwamba hili ni tatizo kubwa sana na namuomba Mhe. Waziri tuwe makini na sisi wazee kuwalea watoto wetu, hili si la Mhe. Waziri ni letu sisi wazazi. Iwapo sisi wazazi tutakuwa makini na kuwafundisha watoto wetu, naamini mtoto atakapokuwa anatoka nje baada ya mafunzo yale atakuwa na heshima nzuri na anapokwenda kwake atakuwa na heshima nzuri kwa mumewe na vitendo vyote anavyovifanya vya ndani vinavyotakiwa vitakuwa ni vizuri.

Hivi sasa niseme kwamba utamaduni huu umeondoka kutokana na mafunzo ambayo sasa hivi hatunayo na mafunzo haya hatuna kwa sababu tunakwenda na wakati, tukisema kama tunakwenda na wakati tunaharibikiwa. Naomba hili tujitahidini wazazi pamoja na walezi turudishe asili yetu ya Kizanzibari kuwafundisha watoto wetu na kuwapa malezi bora, ili watakapofika makao wawe na heshima iliyo nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nakushukuru, ahsante.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima katika Baraza lako tukufu jioni hii ya leo. Nakushukuru wewe pia kunipa nafasi hii

ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2015/2016.
Pia, nimpongeze kwa sana Mhe. Naibu Waziri kwa juhudi zake kubwa sana kwa wizara hii. Pia nitoe pongezi kwa watendaji wote wa wizara hii kwa juhudi zao kubwa hasa katika Sekta ya Utalii ambayo ni uti wa mgongo kwa nchi yetu hii.

Vile vile, nimpongeze sana Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa juhudi zake kuongoza kamati hii na kwa ripoti yao nzuri sana waliyoisoma hapa, na wajumbe wake wote kwa kazi yao waliyoifanya na ya umakini mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwenye ukurasa wa 15 kifungu nambari 45 katika Sekta ya Michezo. Kwanza nataka niipongeze sana serikali kwa juhudi zake kubwa na kwa maendeleo makubwa iliyoonesha kwa mwaka huu hasa katika matengenezo ya uwanja wa michezo wa Amani, uwanja wa Gombani Pemba na kubwa kabisa nawapongeza sana serikali katika juhudi zao walizochukua katika uwanja wa *Mao-Tse-Tung* katika kuona kuwa uwanja ule uko katika hali mbaya na kutafuta wafadhili mbali mbali na hatimae kupata wananchi wa Jamhuri ya China, kutusaidia katika uwanja ule kujenga uwanja wa kisasa kabisa.

Kwa hivyo, mimi napongeza sana serikali pamoja na waziri kwa juhudi zake kubwa hizo walizoonesha mpaka kupata wahisani, wakatusaidia kujenga uwanja ule na sasa hivi naona uwanja ule uko katika hatua ya kuendelea kujengwa na umeshabomolewa kwa vizuri na uko katika hatua nzuri ya kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea hapa hapa katika sekta hii ya michezo. Kwa kweli serikali yetu inajitahidi sana katika kuonesha nia njema ya wanamichezo wetu kujitahidi kujenga viwanja kwa sehemu mbali mbali, ili vijana wetu kuweza kucheza mpira vizuri. Lakini la kusikitisha niseme hasa katika timu zetu hizi wanakosa wadhamini na mimi nasema kwa nini wadhamini tusiwaruhusu wakatusaidia. Tukiangalia mipira yetu ya Bara sasa hivi wadhamini ndio wanaendesha, wanaweka zawadi mpaka shilingi milioni mia moja mshindi wa kwanza anachukua, sasa sisi hapa tunashindwa changamoto hizo za zawadi ndio unakuta timu zetu hazina hamasa za mechi.

Ukipita uwanja wa Amani pale unauliza leo timu gani na gani inacheza utakuta ligi kuu lakini watu kidogo sio mpira wa kuhamasika ukakuta watu wamejaa kama zamani. Sasa hili mimi naona tatizo kubwa ni wadhamini tungewaruhusu wadhamini wetu hawa wanaotaka kujitolea katika ku-*support* huu mpira, waje na tuwaruhusu kwa sababu timu zetu hazina fedha.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine utawaonea huruma unakwenda kwenye mechi hata gari ya kwenda kutoka pale Miembeni ufike uwanja wa Amani basi usafiri wanakuwa hawana. Kwa kweli inatia huruma na inasikitisha timu kama ile kubwa siku ya kufika uwanjani ule usafiri wanakosa, siku nyengine wanakosa mpaka jezi za kuvaa kwenye mechi hizi, hata viatu wanakosa kutokana na kwamba hakuna fedha za kuweza kuwasaidia hata wafadhili wenyewe wanashindwa kujitolea kwa sasa hivi kama zamani walivyokuwa. Sasa hivi hamna wafadhili hao wa kusaidia michezo yetu hii hasa mpira wa miguu kujitolea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme jimboni kwangu mwaka jana nilifanya mechi ya jimbo tu, lakini niliweka zawadi nzuri kiasi ambacho ule mpira ulikuwa balaa mpaka tutafute askari kulinda ili fainali iishe salama. Kwa sababu kule kuhamasika na kila mtu anataka kuchukua zawadi ile, hata keshokutwa tarehe 17 mimi nimeanzisha ligi yangu tena, lakini nachezesha kwenye uwanja wa JWT pale Mwanyanya, naomba uwanja ule kwa sababu ya usalama na kwa kuwa mechi zile zinakuwa na hamasa kubwa kwa kutangazia zawadi nzuri, ili zile timu zetu zipate kuhamasika na kucheza mpira kwa nguvu zote kushinda ili kuonesha vipaji vyao. Tukiangalia sasa hivi mpira ni ajira, vijana wetu wakiwa watacheza mpira vizuri basi wanaweza wakaajiriwa katika sehemu mbali mbali.

Kwa hiyo, mimi namwambia Mhe. Waziri tuangalie sana suala la wadhamini tuwatafute sasa hivi, timu hazina wafadhili mameneja wenyewe wanakuwa hawana pesa, kuna pesa za kumlipa kocha, unataka kulipa madaktari, unataka kulipa vitu mbali mbali vya kuchezwa kwa mafanikio. Kwa hivyo, mimi naomba wafadhili tuwaangalie kwa upande mwengine tuweze kuwaruhusu waweze kutusaidia katika michezo yetu ya mpira wa miguu katika ligi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Sekta ya Utalii; kama nilivyosema mwanzo utalii ni uti wa mgongo hasa kwa nchi yetu ya Zanzibar, tunategemea karibu pato asilimia 25 ya nchi yetu kwa kupitia utalii. Katika biashara hii ya utalii, inatusaidia sana na siku baada ya siku pato hili linakua na naamini kwa umakini wa Mhe. Waziri anajitahidi sana kuimarisha sekta hii ya utalii. Tukiona kitabu chake mafanikio mengi tumepata kwenye sekta hii. Mimi nampongeza sana kwa juhudi zake hizo kubwa.

Pia, niipongeze sana serikali kwa juhudi zao kubwa kufikisha miundo mbinu hasa ya barabara kwenye mahoteli ya kitalii mashamba kote, barabara ni safi pia umeme ni wa uhakika napongeza serikali kwa juhudi zao hizo na kupata maji safi na salama. Kwa hiyo, serikali inajitahidi ili kuwapunguzia wale watalii yale makali ya uwekezaji wao ili waweze kuwekeza kwa urahisi. Kama kilivyo kitabu cha Mhe. Waziri hivi sasa tuna hoteli za *five star* karibu 16 ambazo daraja la juu kabisa, tukiangalia moja iko Mji Mkongwe Hyatt. Kwa kuwa hoteli ile mimi nimei-*round*

siku moja, lakini nilipoi-*roun* ndani hoteli ile nilisema kama siko Zanzibar. Ile hoteli imejengwa kupindukia kiwango, wale wawekezaji wamejitahidi sana na tuwasaidie kwa hali na mali, kwa sababu wametia fedha nyingi sana pale.

Kwa hiyo, mimi nawapongeza sana hoteli ile kwa juhudi zake kubwa na naamini mapato mengi yanapatikana kupitia pale kwa serikali yetu na kuweza kuokoa mambo mengi ambayo ni changamoto zinazotukabili sisi.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye kifungu cha 44(iv), kuimarisha miundombinu ya Hoteli ya Bwawani. Mhe. Waziri, mimi nampongeza sana kwa kuimarisha Hoteli ya Bwawani, kama ninavyojuwa hoteli hii ni historia ya wazee wetu waliojenga, tuseme ni hoteli ya kwanza Zanzibar kwa utalii na malengo ya Mzee wetu Abeid Amani Karume kuona Zanzibar inakuwa na hoteli za kisasa kama zile na sasa hivi hoteli ziko nyingi, lakini nia yake ilikuwa ndio kama hii iwe ya kimataifa kabisa. Mhe. Waziri pia nimpongeze kwa kuiimarisha hoteli ile kwa kujenga vyumba na kuviimarisha.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nimesikia kipindi cha nyuma Bwawani imetiwa *AC Salama Hall*, sasa hivi kuna *AC* nzuri nampongeza sana kwa juhudi zake hizo kwa kweli wanapiga hatua siku hadi siku. Pia akiangalia wafanyakazi wake Mhe. Waziri wajitahidi sana na hoteli ile japo wana changamoto, lakini wanajitahidi hoteli ile huioni kama imefungwa, iko *live* inaendelea ku-*survive* lakini wanatengeneza matengenezo mengi.

Mimi nawapongeza sana kwa kweli wanajitahidi hasa meneja pale anakwenda mbio kweli kweli, namshukuru sana na nampongeza kwa juhudi zake hizo na wakipewa wenyewe hizo nguvu Mhe. Waziri hawa watendaji wetu wanaweza kutufikisha mbali hoteli ile, maana yake wana moyo wa kuiendesha na kuiongoza.

Pia, kwa wale wafanyakazi wetu waliokuwa pale mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri wanakuwa na wasi wasi mkubwa na tunawaweka kwenye njia panda kwenye ajira zao, ile hoteli utasikia kila siku ishapewa mwekezaji, unaambiwa mwekezaji mwezi wa Disemba anapewa, keshokutwa utasikia mwekezaji mwengine anapewa, kwa kweli wale wafanyakazi hawajui hatima yao nini, hebu naomba Mhe. Waziri nia ya serikali ni nini kwa hoteli ile, kumpa mfadhili au kuendelea kuiboresha na kuiendeleza katika mazingira mazuri ili iweze kupokea wageni siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tunaona kwenye kitabu chake amesema kuimarisha miundombinu ya hoteli ya Bwawani. Kwa hivyo, kama kuna nia ya kupewa mwekezaji naomba aeleze waziwazi na wananchi wajue nia ya serikali, kama hawana nia hiyo basi iondoke dhana hiyo wajibiwe wananchi na wafanyakazi

wajue kama hoteli hii iko katika mikono yao na wawe na imani ya kuichunga na kuiendeleza hoteli ile iweze kufikia malengo mazuri ili kuwapokea wageni na kuweka ile haiba inavyotakiwa katika nchi yetu.

Suala jengine ni suala la utalii, ukitizama hoteli za kitalii nyingi sana hata juzi nilisema hapa zinawasumbua sana hasa hawa wafanyakazi wetu, wachuuzi wa samaki au bidhaa mbali mbali, wanapeleka bidhaa zao kwenye hoteli, lakini wananyanyaswa sana Mhe. Waziri na juzi nilisema hapa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Wachuuzi wanakwenda na samaki wao wanakopesha lakini sasa kulipwa inakuwa tabu.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana hawa wawekezaji kidogo waambiwe wanapopeleka hawa wanyonge wetu kitoweo wawasaidie kuwalipa kwa haraka kwa sababu na wao mtaji wao ndio uko hapo na sisi tunafurahi sana wao wakiwekeza hapa kwetu, Lakini hawa wavuvi wetu wakiuza mazao yao na sisi tunafaidika hivyo naomba sana waangaliwe sehemu ya kupata katika nchi yao ni hapa, wakulima na wavuvi pamoja na wafugaji.

Naomba sana waziri atie mkazo huo kwa wawekezaji wake anapowapa leseni hizi basi waambiwe wafahamishwe kwamba kuna wananchi wetu wanyonge wasaidiwe katika namna moja au nyengine, hata katika sehemu nyengine za mahoteli wasaidiwe pia miundombinu kama mambo mengine ya kutaka maji safi na salama wawekezaji wanafunga.

Leo ninavyosikia Pemba wamefunga kule kwa hivyo naomba wawekezaji kama hawa waangalie sana na wawasaidie wanyonge wetu wa nchi hii wasiwanyanyase, wamekuja kufanya biashara na sisi na wao wanategemea kupata fedha kutoka kwetu sisi. Kwa hiyo, nawaomba sana na wao watujali sisi wananchi tuliokuwa hapa wanyonge watusaidie vile vile tuweze kufanikisha yale malengo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa niende kwenye ukurasa wa 14 kwa kifungu nambari 42, Sekta ya Utamaduni. Katika kifungu cha 43(iii) kukuza kazi za sanaa pamoja na kuendeleza. Mhe. Waziri mimi nampongeza sana kwa kuona suala hili muhimu kukuza suala la sanaa na kuliendeleza katika nchi yetu ya Zanzibar.

Vile vile, katika 43(iv) Matamasha ya Maonesho ya Filamu na Muziki, pia wameona jambo hili ni muhimu sana mimi nampongeza sana kwa juhudi zake hizi. Kwa sababu matamasha haya na maonesho ndio yanavutia watalii kwenye nchi yetu. Kwa sababu watalii haya matamasha wanayafahamu sana na wanataka kuoa jinsi gani sisi tumejipanga kwa ajili ya muziki wetu na matamasha ya filamu yetu wanataka kuona tamaduni zetu ziko vipi kwani tofauti na zao. Kwa hivyo, hili

suala la muziki na filamu mimi nalipongeza sana kwa kuliona jambo la muhimu kwa vijana wetu na utamaduni wetu.

Pia, katika kifungu 43(v) kwenye ukurasa wa 14 Kufunga vifaa vya kisasa katika studio ya kurikodi na (vi) muziki na filamu. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri hata juzi nilisikia kwamba ile studio ya Rahaleo imeshakamilika sasa iko tayari kufanya kazi kurikodi a vifaa vimeshakuja na vishafungwa pale. Hii ni hatua kubwa kwani Zanzibar tuna vijana wengi wenye vipaji hasa vya kuimba hasa kwenye filamu kama alivyosema Mhe. Bi Panya Ali Abdalla wapo wasanii wetu wazuri tu, lakini wanashindwa kurikodi kutokana na fedha hawana, au kutokana na uwezeshaji wa kuweza filamu zao kuzitimiza wanashindwa kwa sababu ya fedha hawana mfukoni.

Mhe. Waziri, nampongeza sana lakini kwa vifaa hivi kuwa tayari na kuweza kurekodi. Lakini hawa wasanii wetu wakisha kurikodi hii miziki yao pahala pa kwenda kuimba kuonesha wameimba vipi wasanii wetu hii nikama sehemu ya ajira upande wao, wanakuwa hawana ukumbi maalum wa kuweza kwenda kuimba kuonesha kipaji chao kiko vipi, wakishakuimba *CD* zao wanaweka ndani watapeleka redio, lakini sehemu ya kwenda kuonesha zile nyimbo zao walivyoimba hamna.

Lazima hili liangaliwe kwa jicho la huruma kabis, kwa sababu wanapofanya matamasha yao na wao wanapata fedha, wakienda kuimba nyimbo zao, wakiimba kwenye tamasha lolote la muziki wao watalipwa pale kama shilingi milioni moja au laki tano, ili waweze kujikimu na wao nyimbo zao walizirekodi ziwe kama faida au kama ajira kwao wao. Sasa naomba sana Mhe. Waziri aangalie ukumbi gani hawa wakisha kurekodi nyimba zao watakwenda kuimbia wapi, au watafanya wapi haya matamasha yao? Naomba waziri aangalie.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 5 katika kifungu Nam. 14 sekta ya utamaduni; nije kwenye ukumbi huu wa Ngombe Kongwe. Ukumbi huu uko katika hali mbaya Mhe. Waziri kama nilivyosema tunajitahidi kuwatafutia miundombinu hawa wasanii wetu waweze kuimba, kurikodi, lakini kwenda kufanya lile tamasha lao wawape ukumbi ule, kwani ninavyojua mimi ukumbi ule umejengwa kwa wale wafadhili ili kufanywe tamasha la muziki pale hawa wasanii wetu waje kuimba ili wapate ajira na wapate fedha, leo wanakaa na nyimbo zao kwenye mifuko nyimbo itasaidia nini.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba ukumbi ule Mhe. Waziri sasa hivi uko katika hali mbaya unavuja, lakini nasikitika kwa nini hamuwezi kumpa mwekezaji akaweza kuutengeneza hata wasanii wetu wakiweza kuimba mpaka leo kuna ubinafsi gani pale. Mhe. Waziri, hebu nakuomba uangalie suala hili hii serikali yetu na hii nchi

yetu umejengwa ukumbi ule umekaa sasa hivi unaharibika mapaa yote yanavuja, yamepasuka pasuka hata hiyo *show* ikifanyika ikija mvua pale hakuna chochote sasa inakuwa ule ukumbi umekaa bure hauingizi chochote kwa serikali.

Mhe. Waziri, najua kwa umakini wake mkubwa anaelewa suala hili na yeye ni mdau mkubwa wa wasanii wetu hawa kuwafanyia mambo mazuri, naamini kabisa anaweza kusaidia ule ukumbi ukafanya kazi ili wasanii wetu wakaweza kufanya kama ajira yao na wakaweza kupata fedha na wakalipwa pale kwa kufanya matamasha yao mbali mbali ya Kimataifa na hata yetu ya Zanzibar zitawasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 13, kifungu Nam. 42…

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa umebakiwa na dakika tano.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante nitamalizia hizo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Sekta ya Habari; sekta hii ni muhimu sana kwenye nchi yetu tena habari ni kitu ambacho tunahitaji kila siku tukipate. Lakini mimi niipongeze sana serikali, nimpongeze Mhe. Waziri katika kifungu hiki Nam. 42 kuendeleza kufunga vifaa vya kisasa katika studio za *record,* vipindi vya kutumia mfumo wa *digital* kwa *ZBC*. Kwa kweli mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi yake hii kufunga vifaa vya kisasa itaweza kusaidia katika mfumo wa *digital* kwa kurusha vipindi vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nisikitike zaidi hapa kuna suala la *ZBC*. Kwenye ripoti ya kamati inasema kama inashindwa kujiendesha, haipati fedha za kujiendesha. Kituo kama hiki mimi nasikitika sana, kituo ni kizuri na kinaweza kujiendesha lakini sijui kwa nini mfumo unakuwa hivi hata inakuwa inashindikana kupata fedha hawa ili kuweza kuendesha kituo hiki bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe mfano mmoja kama mifano mingine imezungumzwa hapa. Mhe. Bi. Panya, kasema hawa ndugu zetu wanaokaa hapa wanashindwa kupata posho zao, kwa kweli inasikitisha. Mimi nimekaa hapa nasikia baridi natamani nitoke hata nje hii baridi ilivyokuwa kali, lakini sasa hawa ndugu zetu wanakaa masaa hayapungui matano humu ndani kwa hivyo hali yao inakuwa vipi.

Naomba tuwaangalie kwani kazi hii inaumiza na wao kazi yao kumtizama mtu huyu, hawana hata muda wa kukaa kusema kuzungumza au kupumzika wakimaliza huko kurikodi huyu, wakimrikodi na huyu; yaani wanajitahidi sana Mheshimiwa unataka ukae kwenye *TV* ukawa nyumbani basi unasikia raha kila mtu unamuona kwenye Baraza hili, unajua Mheshimiwa fulani yupo, Mheshimiwa fulani yupo

jinsi hawa ndugu zetu wanavyofanya kazi. Mimi nawapongeza sana kwa juhudi zao na nawaomba moyo wao wazidishe kwa serikali yao kama walivyosema mwakani watalipwa vizuri lakini tuangalie sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kituo hiki siwezi kuamini kama hakijiendeshi kuna mfumo tu haujakaa sawa. Mimi niseme kitu kimoja, juzi niliangalia kituo hiki cha *ZBC*, mimi napenda sana kuangalia kwanza napenda hata king'amuzi changu kikiisha pesa *ZBC* mimi nakuwa napata. Unapata *ZBC* na *TBC* kwa hiyo nikipata *ZBC* mimi inanitosha si lazima kupata vituo vyengine, lakini mimi napata vituo vyote kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti, lakini juzi nimeangalia Mhe. Rais yupo Ujerumani hii ni kupitia *ZBC* taarifa ya habari, yupo Ujerumani anaulizwa na wananchi wale *Diaspora* wa kule kwamba je, Serikali ya Umoja wa Kitaifa itaendelea au haiendelei. Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa umakini wake mkubwa na umahiri mkubwa akasema Serikali ya Umoja wa Kitaifa itaendelea kwa sababu serikali hii imetengenezwa kwa mujibu wa Katiba ya wananchi. Kwa hivyo, lazima iende kwanza kwa wananchi, lakini kwa kuendelea itaendelea. Mimi nampongeza sana Dkt. Shein kwa imani yake na juhudi zake kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tena nilikaa sio *ZBC* sasa kituo kingine *Star TV*, mkutano wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Kibandamaiti anasema kwamba safari hii tukipewa tusipewe tutachukua tu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nasikitika upande mmoja, naangalia vitu vyote lakini wanyonge waliokuwa hawana pesa ya kulipia hawawezi kuona *Star TV* kama mimi, nimeweza kuona nimemsikia Makamu wa Kwanza anasema hivyo, lakini Rais wa Zanzibar nimemsikia Ujerumani anasema Serikali ya Umoja wa Kitaifa itaendelea.

Kwa hiyo, faida ya vyombo vya habari muhimu *ZBC* pia ioneshe kwa sababu wananchi hawapati kuona na hawapati kupima hawa viongozi wanasema vipi, kila mwananchi apate kujua hasa kipindi hiki, tupate kujua vyombo vya habari viweze kuonesha viongozi wetu wanazungumza vipi.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama tofauti mimi nimepata kujua wote wawili, nimepata kupima nani mwenye busara na nchi hii, nani aliyekuwa hana busara na nchi hii. Huyu anayesema atachukua kwa nguvu, mimi naona haitakii mema nchi hii, lakini Rais wa Zanzibar anasema Serikali ya Umoja wa Kitaifa itaendelea. Sasa ukitizama na ukipima vyombo hivi vya habari ni muhimu vyote, sasa tutizame jinsi gani ya kuwasaidia hawa watu wanyonge kuzisikia hizi taarifa za viongozi wetu, wepi wana moyo mzuri wa nchi hii.
Mimi nikitizama vyombo vya habari vilivyonisaidia kupata taarifa, naona Makamu wa Rais lugha aliyoitumia sijaipenda sana, sijafurahi nayo kwa sababu anaonesha

hana imani ya nchi hii, kusema hivyo hapendi amani ya nchi hii. Lakini Rais wa Zanzibar ukitizama kwa mtizamo wake ana imani na anapenda kuishi kwenye Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa, anasema kwa moyo safi kwa ajili ya kuweka amani katika nchi hii. Kwa hivyo, naomba vyombo vya habari hivi Mhe. Mwenyekiti niseme vina umuhimu wake na hasa *ZBC*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, kwa mashirikiano ambayo mmenipatia na hatimae tukaweza kufika hapa. Waheshimiwa Wajumbe, naomba basi kuchukua nafasi hii kuakhirisha Baraza hili hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 16/06/2015 saa 3: 00 za asubuhi.

*(Saa 1:47 usiku kikao kiliakhirishwa mpaka tarehe 16/06/2015 saa 3:00 asubuhi)*